Jumatano Februari 19, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580158
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Utata waibuka vifo vya ng'ombe 1,400 waliokamatwa hifadhini

UKURASA 3



Ukurasa 18

Mkuchika afafanua ushiriki wa nchi utawala bora Afrika

Licha ya ulemavu wa kusikia atangaza atagombea 2020

Ukurasa 15

Kimataifa

siasa

JUMATANO FEBRUARI 19, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Kifo cha mwanamuziki Kizito chaitikisa Afrika Mashariki

Ukurasa 14

Prof. Lipumba tayari kurudi Ukawa ikiwa...

• Aonya kupokea walioenguliwa CCM

Na Sabato Kasika

WAKATI joto la uchaguzi mkuu likiendelea kupanda, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) Taifa, Profesa Ibrahim Lipumba, ameibuka na kuanza kukumbushia uwezekano wa kufufua umoja wa kimkakati uliounda na wapinzani waliojiunga na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Hata hivyo, anataja masharti kwa vyama vya upinzani vinavyohitaji ushirikiano huo wa kimkakati akisema ili kuishirikisha CUF ni lazima wakubaliane naye kuwa hakuna sababu ya kukumbatia waliotemwa na chama tawala.

Mwenyekiti huyo anasema, kama vyama vya Chadema na ACT Wazalendo vinataka CUF iungane navyo, katika uchaguzi mkuu, basi visipokee 'mabaki' yaliyoenguliwa kutoka Chama Cha Mapinduzi.

Kwake ndilo sharti kuu, ambalo kiongozi huyo analitoa wakati akizungumza na wanahabari kwenye makao makuu ya chama hicho, yaliyopo Buguruni Dar es Salaam.

Kiongozi huyo anasema, CUF haiko tayari kuungana au kushirikiana na vyama vingine vinavyosubiria wagombea walioenguliwa na kuonekana hawafai, katika nafasi mbalimbali ndani ya CCM.

Endelea 14

Afrika Kusini; 'siasa kali' yakwamisha kwa muda hotuba ya Rais Ramaphosa

Ukurasa 19

Philip Mangula.

Neno la 'lala salama' madiwani waondokao Ukurasa 17

UKURASA 13

# ZITTO: SIHOFII CHOCHOTE

UKURASA 2



Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (katikati), akisindikizwa na wafuasi wa chama hicho, wakati akitoka kusikiliza kesi ya uchochezi inayomkabili, katika Mahakama ya Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**KIONGOZI WA CCM AKUTWA AMEKUFA KANDO YA BARABARA**
KATIBU wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Kata ya Katoke, Muleba mkoani Kagera, Jaspa Jasson (41), amekutwa amekufa huku mwili wake ukiwa...

**UKURASA WA 25**

**MASWALI LUKUKI KIFO CHA MWIMBAJI INJILI**
MASWALI kadhaa yameibuka baada ya kifo cha msanii wa nyimbo za injili nchini Rwanda, Kizito Mihigo, huku wananchi wakilinyooshea kidole Jeshi la Polisi...

## ULAWITI SASA NI SHIDA NCHINI- 3

UKURASA 4

## Wachambuzi wasema pigo Mashinji kuhama Chadema



UKURASA 2






Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store


**MICHEZO** TWIGA STARS YAONJA MACHUNGU UNAF UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole (kulia), akimpongeza aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, baada ya kuomba kujiunga na CCM, katika Ofisi Ndogo za Lumumba, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto asema haogopi chochote

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amerejea nchini huku akiweka bayana kwamba pamoja na vitisho vyote hakuna chochote atakachofanyiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kurejea, Zitto aliwataka Watanzania wafahamu Tanzania ni ya mfumo wa vyama vingi, hivyo lazima kuwe na tofauti za mawazo, mikakati na mitazamo.

Kurejea kwa Zitto kumethibitisha kauli ya Katibu wa Uenezi wa ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, kuwa kiongozi huyo hajashindwa kurejea nyumbani kwa sababu ya hofu na vitisho anavyovipata bali ni kutokana na afya yake kutokuwa imara na madaktari kumshauri apumzike.

Pia Februari 10, mwaka huu, mdhamini wake, Ray Kimbita, aliiambia Mahakama ya Kisutu kuwa Zitto ameshindwa kufika mahakamani kutokana na kulazwa nchini Marekani.

Baada ya kuwasili nchini juzi, Zitto alisema: "Hakuna kosa ambalo nimelifanya. Nilitekeleza wajibu wangu kama kiongozi wa kisiasa na sina hofu nitaendelea na shughuli zangu kama kawaida."

"Inatakiwa badala ya watawala kutumia dola au vitisho, washindane kwenye hoja, ndilo jambo la msingi ambalo Watanzania wanatakiwa kulifahamu kwa sababu nchi yetu imekuwa ipo siku zote.

"Hapajawahi kuwa na nyakati ambazo watu wana hofu ya mawazo kama kipindi hiki lakini huiondoi hofu kwa kuikimbia, unaiondoa hofu kwa kuikabili ndiyo maana licha ya vitisho vyote nilivyopewa, nimerudi nchini na hakuna chochote watakachoweza kunifanya," alisema.

Kuhusu ziara aliyoifanya nje ya nchi, kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alisema ilikuwa na mafanikio makubwa.

**VITISHO ALIVYOPOKEA**

Januari 31, mwaka huu, bunge liliahirisha shughuli zake kwa muda ili kujadili hoja ya dharura kuhusu madai ya Zitto kuandika barua ya kuzia mkopo wa Benki ya Dunia (WB) kwa serikali ya Tanzania ambao ulikuwa uelekezwe katika elimu.

Mbunge wa Siha (CCM), Dk. Godwin Mollel, alitoa hoja kuwa Zitto aliandika barua kwenda Dunia ya Dunia kutaka fedha hizo zizuiwe licha ya kwamba zilikuwa na manufaa kwa nchi.

Kutokana na hatua hiyo, Dk. Mollel alisema Zitto alikiuka Katiba ya nchi ambayo wabunge wote waliapa kuwa watailinda na kuiheshimu ndipo Spika wa Bunge, Job Ndugai aliposema alivyopima hoja hiyo, aliona ni nzito kwa madai kuwa inahusu usaliti kwa taifa.

Hatua hiyo ya Ndugai na hoja ya Dk. Mollel, viliibua kauli tofauti huku Mbunge wa Kuteuliwa (CCM), Abdalah Bulembo, akisema kwa kitendo hicho, Zitto hatakiwi kurudi bungeni.

"Mimi si mwanasheria, sijui taratibu za kibunge mtu anaposaliti nchi yake anatakiwa kurudi Bungeni humu? Hatakiwi huyu ni msaliti na serikali mko pale wanasheria," alisema Bulembo huku akiungwa mkono na Mbunge wa Ileje (CCM), Janet Mbene na Mary Chatanda wa Korogwe Mjini (CCM).

**AGIZO LA NDUGAI KWA AG**

Kutokana na michango hiyo ya wabunge, Spika Ndugai alisema jambo hilo lina dalili za ujinai, hivyo kumwagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardus Kilangi, kuchukua hatua za kisheria iwapo itaonekana hivyo.

Naye Prof. Kilangi alisema:"Mheshimiwa Spika maelekezo yako, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeyapokea na tutalifanyia kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo."

# Wachambuzi wasema pigo Mashinji kuhama Chadema

**Na Waandishi Wetu**

WACHAMBUZI wa masuala ya siasa nchini, wamesema uamuzi wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni pigo kwa chama hicho na ni funzo kubwa kwa vyama vya upinzani.

Wamesema hatua hiyo inatoa ujumbe kwa vyama vya upinzani nchini kwamba vinapaswa kutengeneza viongozi vyenyewe kutoka ndani ya vyama kuliko kupokea kutoka nje.

Dk. Mashinji jana alitangaza kuhamia CCM ikiwa ni takriban miezi miwili tangu alipoondolewa katika nafasi ya Katibu Mkuu wa Chadema, nafasi hiyo ikichukuliwa na Mbunge wa Kibamba, John Manyika.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, alisema uamuzi wa Dk. Mashinji kuhamia CCM huenda ukawa na athari kwa Chadema kama msomi huyo alikuwa na wafuasi wengi ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Alisema Chadema wanapaswa kujipanga zaidi kutokana na kitendo hicho, japo ni jambo la kawaida kwa wanasiasa kuhama unapokaribia uchaguzi.

"Lakini, ukipoteza mwanachama, kuna nguvu inapungua ndani ya chama, Chadema inapaswa kujipanga na kuzuia wanachama wasiondoke zaidi.

"Unakumbuka mwaka 2015? Wanachama wengi kutoka CCM walihamia Chadema, walikuwa wanajua upinzani unakwenda kuchukua nchi na wao ndiyo ingekuwa fursa ya kupata vyeo, walikosa na wakarudi walikotoka," alisema.

Profesa Gaudence Mpangala wa Chuo Kikuu cha Katoliki cha Ruaha (Rucu), alisema: "Ni jambo la kawaida kwa wanasiasa kuhama hususan wale ambao hawana misingi katika vyama vyao."

Alisema hatua ya Dk. Mashinji kuhamia CCM inatoa funzo kwa vyama vya upinzani akifafanua: "Walipokea wakidhani watanufaika, sasa wanapaswa kutopokea wanachama kutoka vyama vingine na kuwapa vyeo, wajiimarishe wenyewe."

**KAULI YA MASHINJI**

Akizungumza katika Ofisi Ndogo za CCM zilizoko Mtaa wa Lumumba jijini Dar es Salaam jana baada ya kupokewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, Dk. Mashinji alisema:

"Miaka 47 bado ni kijana, kama Rais Magufuli anavyosisitiza, maendeleo hayana chama, hivyo nimwombe Mwenyekiti wa CCM kama ataridhia anikubalie nijiunge na chama hiki."

Alidai CCM ina nia ya kuwapa maendeo wananchi tofauti na chama alichotoka.

"Baada ya kutafakari mwenendo mzima wa siasa na uchumi nchini na kuangalia kwa kina nani wako tayari, nikaona kwa upande wetu Chadema bado tuko mbali sana kuchochea mambo haya ya maendeleo," alidai.

Dk. Mashinji alisema lengo kuu kwa nchi inayoendelea kama Tanzania ni maendeleo na kwamba hatua ya kulumbana asubuhi mpaka jioni iliyokuwa inajitokeza Chadema ni mojawapo ya sababu zilizomwondoa.

Dk. Mashinji aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chadema akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Dk. Wilibrod Slaa aliyeachana na chama hicho siku chache kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwaka 2015.

Dk. Mashinji alikuwa ni Katibu Mkuu wa nne kukiongoza chama hicho tangu kilipoanzishwa baada ya Bob Makani, Dk. Walid Kabourou na Dk. Slaa.

Wakili maarufu katika mikoa ya kaskazini, Martin Kilasara, alisema jana kuwa uamuzi wa Dk. Mashinji kukihama Chadema na kujiunga na CCM ni haki yake ya kikatiba.

## HABARI KITAIFA

# Utata vifo ng'ombe 1,400 hifadhini Maswa

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

ZAIDI ya ng'ombe 1,400 wa wafugaji wa Wilaya za Itilima na Meatu mkoani Simiyu wamekufa katika mazingira yenye utata mikononi mwa maofisa wa Pori la Akiba la Maswa.

Inadaiwa walikufa baada ya kushikiliwa hifadhini kwa miaka mitatu bila kupatiwa huduma muhimu za chanjo, dawa, maji na malisho licha ya Mahakama kutoa hukumu kwa wamiliki kurejeshewa mifugo yao.

Wafugaji hao wamesema tangu mwaka 2017, ng'ombe 1, 484 walikamatwa kwa madai kuwa walikuwa ndani ya pori hilo, na kwamba licha ya Mahakama kuamuru warudishiwe ng'ombe wao, waliendelea kushikiliwa na kuendelea kufa na kubaki 72, hivyo kusababishia umasikini mkubwa.

Wafugaji hao walifikisha kilio hicho kwenye mikutano wa hadhara ilioitishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyefika katika vijiji vya Laini 'A' na Laini 'B' wilayani Itilima, Mwangudo na Malwilo wilayani Meatu mkoani Simiyu ambapo walisema licha ya Mahakama kutoa uamuzi wafugaji hao warejeshewe mifugo, hawajarudishiwa, na kwamba inadaiwa imekufa.

Miongoni mwa wamiliki wa mifugo hiyo ni walioshinda kesi kwa upande wa Itilima ni Malimi Sendama, Ngasa Mbeho, Kongwa Tulutu na Maduhu Mbuli, ambao walimkabidhi Waziri Mpina risiti zinazoonesha mifugo hiyo kuuzwa kwa bei ya kutupa, huku ngombe anayetakiwa kuuzwa kwa Sh. 400,000 hadi Sh. 500,000 akiuzwa Sh. 100,000.

Wafugaji wengine kwa upande wa Meatu waliodhulumiwa ng'ombe 345 ni Subi Maduhu, Masunga Muhamali, Zengo Kusekelwa, Kija Badila, ambao mifugo yao inadaiwa kufa huku mfugaji mwingine akidai ng'ombe wake 55 ambao Mahakama iliamuru alipe faini ya Sh. milioni 1.4 ili arudishiwe mifugo yake na kulipa faini hiyo, lakini mifugo yake haijarudishwa.

Akiwasilisha kilio kwa niaba ya wafugaji hao, Katibu wa Mbunge wa Itilima, Alex Ngulukulu, alisema wahifadhi hao walitoa maelezo kuwa ng'ombe 289 wamekufa, wakati si kweli kwani askari wa hifadhi walikuwa wanaendesha minada ya kuuza mifugo hiyo.

"Ng'ombe walikuwa wanauzwa kwenye minada wakati kesi ikiendelea mahakamani na tuna ushahidi wa kutosha wa risiti zote walizokuwa wanatoa kwa wanunuzi wa mifugo hiyo," alisema Alex.

Diwani wa Kata ya Tindabuligi, Tabu Maghembe, alisema maelezo yaliyotolewa kwamba mifugo hiyo imekufa hawakubaliani nayo kwani hakuna mlipuko wowote wa magonjwa ulioripotiwa katika kipindi hicho, hivyo kumuomba Mpina kufikisha kilio hicho cha wafugaji wa Itilima na Meatu kwa Rais John Magufuli ili aingilie kati kupata haki yao.

Aidha, wafugaji hao walilalamikia kitendo cha maofisa wa Pori la Akiba Maswa kutanua mpaka bila kuwashirikisha wananchi, hivyo kuendelea kupunguza eneo la malisho na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafugaji.

Pia wananchi wa wilaya za Maswa na Meatu wamelalamikia mgogoro wa mpaka katika Ziwa Kitangiri, na kwamba wamekuwa wakizuiliwa kuvua na kukamatwa kwamba wameingia wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida.

Akizungumza baada ya malalamiko hayo Waziri Mpina aliwaagiza Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu kuitisha kikao cha pamoja kitakachomhusisha Mhifadhi Mkuu wa Pori la Maswa, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania na Mwanasheria wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wafugaji wanaolalamikia kudhulumiwa mifugo yao. Aliwataka kupitia vielelezo vyote vilivyotumika kukamata, kutunza na kuuza mifugo pamoja na kupitia hukumu ya Mahakama ili haki iweze kutendeka .

Pia alimuagiza Kamishna wa Ardhi, Mkurugenzi wa Uvuvi Tanzania, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meatu na Mkurugenzi wa Iramba kupitia upya mipaka hiyo na kumaliza kabisa mgogoro huo kuhusu uvuvi katika Ziwa Kitangiri

Waziri Mpina ameagiza wafugaji wote mkoani Simiyu walioshinda kesi mahakamani na kutakiwa kurejeshewa mifugo yao kuwasilisha vielelezo vya hukumu za kesi hizo kwenye ofisi za Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu ili haki iweze kutendeka.

## Kiongozi wa CCM akutwa amekufa kando ya barabara

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

KATIBU wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Kata ya Katoke, Muleba mkoani Kagera, Jaspa Jasson (41), amekutwa amekufa huku mwili wake ukiwa kando ya barabara.

Licha ya kiongozi huyo kukutwa akiwa amefariki dunia katika mazingira ya kutatanisha, mwili wake umeonyesha majeraha ya kujinyonga huku eneo hilo likiwa halina hata mti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema jana kuwa juzi majira ya saa 7:00 mchana, walipata taarifa za kutoweka kwa kiongozi huyo na jana saa 1:30 asubuhi mwili wake kukutwa katika kijiji cha Bisore, wilayani Muleba akiwa amefariki dunia.

"Licha ya mazingira ya mwili huo kukutwa mahali ambapo hakuna mti na kando ya barabara na hakuna alama zinazoonyesha alama za kufanyika vurugu, kilichoonekana ni eneo kufanyika sehemu nyingine," alisema.

"Suala la marehemu kijinyonga au kunyongwa na mtu au watu ambao hawajafahamika na mwili kupelekwa eneo hilo kwa lengo la kupoteza ushahidi halijawa bayana. Hakuna ushahidi mpaka sasa kuonyesha kama kabla ya kufikwa na umauti alikuwa na ugomvi," aliongeza Malimi.

Kamanda Malimi alisema uchunguzi wa daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa aliyeambatana na polisi kwenda kwenye eneo la tukio, unaonyesha kuwa Jasson alifariki dunia baada ya kukosa hewa, hali iliyosababishwa na kukabwa shingoni.

Aliongeza kuwa uchunguzi wa daktari pia ulionyesha dalili zote za kujinyonga kutokana na kuwa na alama za michubuko ya shingoni, kujisaidia ndani ya mavazi, haja kubwa na ndogo.

Kwa maelezo ya mashuhuda, Kamanda Malimi alisema hadi anafikwa na mauti Jasson alikuwa ametengana na mkewe kwa takriban miaka minne kwa kutelekeza familia yake na kuhamia Kijiji cha Bisore kuishi na mwanamke mwingine, aliyejulikana kwa jina la Beatrice Zakaria.

Alisema kutokana na kifo hicho, Jeshi la Polisi limeanza upelelezi ili kubaini chanzo cha tukio hili lenye utata ikiwamo kuwabaini watuhumiwa waliohusika na jambo hilo.


**KUPOTEA KWA CHETI**



ZAWADI WILLIUM HAONGA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2925-0231 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NALYELYE SEKONDARI mwaka 2015.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
KW/RB/986/2020.

156369



IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(COMMRCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM
COMMERCIAL CASE NO 8 OF 2020
GA INSURANCE TANZANIA LIMITED……………………PLAINTIFF
VERSUS
GOLD SHIELD INSURANCE SERVICES (EA) LIMITED……………DEFENDANT
SUBSTITUTED SERVIC E BY PUBLICATION

TO: THE CHIEF EXECUTIVE AND PRINCIPAL OFFICER,
GOLD SHIELD INSURANCE SERVICE (EA) LIMITED,
AZIKIWE/SAMORA,
1ST FLOOR, PLOT NO 8
P.O. Box 8053
DAR ES SALAAM

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has filed a suit against you with particulars set out in the plaint filed in this Court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are directed to collect copies of the summons and plaint from the Court's Registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam. You are ordered to file your written statement of defence within twenty one (21) days of publication of this notice. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 17th day of March, 2020 at 10:00 am when this case will be heard.

TAKE FURTHER NOTICE that should you default to file your written statement of defence and/ or enter appearance as herein provided, the suit will proceed and a decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 13th day of February, 2020.

115636302



# TANGAZO.



HAMADI WAZIRI KIFFERA WA HEDARU MWENYE RB NO- MOS/RB/ 1217/20



GEORGE SAMWELI MRAHAGWAWA DODOMA - MTANANA WILAYA YA KONGWA JIRANI NA KIBAIGWA MWENYE RB NO- MOS/RB/5352/19

WENYE PICHA HAPO JUU, WANATAFUTWA NA MWAJIRI WAO ABDALLAH MSHANA KWA TUHUMA ZA WIZI.

WANAPENDA KUTEMBELEA MAENEO YAFUATAYO DODOMA MJINI, ARUSHA TENGERU, HEDARU MJINI, LUSHOTO, MOMBO NA DAR-ES-SALAAM.

KWA ATAKAYEMUONA/WAONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI AU KUPIGA SIMU NAMBA 0715-268411 .

DONGE NONO LITATOLEWA.

156366



# KUMBUKUMBU

Ilikua Februari 19, 2019 siku ambayo ulitutoka, ikawa dakika, masaa, siku na hatimaye leo umetimiza mwaka mmoja toka mpendwa wetu ulipotwaliwa kwenda mbinguni kwenye makao yako ya milele.

Ni vigumu kwetu kukubali kwamba haupo nasi kimwili, lakini tunafarijika kwa imani kwamba uko nasi kiroho na unaendelea kutuombea huko ulipo, nasi tunazidi kukuombea uendelee kupumzika kwa amani.

Matendo yako yatabaki daima ndani ya mioyo yetu, upendo na amani uliotuachia vitaendelea kuwa mwongozo katika maisha yetu. Mpendwa wetu tulikupenda sana na tutaendelea kukupenda na kukukumbuka daima.



GLORY WALTER MZIRAY
Kuzaliwa 27 Disemba 1977
Kufariki 19 Februari 2019

Unakumbukwa sana na mume wako, watoto wako, wazazi wako, wadogo zako, ndugu jamaa na marafiki.

Ibada ya kumbukumbu kumshukuru Mungu tangu alipomtwaa mpendwa wetu marehemu Bi Glory Walter Mziray itafanyika Jumamosi tarehe 22 Februari 2020, nyumbani kwa wazazi wake, Mikese, Morogoro kuanzia saa 5 asubuhi. Wote mnakaribishwa.

Uendelee kupumzika kwa amani mpendwa wetu Glory Walter Mziray.

**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA, JINA LAKE LIHIMIDIWE MILELE. AMINA**

*2 TIMOTHEO 4:7*

115635102

RIPOTI MAALUM - 3

# Kadhia ya ulawiti inavyotesa wanafunzi

## ■ Wizara yaanika mikoa vinara
## ■ Adhabu kifungo cha maisha jela

*SEHEMU ya pili ya ripoti hii jana, ilianika kilio cha walimu, wazazi na wadau wa jamii kuhusu vitendo vipya vya ulawiti dhidi ya wanafunzi wa shule za msingi wilayani Mkuranga mkoani Pwani. Endelea na sehemu ya mwisho kujua mengine yaliyojificha katika kashfa hiyo:..*

Neema Nyasulu, Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Kimanzichana, alisema ana taarifa za vitendo hivyo kufanyika miongoni mwa wanafunzi wenyewe au wanafunzi kutendwa madhila hayo na ndugu zao wanapokuwa mazingira ya nyumbani.

"Unajua suala la ulinzi na usalama wa mtoto linahitaji mshikamano. Katika maeneo haya, sisi tunapata tabu sana, wazazi wengi wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kulea watoto, japo kila mara huwa tunajitahidi kupita na kuwapa elimu," alilalamika. Ofisa katika Dawati la Jinsia Wilaya ya Mkuranga, Anna Zella, alikiri kuwa na taarifa za kufanyika kwa vitendo hivyo katika baadhi ya shule na tayari wameanza kutoa elimu kwa wanafunzi katika shule hizo.

"Ni kweli tuna taarifa za matukio haya, yapo kwenye baadhi ya shule. Tuna taarifa kutoka shule za msingi... (alitaja majina ya shule tatu), tumeshazifikia na kutoa elimu na kesi nyingi haziripotiwi, ingawa kwa sasa naona wameanza kutoa taarifa baada ya kuwapa elimu," alisema.

**VIGODORO**

Nipashe ilizuru katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mkuranga na kuzungumza na ofisa wake, Foibe Peter, ambaye alikiri kuwapo kwa vitendo hivyo katika shule nyingi za eneo lake la kazi. Ofisa huyo aliitaja Nipashe majina ya shule nne za msingi (tunazihifadhi), ambazo zimeripotiwa kwenye ofisi yake kuwa na matukio ya watoto ama kutendwa au kutendeana wenyewe madhila hayo.

Peter alisema anafikiri umaskini, mila na desturi za maeneo hayo zinachangia kushamiri kwa vitendo hivyo, kidole chake akikielekeza zaidi kwa wakazi wanaruhusu watoto kushiriki katika ngoma maarufu ukanda wa Pwani ya 'kigodoro', huku baadhi yao wakishindwa kutekeleza ipasavyo malezi ya watoto kutokana na kutengana.

"Asilimia kubwa ya eneo hili wanashikilia zile tamaduni za kucheza watoto, na wanapokuwa wanacheza michezo hiyo, watoto nao wanaona.

"Na ukiangalia michezo yao, ni ya aibu sana, haifai hata mtoto aone kwa sababu akitoka hapo na yeye anaenda kujaribu na pia inambomoa badala ya kumjenga hata kama alikuwa na tabia njema.

"Wakati mwingine hali ya umaskini nayo inakuwa tatizo, baadhi ya wazazi huwa wanalala chumba kimoja na watoto wao. Unaweza kufikiri mtoto amelala, kumbe anaona na mwisho wa siku ndiyo hivyo, wanajaribu na wao, na kibaya zaidi wanaenda kujaribishia kwa watoto wenzao bila kujua kama kuna madhara," alibainisha.

Ofisa huyo wa serikali alibainisha kuwa katika kipindi cha miezi mitatu kilichoanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana, kulikuwa na mashauri 27 yaliyoripotiwa ofisini kwake kutoka mamlaka mbalimbali wilayani humo kuhusu watoto kufanyiwa ukatili wa kingono na kulawitiwa. Kati yao, sita ni wavulana na 21 ni wasichana.

**DED ANENA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mshamu Munde, alisema: "Siwezi kusema tatizo la watoto kufanyiana vitendo viovu lipo au halipo, lakini ninachotaka kusema ni kwamba suala la malezi ya watoto linahitaji ushirikiano kwa pande zote, huwezi kumwachia mtu mmoja."

Munde alikiri kuwapo kwa kikwazo cha uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali wilayani humo na wako kwenye mkakati wa kusaka ufumbuzi.

"Ikumbukwe kwamba uhaba wa vyumba vya madarasa unatokana na kuongezeka kwa wanafunzi ambayo ni matunda ya elimu bure, sasa hivi wazazi wengi wanajisikia furaha na amani kupeleka watoto wao shuleni tangu ulipoletwa utaratibu huu. "Na hakuna wanaoishia njiani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambako wanafunzi wengi walikuwa wakipata matatizo ya kiuchumi katika familia zao na kulazimika kukatisha masomo. Sasa hamna mambo hayo na ndiyo maana mahitaji ya vyumba vya madarasa yanakuwa makubwa.

"Tunafahamu pia kwamba shule nyingi hazina uzio na huenda nalo likawa chanzo cha vitendo hivyo, lakini kwa sasa ni lazima tuangalie namna ya kutatua vyumba vya madarasa ambavyo ni muhimu zaidi. Hatuwezi kusema kwa sasa tunaweka uzio katika shule wakati bado tunaumiza kichwa kwenye tatizo hilo la msingi," alisema.

**KAULI YA WIZARA**

Nipashe ilimtafuta Mkurugenzi wa Maendeleo ya Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, ambaye alibainisha kuwa tatizo la vitendo vya ulawiti dhidi ya watoto ni kubwa na halifanyiki Mkuranga tu, bali maeneo mengi nchini.

"Tatizo la ulawiti kwa watoto nchini ni kubwa na si Mkuranga pekee, linafanyika maeneo mengi nchini. Zamani vitendo kama hivi vilikuwa ni siri, watu walikuwa wanaogopa kutoa taarifa, lakini huenda tunaona kwamba vimeongezeka kwa sababu watu wanatoa taarifa kwa wingi sasa hivi," alisema.

Magwiza aliweka wazi kuwa katika takwimu zao kwa mwaka ulioishia Desemba 2019, Mkoa wa Tanga ulikuwa unaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya vitendo hivyo na Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa kinara kwa mwaka 2018.

Alisema tayari wameanzisha kampeni waliyoipa jina la 'Twende Pamoja', inayoendeshwa nchi nzima kwa lengo la kutoa elimu ya kukomesha vitendo hivyo.

"Baada ya kuona vitendo hivyo vimezidi kuripotiwa, tumeanzisha kampeni hiyo, tunashirikiana na halmashauri zote na madawati ya jinsia, tunatoa elimu ya kupambana navyo ili kuvikomesha.

"Sisi tunajua kuna ukatili wa watoto unaoendelea kwenye maeneo mengi, na tuna kampeni tumeanzisha, kuna mifumo mbalimbali tumeanzisha kwenye halmashauri na vijiji ambazo ni kamati za ulinzi kwa wanawake na watoto, lakini tunahamasisha kuanzishwa kwa madawati ya ulinzi shuleni ili kuwalinda watoto hawa," alibainisha hatua zinazochukuliwa.

**KIFUNGO CHA MAISHA**

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inaitaka serikali, wazazi, walezi na jamii kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

Pia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) ambao Tanzania imeridhia kwa kutia saini, unazitaka serikali za nchi husika kuchukua hatua za kisheria na kiutawala ili kuwaepusha watoto dhidi ya unyanyasaji wa kimwili, kiakili, mateso na udhalilishaji.

Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) iliyoangazia kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2018, ilibainisha kuwa watoto 2,365 walibakwa nchini, sawa na watoto 394 kwa mwezi na watoto 13 kwa siku.

Vilevile, Ripoti ya Hali ya Uhalifu Tanzania kwa mwaka 2017 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ilibainisha kuwa katika kipindi cha miezi 12 ya mwaka huo, matukio ya uhalifu dhidi ya watoto yalikuwa 13,457.

Wakili Leonard Manyama, katika ufafanuzi wake wa kisheria kwa Nipashe kuhusu aina hiyo ya ukatili, alisema kifungu cha 131 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16, kinatoa adhabu ya kifungo cha maisha kwa mtu yeyote anayekutwa na hatia ya kubaka au kulawiti mtoto.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

**HABARI KITAIFA**

# Ewura yawaonya mawakala wasambazaji gesi za kupikia

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imewataka wasambazaji wakubwa wa gesi za kupikia (LPG), kufuata masharti na kanuni kinyume chake watafutiwa leseni.

Meneja wa Ewura Kanda ya Mashariki inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara, Injinia Nyirabu Musira, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati mamlaka hiyo ilipokutana na kundi hilo.

Lengo la mkutano huo ni kuangalia kanuni zinazosimamia biashara hiyo na jambo la pili, mamlaka hiyo iliwaelekeza namna ya kuomba leseni ya biashara kwa wasambazaji wakubwa.

Musira alisema lipo ongezeko la matumizi ya LPG na mwaka 2010 tani za ujazo 20,000 ziliingizwa nchini na mwaka 2018 ujazo uliongezeka na kufikia zaidi ya 140,000. "Kukiwa na ukiukwaji wa kanuni, Ewura inayo sheria inayotoa nguvu kwetu kutoa adhabu na kushtaki, maagizo tunayotoa yana nguvu sawa na ya Mahakama Kuu na ukiukwaji ukiwa mkubwa tunaweza kufuta leseni," alisema.

Musira alisema lengo la kukutana na wasambazaji hao ni kuwaeleza kuhusu kanuni za uendeshaji wa biashara ya LPG ambazo zilikuwapo tangu mwaka 2012 na kufanyiwa mapitio mwaka 2018.

"Leo tumekaa pamoja kujenga uelewa kuhusu kanuni kabla hatujaingia kwenye utekelezaji wake, maeneo makubwa ya maboresho ni kuangalia biashara ya LPG kuweka mazingira au mikataba kati ya wasambazaji wakubwa na wadogo. Tunafahamu LPG sasa hivi inasambazwa mpaka maeneo ya ndani ya vijijini hivyo wapo wengi hivyo ni vizuri kuwapo mikataba ambayo itawasimamia wasambazaji wakubwa na wadogo."

Pia alisema wanaweka mazingira ambayo wote wanaofanya biashara hiyo wanaifanya kwa kufuata masharti ya leseni inayotolewa na mamlaka hiyo.

Kuhusu malalamiko ya mitungi ya gesi kuisha haraka, Musira alisema miongoni mwa mambo yanayosisitizwa na kanuni hiyo ni wawafanyabiashara lazima wawe na mzani.

Alisema matumizi ya kanuni hiyo yameshaanza kutumika na kuwataka kila mmoja kufuata masharti.

Akizungumzia bei ya gesi hizo, alisema changamoto iliyopo ni kununuliwa kulingana na soko lililopo kutokana na kutokuwa na uingizaji wa pamoja wa LPG.

"Bei hutokana na gharama za ununuzi sasa kwa sababu hufanywa tofauti na kila muuzaji kumekuwa na changamoto ya kuweka bei kikomo, mamlaka inaangalia hilo kwa umakini na kuona ifike mahali kuwe na uagizaji wa pamoja na kujua bei kuingiza na kuuzia," alisema.

Msambazaji mkubwa gesi kutoka kampuni ya Taifa Gas Tanzania mkoa wa Mtwara, Rashied Omary, alisema kanuni hizo za Ewura ni mpya kwako na kwamba inawezekana lengo ni zuri, lakini ipo changamoto katika utekelezaji.

"Umuhimu mkubwa ulikuwa kwanza kuwahamisha wananchi waachane na nishati za mkaa na kuni kwa sababu bado kuna uwelewa mdogo wa matumizi ya gesi kwa mikoa ya pembezoni," alisema. Alisema kanuni hizo zinabana mwitikio wa wasambazaji wakubwa wa gesi kuwekeza katika biashara hiyo.

"Masharti ni mengi mno, leo hii unatakiwa uombe taratibu zipo nyingi mno kwa mtu ambaye yupo maeneo ya pembezoni ninakotoka sidhani kama atahamasika kuwekeza katika biashara hii," alisema.

Alisema matokeo yake badala ya kumfanya mwananchi ahamasike kutumia gesi itakuwa ngumu kwa sababu kunahitajika uwekezaji mkubwa kwa msambazaji.

"Uwekezaji kwa msambazaji na kampuni unatakiwa uwe na kiwango cha chini cha Sh. milioni 30 cha kuwekeza katika biashara hii, leo Ewura inakuja na masharti mengine ambayo nayo ni gharama," alisema.

## Atozwa faini 300,000/- kuua mke bila kukusudia

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma imemhukumu kulipa faini ya Sh. 300,000 mkazi wa Kijiji cha Kiyungwe, wilayani Kasulu kwa kosa la kumuua mke wake kwa kipigo, Agosti 15, mwaka 2018.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo Wakili wa Serikali, Happy Mayunga, alidai mshtakiwa Msafiri Ntarakila (68) alitenda kosa hilo usiku baada ya kurudi nyumbani kwake akiwa amekunywa pombe na kukuta mke wake hayupo nyumbani.

Mayunga alidai mshtakiwa baada ya kumkosa mke wake alimtafuta na kumpata ndipo alipoanza kumpiga sehemu mbalimbali za mwili hatua iliyosababisha mwanamke huyo kuvuja damu nyingi kutokana na majeraha.

Alidai kuwa watu wanaoishi karibu walisikia kelele na kwenda kutoa msaada wa kumpeleka hospitali mwanamke huyo ambaye hata hivyo alipoteza uhai akiwa njiani.

Awali Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Ivin Mugeta, anayesikiliza kesi hiyo alimhoji mshtakiwa kama alitenda kosa hilo na mshtakiwa alikiri kutekeleza mauaji ya mke wake.

Wakili upande wa utetezi, Sadiki Aliki, alimwomba jaji kutoa maelezo kuhusu ya mteja wake na alidai kuwa alimwambia kuwa aliua bila kukusudia baada ya kuibuka ugomvi na kwamba anaomba mashtaka yake yabadilishwe kutoka kuua kwa kukusudia hadi kuua bila kukusudia.

Upande wa mashtaka ulikubaliana na shtaka lake liwe la kuua bila kukusudia.

Kutokana na mshtakiwa kukiri kosa, upande wa Jamhuri uliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kama funzo kwa mshtakiwa na jamii. Wakili wa upande wa utetezi, Aliki aliiomba mahakama kupunguza adhabu kwa mshtakiwa kutokana na kosa hilo kuwa la kwanza, mazingira ya kosa kuonyesha si ya kukusudia, umri wake wa miaka 68 pamoja na kutegemewa na familia ya wajukuu watano.

"Nimezingatia utetezi wa kosa ulilolifanya na umri ulionao hivyo mahakama hii inakuhukumu kulipa faini ya Sh. 300,000 kama utaipata na ukiikosa basi utatumikia jela miaka mitatu," alisema Jaji Mgeta.


**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ**

**ADRIANO STEPHEN KIMBALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC 949 BVJ AINA YA PIAGGIO APE. Chassis namba MBX0902CFVK537231. Engine namba TBPDMKV3004728.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/553816/2019.**

156361

**JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA HATI YA KIAPO**

Mimi LEWIS HAMZA MSUMARI wa TANGA, nikiwa na akili zangu timamu nimefika mbele ya Hakimu kutamka yafuatayo:

1. Kwamba mimi ni mmiliki wa kiwanja Na. 69, kitalu"E" kilichopo Makororakati-Tanga.
2. Kwamba, Hati ya kiwanja hicho imepotea na nimefanya jitihada ya kuitafuta bila mafanikio, nimefika Polisi kutoa taarifa na kupewa Loss Report TAN/RB/153334/2020.
3. Kwamba kwa kiapo hiki naomba Ofisi ya Mipango Miji Tanga iweze kunipatia hati nyingine ya umiliki wa kiwanja tajwa hapo juu ili niweze kulipia Ada za serikali

UTHIBITISHO:
Nathibitisha kuwa yote niliyo yatamka hapo juu ni kweli, kweli tupu kwa kadri nijuavyo kwa sheria za viapo.

115636802

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MARTIN EDWARD MUGANYIZI,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN DATSUN, Namba T244AFS, lenye chassis No.D21424561, Engine No. NA1607570W. Kadi ilipotea na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 6/10/2019 na kupewa No: KAG/BUK/RB/563467/2019.

Kwa yeyote atakayeiona aipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye. Au awasiliane naye. No: 0767290501.

156360

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA**
**MAHALI MASWA**
**RUFAA NO. 02 YA MWAKA 2020**
**KATI YA**
**MAYUNGA KANYUMBA………………..MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**NSHOMA LUGOYE…………………..MJIBU RUFAA**

**WITO/TAARIFA**
**KWA: NSHOMA LUGOYE POPOTE ALIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Rufaa dhidi yako katika Baraza hili la ardhi Wilaya ya Maswa. Maelezo ya Rufaa yanaweza kupatikana hapa barazani. Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi kabla ya tarehe 23/03/2020.

Pia unafahamishwa kuwa Rufaa hii imepangwa kusikilizwa tar 23/03/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.F Kanyerinyeri Mwenyekiti baraza la ardhi na nyumba Wilaya ya Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza rufaa hiyo upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 06/02/2020.

J.F KANYERINYERI
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA.

215635002

**KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA**

**MENGI KIRUBA RISASI** anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja **PLOT NO. 30 BLOCK 'Q' MAPINDUZI NORTH MANISPAA YA DODOMA** iliyotolewa na **Wizara ya Ardhi kwa Na.10250.**

Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi **DOM/RB/1306/2018.**

215634602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi Na.14/2020**

**Ombi la PAULINA DAUDI Kuteuliwa**

Msimamizi wa mirathi Marehemu ATHUMAN HAMISI WALA

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 2/3/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimsmizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Sahihi ya Hakimu

215634702

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA**

PILI ABDALLAH AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA ABDALLAH AMANI MKAZI WA KOLANDOTO MANISPAA YA SHINYANGA.

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 3 KITALU "L" MAJENGO MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2007 MAENEO YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA PILI ABDALLAH KWA SIMU NAMBA 0685041125 AU 0688565964

RB NAMBA SHY/RB/2019, CONTROL NAMBA 9910811747665

JACOB NKONUKA
AFISA ARDHI
SHINYANGA.

AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

215634302

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**Katika Mahakama ya WILAYA YA TEMEKE**
**MIRATHI Na; 04/2020**

**Maombi ya Baraua za usimamizi wa Mirathi ya Marehemu STANSLAUS BARONGO MANUMBU na MICHAEL STANSLAUS MANUMBU Waombaji**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji hapo juu .

Mapingamiza yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa 03 mwaka 2020

Imewasilishwa JUMATATU leo tarehe 17 mwezi wa 02/2020.

156353

**KUPOTEA KWA CHETI**



**THECLA DAMIAN KALENGA** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.0639-0082 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia UDZUNGWA SEKONDARI mwaka 2007.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOM/RB/12981/2019**

115633402

**KUPOTEA KWA CHETI**



**ZAHARA SAIDI ADAMU** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.4791-0033 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MSAJE SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MS/RB/8202/2019.**

115633402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuwanusuru watoto wetu dhidi ya ulawiti

**UCHUNGUZI** uliofanywa na Nipashe katika shule za msingi, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, umebaini kuwapo kwa shida kubwa ya wanafunzi kulawitiana wenyewe kwa wenyewe.

Katika uchunguzi huo, ambao ripoti yake imechapishwa gazetini kuanzia Jumatatu hadi leo, wanafunzi wanaofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili, wengi wao ni wa darasa la pili, tatu na nne.

Mmoja wa mwanafunzi aliyefanyiwa kitendo hivyo, alieleza kwamba wengi wanaowafanyiwa wenzao vitendo hivyo ni wa darasa la saba.

Alieleza kwamba wanaofanya vitendo hivyo wamekuwa wakiwavizia wenzao wanapotoka shuleni jioni kurudi majumbani mwao, wakati wa mapumziko au kabla ya kuingia darasani kwa sababu baadhi huingia kwa kupishana (shift).

Mbali na wanafunzi kuzungumza, pia mamlaka zote husika za kiuongozi katika wilaya hiyo ya Mkuranga, zilikiri kulifahamu tatizo hilo.

Walimu wa shule zilizofikiwa wakati wa uchunguzi huo, nao walikiri kuwapo kwa shida hiyo katika shule wanazofanyia kazi, huku wakisema walibaini tatizo hilo baada ya baadhi ya wazazi wa watoto kuripoti na wanafunzi kutajana wenyewe.

Walimu hao walisema baada ya kuripotiwa kwa baadhi ya wanafunzi kufanyiwa ulawiti, waliamua kuitisha ukaguzi kwa wanafunzi wote katika shule hizo na ndipo walibaini hilo kwa sababu wanafunzi wenyewe walitaja mtandao wao unaofanya na kufanyiwa vitendo hivyo viovu.

Walimu hao walisema baada ya kubaini hilo, walianzisha mpango wa kuwadhibiti hususani kwa kujenga tabia ya kutembelea maeneo ambako wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo.

Miongoni mwa sababu zilizotajwa kuchangia kasi ya tatizo hilo ovu, ni pamoja na mila na desturi za eneo husika hususan za watoto kufundishwa masuala ya vigodoro.

Sababu nyingine ni wazazi kushindwa kuwajibika ipasavyo katika malezi ya watoto wao pamoja na ukosefu wa uzio katika baadhi ya shule hizo. Tukio hilo na mengine yanayofanana na hayo si mema kwa ustawi wa afya ya mtoto pamoja na haki zake zote za msingi zinazomtambua na kumlinda.

Mtoto ana haki ya kulindwa, haki ya kupata elimu na haki nyinginezo ambazo kila mtu kuanzia mzazi, jamii na serikali kwa ujumla wanapaswa kuzisimamia na kuhakikisha anazipata.

Tunafahamu kwamba kufanyiwa vitendo vya ulawiti kwa mtoto kunamwathiri si tu kiafya, bali pia kiakili na kisaikolojia na maendeleo yake katika taaluma.

Na kwa sababu hiyo, kuna hatari ya mtoto anayefanyiwa hayo, kushindwa kufanya vizuri kitaaluma na hata kutokufikia na kutimiza ndoto zake katika siku za mbeleni.

Mambo haya yote wanatakiwa kuyafahamu makundi yote yanayohusika na maendeleo ya mtoto huyo, na kuhakikisha wanamlinda dhidi ya kadhia zozote mbaya.


Tunawashauri wazazi na walezi wahakikishe wanatimiza wajibu wao wa malezi mema na yenye maadili kwa mtoto ili kuepusha mtoto huyo kuingia kwenye madhila hayo.

Jamii nayo inatakiwa kuwa na hofu ya Mungu, na kumlinda mtoto yeyote wanapoona kuwapo kwa viashiria vya kumdhuru au kumwathiri, ikiwezekana kutoa taarifa wanapowabaini watu waovu wanaosababisha madhila kwa watoto.

Serikali nayo unao wajibu wa kuhakikisha inaboresha miundombinu kama uzio, ambayo itasaidia hata kama kwa kiwango kidogo kupunguza mianya ya watoto kutoka shuleni hususani wanapopumzika na kwenda kufanya mambo hayo au kushawishiana.

Kadhalika, mamlaka husika zikiwamo Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mshtaka na Mahakama kuhakikisha kwamba wanaharakisha kesi za vitendo hivyo na wanaobainika kutenda uovu huo kuadabishwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wananchi changamkieni kujiandikisha kwenye BVR

**OKTOBA** mwaka huu ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, ambao utafanyika kwa mara ya sita, ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kwa sasa yapo mambo kadhaa yanayoendelea kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo, mojawapo ikiwa ni uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, ulioanza mwanzoni Desemba mwaka jana.

Uandikishaji huo unaendelea, katika maeneo mbalimbali nchini, ili kuhakikisha watu wote wenye sifa za kuchagua viongozi wanajiandikisha na kupata kadi ya kuwawezesha kuwachagua viongozi wanaowataka. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), ilishatoa ratiba ya uandikishaji huo kwa kila mkoa, na sasa waandikishaji wapo jijini Dar es Salaam, wakiendelea na kazi hiyo ambayo ni inaanzisha mwendo wa uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu. Uzinduzi rasmi wa uboreshaji wa daftari hilo ilifanywa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Julai mwaka jana, huku akihimiza vijana waliotimiza umri wa miaka 18 kujitokeza kwa wingi kujiandikisha.

Vijana wanatajwa kuwa walengwa wakuu kwa vile wanaingia kwa mara ya kwanza katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu, hivyo ni muhimu wachangamkie daftari hilo.

Kwamba, bila kujiandikisha hawataweza kutumia haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka, hivyo kujiandikisha kutawahakikishia ushiriki wao katika uchaguzi wa viongozi.

Kwa maelekezo hayo, wanaotakiwa kujiandikisha wamo wale ambao hawakujiandikisha mwaka 2015 ingawa walikuwa na sifa, na pia kutoa kadi mpya kwa waliopoteza na hata zilizoharibika. Mbali na hayo, kingine ni kuhamisha taarifa za wapigakura waliohama kata au majimbo na kwenda maeneo mengine ya kiuchaguzi, kurekebisha taarifa za wapigakura zilizokosewa, yakiwamo majina.

Vilevile kinachoendelea sasa katika uboreshaji wa daftari hilo, ni kuondoa wapigakura waliopoteza sifa kama vile waliofariki dunia, lakini kikubwa zaidi ni vijana kutambua haki yao hiyo na kuitumia inavyotakiwa. Kimsingi ni kwamba kujiandikisha BVR ni hatua muhimu kuliko hata pengine kuliko kuwa mwanachama wa chama cha siasa, kwani hata wasio na vyama wanapigakura ili mradi wawe wamejiandikisha katika daftari hilo.

Mwaka huu wa 2020 ni wa uchaguzi mkuu, hivyo ni vyema pia kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura akaelewa kile ambacho anapaswa kukifanya na hasa kutambua kuwa ana haki ya kuchagua kiongozi anayemtaka. Vijana wanahimizwa kujitokeza kujiandikisha kwa wingi, kwa sababu kuna hatua kadhaa ambazo ni muhimu wakazielewa ili mwisho wa siku wasije kubaki wakilalamika baada ya uchaguzi.

Kwanza ni vyema wakajua kuwa katika suala la uchaguzi au kupigakura laweza kuwa ni wajibu wa kila Mtanzania mwenye sifa, hiyari na haki, hivyo ni hayo yanatakiwa kutimizwa inavyotakiwa.

Kwa mfano kujiandikisha kwa hiari, kunamaanisha kufanya hivyo bila kusukumwa au kushurutishwa, lakini uhiari huo usimfanye mtu akaacha kutumia haki yake ya kuchagia kiongozi anayemtaka.

Mtu anaweza kuchukulia tu kwamba, kwa vile kupiga kura ni suala la hiari, basi haoni sababu yoyote ya kujiandikisha katika daftari hilo, au kwenda kushiriki kwenye uchaguzi.

Lakini ukija kwenye suala haki, ni kufanya jambo kwa usahihi, yaani kwa kufuata taratibu na hata kanuni zilizowekwa, pamoja na hayo, haki inaambatana na wajibu.

Hivyo, ili mtu apate haki, ni lazima atimize wajibu, hata katika uchaguzi yaweza kuwa ndivyo ilivyo, kwamba mtu hapaswi kudai haki kutoka kwa uongozi usiofaa, kwa sababu hatimizi wajibu wa kupiga kura.

Kura ndiyo inayoweza kusaidia kuepusha kupata viongozi wabovu au wasiofaa, hivyo ni wajibu, hiari na haki kwa vijana wenye sifa kujiandikisha.

Pamoja na hayo, wanatakiwa kutambua kuwa katiba ya Tanzania inampa haki kila raia kuchagua na kuchaguliwa.

Hivyo watumie haki hiyo ya kikatiba kujiandikisha kwa wingi, ili hatimaye wachague viongozi wanaowataka na pia wale wanaotaka kuwania uongozi, watumie haki hiyo.

Kwa maana nyingine ni kwamba watu kutoshiriki, katika uchaguzi inakuwa ni sawa na kujinyima haki yao wenyewe ya kupata viongozi wa kuwakilisha kwenye vyombo vya maamuzi kama bunge.

HABARI KITAIFA



Ofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Neema Urio, akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (kushoto), kuhusu uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika kituo cha Kivukoni, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali kugawa vifaa kuzuia athari za zebaki

**Na Robert Hokororo,** IKUNGI

WAKATI serikali inaendelea kuweka utaratibu wa kupata mbadala wa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, imeshauri watumie vifaa vinavyowakinga wakati wakifanya shughuli hizo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, alitoa rai hiyo jana, alipozungumza na wachimbaji wadogo kwa nyakati tofauti katika vijiji vya Sambaru wilayani Ikungi na Londoni wilayani Manyoni mkoani Singida.

Sima alisema serikali inaendelea na kuwapa elimu wachimbaji hao katika maeneo mbalimbali nchini ili waepuke madhara ya kiafya yanayotokana na kemikali hiyo.

"Tanzania tuliridhia Mkataba wa Minamata mwaka jana, unaotaka kupunguza ama kuondoa kabisa matumizi ya zebaki kwa ninyi wachimbaji ili kuwaepusha madhara ya kiafya na kimazingira katika maeneo yenu," alisema.

Akiwa katika ziara hiyo, Sima alitembela na kuona shughuli za uchimbaji na kukagua namna wanavyotunza mazingira, akieleza kuwa jukumu la serikali ni kutoa elimu juu ya madhara ya zebaki ili kulinda afya za wachimbaji wadogo.

"Niwaahidi tu, tutashirikiana na Ofisi ya Madini ili mpate vifaa maalum vya kujikinga wakati wa kuchenjua badala ya mikono, tutawaletea gloves mvae mikononi na maski wakati tunachoma ili kufunika pua kwani kemikali hii ina madhara kiafya," alisema.

Naibu waziri huyo aliwataka wachimbaji hao kuacha kukata miti wakati wa shughuli za uchimbaji wa dhahabu na badala yake wawe na utamaduni wa kutumia njia mbadala kama ambavyo wanavyoelekezwa na mamlaka zinazohusika.

Aliongeza kuwa jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais na serikali kwa ujumla ni kuhakikisha nchi inakabiliana na matatizo ya mabadiliko ya tabianchi. Alisema kuendelea kuchoma na kukata miti ovyo, kulima kiholela na kuchimba mashimo ovyo kwa ajili ya madini, kutasababisha mvua isinyeshe na jua kuwa kali kuliko kawaida.

# Waziri ataka mgogoro wa mpaka kumalizwa

**Na Lusungu Helela,** UKEREWE

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kumaliza mgogoro wa mpaka katika Msitu wa Hifadhi ya Negoma kwa kuwaachia wananchi wanaoishi ndani ya msitu huo hekta 27 kwa ajili ya makazi.

Hatua hiyo inakuja kutokana na mgogoro wa mpaka kati ya wananchi wenye kaya 57 kuwa ndani ya msitu huo wenye ukubwa wa hekta 650 ambao ni mali ya halmashauri unaotunzwa kwa ushirikiano na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Kaya hizo zinadai kuwa zilikuwapo katika eneo hilo tangu mwaka 1939 na halmashauri hiyo ilipoingia ubia na TFS mwaka 2015, haikushirikishwa kwenye kubaini mipaka halisi ya msitu huo.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Negoma juzi, Kanyasu aliiagiza TFS kugharamia upitiaji wa mipaka wa msitu huku halmashauri itoe wataalamu kwa ajili ya kupima mipaka upya kwa kuzitoa nje hekta hizo 27.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2012, Ukerewe ilikuwa na watu 300,000 lakini kwa sasa inakadiriwa ina zaidi ya watu 450,000 wanaoishi katika kisiwa hicho chenye ukubwa wa kilomita za mraba 530. Kutokana na ongezeko hilo, Kanyasu alisema ni vigumu kuwaondoa wananchi wenye makazi ndani ya msitu hifadhi kutokana na ufinyu wa ardhi.

Alisema licha ya mgogoro huo wa mpaka kudumu kwa zaidi ya miaka 10, kimsingi kulikuwa na mgogoro kati ya wananchi na halmashauri hiyo na si baina ya TFS na wananchi.

Licha ya eneo hilo ambalo halmashauri imeagizwa kuwaachia wananchi kuwa na miti aina ya mikaratusi yenye umri wa miaka mitano iliyopandwa na TFS, Kanyasu aliwataka wananchi hao wasiikate miti hiyo badala yake itakatwa na TFS baada ya kufikia muda wake wa kuvunwa.

Sambamba na hilo, Kanyasu aliwataka wananchi kuwa majirani wema kwa kujiepusha kuendesha shughuli za kibinadamu ndani ya msitu huo badala yake wautumie kwa kufuga nyuki. Katika hatua nyingine, Kanyasu alizitaka halmashauri zilizokuwa na misitu, kuingia ubia na TFS ili kupanda miti katika maeneo hayo.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Hamad Kwendela, alisema katika mchakato wa kuingia ubia kati ya halmashauri na TFS, hawakushirikishwa ili kubaini mipaka halisi.

"Tunashukuru kwa uamuzi huu kwani tunapenda misitu, hivyo tunakuahidi tutakuwa walinzi wa msitu huu," alisema Kwandela.

**Kaya hizo zinadai kuwa zilikuwapo katika eneo hilo tangu mwaka 1939 na halmashauri hiyo ilipoingia ubia na TFS mwaka 2015, haikushirikishwa kwenye kubaini mipaka halisi ya msitu huo.**


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AccessBank Tanzania Limited** imetoa idhini kwa Madalali wake Kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara, Magari, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi nne(14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KARIAKOO MKUNGUNI | MAHENGE/ BENSON,MI CHAEL | MMUYA/G ERION,JO ACHIM | HOUSE | TMK036715 MTONI KIJICHI,MBA GALA KUU | 7/03/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

### MASHARTI YA MNADA

Dhamana zitauzwa mahali zilipo. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.

Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**MAWASILIANO: ACCESSBANK TANZANIA – 0677 860 000**

215637102

# Waathirika mafuriko Isimani wasaidiwa

Na Moshi Lusonzo

WAKAZI wa Jimbo la Isimani mkoani Iringa, ambao wameathirika na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha nchini, wamepewa msaada wa vyakula na nguo ili kukabiliana na mazingira magumu.

Msaada huo umetolewa na Sunshine Group jijini Dar es Salaam jana kwa lengo la kusaidia watu wanaoishi nje ya makazi yao, baada ya nyumba zao kuzolewa na maji katika mafuriko yaliyotokea eneo hilo mwezi uliopita.

Makamu Mwenyekiti wa Sunshine Group nchini, Betty Mkwasa, alisema msaada huo unajumuisha vyakula mbalimbali, mafuta ya kupikia, nguo na blanketi.

"Sunshine Group inayojumuisha kampuni mbalimbali zilizopo nchini, tumeona tuna wajibu wa kusaidia ndugu zetu walioathirika na mafuriko katika Jimbo la Isimani," alisema Betty.

Alisema kampuni zinazounga kundi hilo zimeguswa na tukio hilo, na waliamua kutumia uwezo wao kuangalia namna ya kuwasaidia angalau kuondokana na baadhi ya madhila yanayotokana na mafuriko hayo.

"Tunajua msaada huu hautamaliza shida zote, lakini inaweza kupunguza baadhi ya changamnoto wanazokabiliana nazo sasa.

Nawaomba Watanzania na taasisi zingine kutoa msaada wao ili wenzetu waendelee kuishi maisha ya kawaida," aliongeza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Sunshine, Leo Lee, alisema wameamua kutoa msaada kwa waathirika hao kama njia ya kutambua urafiki wa kindugu kati ya Tanzania na China.

"Watanzani na Wachina tumeishi kama ndugu kwa miaka mingi, pale

wenzetu wanapokabiliana na matatizo ni lazima tuangalia namna ya kuwasaidia ili wasimame na kuendelea na shughuli zao," alisema Lee.

Mke wa Mbunge wa jimbo hilo ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, Germina Lukuvi, alishukuru kwa msaada waliopata na kueleza utasaidia kuwarudishia matumaini watu walioathirika na mafuriko hayo.

"Kwa niaba ya mbunge, nashukuru kupata msaada huu kwa watu wa Isimani, na napenda kusema kwamba utawafikia walengwa ili kuwarudishia matumaini," alisema.

Alisema mafuriko hayo yamerudisha nyuma maendeleo ya eneo hilo kutokana na maji kusomba mazao mashambani, nyumba na miundombinu ya barabara.

# Uchunguzi mgongo, mifupa kufanyika Dar

Na Mwandishi Wetu

MTAALAMU wa magonjwa ya uti wa mgongo na mifupa kutoka India, anatarajiwa kutua nchini wiki hii kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi watu wenye matatizo ya aina hiyo. Uchunguzi huo wa siku mbili, utafanyika katika Hospitali ya Regency, Mtaa wa Alykhan, Dar es Salaam kwa kushirikiana na HCG Multi-Super Specialty ya Ahmedabad, India.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Hospitali ya Regency, uchunguzi huo utafanyika kuanzia keshokutwa na kuwataka watu wenye matatizo kama hayo wajitokeze kwa wingi kufanyiwa uchunguzi.

Taarifa hiyo ilisema mtaalamu huyo kwa kusaidiana na wataalamu wa ndani, watawafanyia uchunguzi watu mbalimbali maumivu ya shingo, maumivu ya mgongo, matatizo ya uti wa mgongo na kuwapatia matibabu stahiki.

Aidha, taarifa hiyo ilisema uchunguzi huo utafanywa na mtaalamu huyo kwa kushirikiana na wataalamu wa hospitali hiyo.

"Juhudi hizi za pamoja mwisho wa siku zitawapa ujuzi wa hali ya juu wataalamu wetu kujua namna ya kufanya upasuaji wa aina hiyo kwa teknolojia ya kisasa, hivyo kufanya upasuaji huu wa kisasa kupatikana nchini na kuokoa fedha nyingi zinazopelekwa nje ya nchi kwa matibabu kama haya," ilisema taarifa hiyo.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kushoto), akizungumza wakati ufunguzi wa kikao cha wadau wa benki na sekta ya kilimo kilichoandaliwa na Benki ya Mandeleo ya Kilimo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Japhet Justime na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania, Italia kushirikiana kukabili mabadiliko tabianchi

Na Lulu Mussa

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema Serikali ya Tanzania iko tayari kuendeleza ushirikiano na Italia katika nyanja za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Aliyasema hayo jana baada ya kufanya mazungumzo na

Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni katika Ofisi Ndogo ya Makamu wa Rais jijini Dar es Salaam.

Alisema suala la mabadiliko ya tabianchi ni nyeti duniani kwa sasa na nchi zinazoendelea ndiyo waathirika wakubwa kutokana na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na nchi zilizoendelea.

Zungu alitoa wito kwa Serikali ya Italia kuendeleza ushirikiano katika nyanja za udhibiti wa taka na kujenga uwezo katika uzalishaji wa nishati mbadala ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.

"Serikali ya Rais John Magufuli inatekeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji kwa lengo la kuongeza nishati ya umeme na kukuza sekta ya viwanda nchini," alisema.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere kutachochea jitihada za serikali za kupambana na uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji wa miti kwa matumizi ya nishati ya kupikia.

Alisema jitahada za dhati zinatakiwa kuwapo pia katika uzalishaji wa umeme wa nishati ya jua na upepo.

Balozi huyo wa Italia nchini alisema nchi yake inalenga kutoa msukumo zaidi katika mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhimiza kilimo rafiki kwa mazingira, nishati mbadala na nishati jadidifu.

Waziri alimhakikishia Balozi Roberto ushirikiano wa dhati katika kupambana na uharibifu wa mazingira nchini ili kuhakikisha Tanzania inabaki salama kwa taifa la sasa na vizazi vijavyo.

## HABARI KITAIFA

# Afunguka mazito akiwania uenyekiti ACT-Wazalendo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Nyangaki Shilungushela, kutoka mkoani Shinyanga, amechukua fomu ya kugombea uenyekiti wa chama hicho ngazi ya taifa.

Shilungushela alichukua fomu hiyo, huku akijinadi kurudisha upinzani wenye kujenga hoja na siyo ubabe wala maandamano yasiyo na tija.

Shilingushela alichukua fomu hiyo juzi kwenye ofisi za ACT-Wazalendo mkoani Shinyanga, na kukabidhiwa rasmi na katibu wa chama hicho mkoani humo, Merkyoli Tafuta, na kueleza kuwa anaitaka nafasi hiyo ili arudishe taswira ya upinzani wa kweli wenye kujenga hoja katika kupigania maslahi ya Watanzania.

Alisema akichaguliwa kuwa mwenyekiti, atahakikisha anarudisha taswira mpya ya upinzani, hivyo kufanya siasa zenye tija za kujenga hoja, na siyo za ubabe na kufanya maandamano ambayo hayana faida kwa wananchi.

"Ndugu wajumbe, kwanza nimeamua kuchukua hii fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti taifa ili kutimiza takwa la katiba, ambapo kila mwanachama ana haki ya kugombea na kuchaguliwa," alisema na kuendelea:

"Pia nimechukua hii fomu sababu taswira ya upinzani imekuwa nzito, namna ya kujiendesha na kufanya ubabe usio na tija."

Naye mgombea wa nafasi ya umakamu wenyekiti wa taifa, Twaha Makani, ambaye pia ni Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Wilaya ya Shinyanga, alisema ameamua kugombea nafasi hiyo ili akabadilishe vijana wa vyama vyote na kuwakomaza kisiasa, na kuacha tabia ya kununuliwa na baadhi ya wagombea na kufanya fujo kwenye uchaguzi.

Alisema vijana wengi hawajua wanachokifanya ndani ya vyama vya siasa, na ndio maana huwa wanatanguliwa mbele kufanya maandamano.

Alisema kama atachaguliwa, atakwenda kujenga hoja ya kudai katiba mpya, ambayo ndio itakuwa suluhu ya kumaliza changamoto yote za kisiasa nchini.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo mkoani Shinyanga, Siri Yasini, aliwapongeza viongozi hao kuthubutu kugombea uongozi wa nafasi za kitaifa, na kubainisha nafasi hizo siyo kazi nyepesi, huku akiomba kwenye uchaguzi huo ambao utafanyika Machi 16, mwaka huu demokrasia itawale.



Katibu wa Chama cha ACT-Wazalendo mkoani Shinyanga, Merkyoli Tafuta, akimkabidhi mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho kutoka Shinyanga, Nyangaki Shilungushela fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti ngazi ya taifa, mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Walimu wahamasishwa kugombea

**Jimmy Mahundi,** SONGEA

UONGOZI wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) mkoani Ruvuma, umewataka wanachama kutumia haki yao ya kikatiba kuwania nafasi mbalimbali za uongozi zinazogombewa katika uchaguzi unaoendelea ngazi zote.

Pia wametakiwa kuepuka kutoa rushwa au kupokea kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria za Tanzania. Ushauri huo ulitolewa na Katibu wa CWT mkoani humo, Shaibu Omary, wakati wa mahojiano na vyombo vya habari, kuhusu utaratibu na ratiba ya uchaguzi wa viongozi wa chama hicho, na kuwataka kushiriki kikamilifu kwa kuwa ni haki ya kila mwanachama kuchagua na kuchaguliwa. Omary alidai kuwa ratiba ya chaguzi hizo zimeanza kuanzia ngazi ya tawi ambapo kuanzia Februari Mosi mpaka 14 ndio wakati sahihi kwa wale wenye nia ya kugombea nafasi kwa ngazi hiyo kuchukua famu, hivyo ni wajibu wao kupata viongozi ambao wataingia katika kuwania nafasi za wilaya na kisha ngazi ya mkoa ifikapo Aprili 30, mwaka huu. Aliwakumbusha wanachama wote kuzingatia ratiba na kujitokeza kuwania ili kupata viongozi bora wenye moyo wa kusaidia.

Kuhusu suala la matumizi ya rushwa kwenye uchaguzi huo, akiwaomba wanachama kuepuka kutoa hongo kwa minajili ya kushawishi wapigakura ili wawachague na kuwa viongozi kama hao hawatakiwi kabisa kwa kuwa ni kosa kisheria pia ni hatari kwa ustawi wa jumuiya hiyo.

## Elimu yahimizwa kwa wazazi wa kike

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imeombwa kuweka msisitizo wa kutoa elimu kwa wazazi hasa wa kike waishio vijijini kuhusiana na ni namna gani wanaweza kufuatilia kwa karibu nyendo za watoto wao.

Hatua hiyo inafuatia kubainika kuwa wapo baadhi ya wanawake huamua kuacha jukumu la malezi kwa baba, hali inayochangia kuongezeka kwa matukio ya ubakaji.

Ofisa Mtendaji Kata ya Kiroka, Mage Baraka, alisema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe, na kubainisha kuwa matatizo ya ubakaji kwa watoto mara nyingi hufanywa na wazazi wa kiume, jambo linalotishia afya na saikolojia za watoto kwa sasa.

Alisema chanzo cha matatizo hayo ni mzazi wa kike kushindwa kumwangalia mtoto, kujua ratiba zake za muda wa kutoka shule na hata yupo wapi na anafanya nini na kwa wakati gani, bali jukumu hilo hubebwa na baba.

Baraka alisema kumwachia baba majukumu hata kwa mtoto wa kike ni suala ambalo linatakiwa kupingwa vikali na kama ni masuala ya mila au tamaduni zinapaswa kuachwa mara moja.

Naye Mtendaji wa Kijiji cha Diovuva Kata ya Kiroka wilayani Morogoro, Rehema Kyatula, alisema matukio ya ubakaji kwa watoto mara nyingi hufanywa na wazazi wa kiume wenyewe na wengine huishia kutoroka bila kuchukuliwa hatua.

Kyatula alisema mwaka 2018 baba mzazi alitoroka na kukimbilia kusikojulikana baada ya kuhisiwa kumbaka mtoto wake wa darasa la tatu.

# Wachimbaji wahimizwa fao la matibabu bure NSSF

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wameshauriwa kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kunufaika na fao la matibabu ya bure.

Mwanachama wa mfuko huo kuanza kunufaika ndani ya miezi sita baada ya kujiunga na kutoa michango. Kwa kuwa wachimbaji wadogo wamekuwa wakipata ajali za mara kwa mara wawapo katika uchimbaji, fao la matibabu litakuwa msaada mkubwa wa matibabu.

Meneja wa NSSF Wilaya ya Kahama, Aisha Nyemba, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kusema kuwa kundi hilo halina utaratibu wa kujiwekea akiba kutokana na kutokuwa na uhakika wa maisha.

Aidha, alisema alifanya ziara ya kuwatembelea wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali ya migodi midogo na kuzungumza nao juu ya kujiwekea akiba kwa ajili ya maisha ya baadaye, lakini walidai hawawezi kujiunga na kutoa michango kwa madai ni marehemu watarajiwa.

Nyemba alisema tangu mwaka 2000 hadi sasa wana wanachama 14,872, kati ya hao 3,636 ndio wanalipa michango kila mwezi, idadi ambayo alisema ni ndogo ukilinganisha na watu waliojiandikisha katika mfuko huo.

"Haiwekezani kundi la waliojiunga na mfuko huu kuwa ni kubwa, wakati wanaolipa michango ni wachache, hata kama watakuwa wamepoteza maisha idadi haiwezi kushuka kwa kiasi hiki," aliongeza Nyemba. Pia alisema kundi kubwa ambalo lilikuwa limejiunga na hifadhi na kushindwa kuendelea kulipa michango ni waliokuwa wafanyakazi wa migodi ya Bulyanhuru na Buzwagi ambao waliachishwa kazi baada ya migodi hiyo kusitisha kuendelea na uzalishaji na kustaafu.

Aliwataka wamiliki wa taasisi binafsi ambazo hawapeleki michango ya watumishi wao katika mfuko huo, kuhakikisha wanawasilisha na kuongeza kuwa Wilaya ya Kahama ina waajiri wengi ambao hawapeleki michango ya watumishi wao hususan kampuni zilizowekeza.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa wa Bunge, Daniel Eliufoo (kulia), akiwapatia maelezo Maofisa Waandamizi wa Jeshi kutoka Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC), walipotembelea ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake. **PICHA: BUNGE**

# Mashauri 172 ubakaji wanafunzi yafunguliwa

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

JUMLA ya mashauri 172 ya makosa ya ubakaji kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani Singida yamefunguliwa mwaka jana katika Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Mkoa.

Vitendo vya ubakaji vimechangia baadhi ya wanafunzi hao kupata ujauzito, hivyo kushindwa kuendelea na masomo yao.

Akitoa taarifa za utendaji wa shughuli za Idara ya Mahakama mkoani Singida, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Singida, Consolata Peter Singano, alisisitiza kuwa mashauri hayo ndiyo yanayoongoza yakifuatiwa na mashauri ya dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa Singano, dawa za kulevya ni pamoja na bangi, mirungi na heroin zinazotengenezwa kwenye viwanda na kwamba ambapo jumla ya mashauri ya makosa 135 yalifunguliwa katika mahakama hizo kwa mwaka uliopita.

"Katika Mkoa wa Singida kwa ujumla wake mashauri ya makosa ambayo yanaonekana kwamba yanafunguliwa sana mahakamani, yamekuwa ni mashauri ya makosa ya ubakaji... ubakaji umekuwa ukiwahusu sana wanafunzi na wengi wao pia wametiwa mimba, kwa hiyo kwa mkoa mzima yapo jumla ya mashauri ya makosa 172," alifafanua Singano.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, dawa hizo zina madhara, hivyo sheria imewekwa ili kuwanusuru watu wasiathirike kwa dawa hizo kwani nyingi zinaathiri ubongo wa mtumiaji kwa kiwango kikubwa.

Mashauri mengine yaliyofunguliwa katika mahakama hizo ni ya makosa ya uhujumu uchumi yanayohusisha nyara za serikali, ambapo jumla ya mashauri ya makosa 112 yamefunguliwa na idadi kubwa ya mashauri hayo yanapatikana Wilaya ya Manyoni kutokana na kuwapo Kikosi cha Kuzuia Ujangili (KDU) na kuna msitu wa Pori la Akiba wa Rungwa Kizigo na Muhes unaowavutia majangili wengi.

# Italia yatoa bil. 5/- kukabili tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

ITALIA imekubali kutoa Euro milioni mbili (zaidi ya shilingi bilioni tano za kitanzania) kwa Tanzania ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, alitangaza msaada huo jijini Dar es Salaam jana, baaada ya mazungumzo na Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni, kwamba fedha hizo ilibidi zitolewe tangu mwaka 2016, lakini hazikutoka kwa sababu ya mabadiliko ya uongozi nchini humo.

"Serikali iliyopo sasa madarakani imeridhia kutolewa kwa kiasi hicho cha fedha. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muunganonaishukuru Serikali ya Italia kwa uamuzi wake kwani fedha hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa jitihada za serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli katika kupambana na mabadiliko yanayotokana na tabianchi," alisema Waziri Zungu.

Aliishukuru serikali ya Italia kwa kuyapa kipaumbele masuala ya kulinda mazingira na namna ya kukabiliana na mabadiliko yanayotokana na tabia nchi.

"Mazingira ni suala muhimu kwa mustakabali wa Tanzania yetu na dunia kwa ujumla. Hivyo msukumo huu ulionyeshwa na serikali ya Italia utachochea sana jitihada za kuyaweka mazingira salama kwa faida ya

vizazi vya leo na kesho," amesema na kuongeza kuwa serikali itasimamia vilivyo kuhakikisha pesa hizo zinafanya shughuli iliyokusudiwa.

Mbali ya kuzungumzia suala la tabia nchi, Waziri Zungu amesema kuwa wamezungumzia pia masuala ya matumizi ya nishati mbadala, matumizi ya taka ngumu ziweze kuwa nishati, maboresho ya fukwe pamoja na nyanzo vya maji.

Balozi Mengoni alisema wataendelea kuimarisha mahusiano kati ya nchi hizo mbili licha ya mabadiliko ya uongozi nchini mwao na kuimarisha ushirikiano katika mambo yote muhimu ili kujenga jamii yenye ustawi mzuri.





# Wananchi waomba huduma kliniki

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

WAKAZI wa Kitongoji cha Maweni, Halmashauri ya Babati mkoani Manyara, wameiomba serikali kuwasaidia kupata huduma ya kliniki kwa watoto. Huduma hiyo, haipatikani kwa muda mrefu kwenye kitongoji hicho, kutokana na wananchi wa eneo hilo, kuifuata katika kituo cha afya kilicho mbali.

Ombi hilo, walilitoa jana kwenye ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Babati wakati ikikagua ujenzi wa Shule ya Msingi Malesh.

Mkazi wa kitongoji hicho, Angelina Aloyce, aliwaambia wajumbe hao kuwa wanashindwa kuwapeleka watoto kliniki kila mwezi kutokana na umbali.

Alisema hadi kufika kituo cha afya kupata huduma hiyo, wananchi wanatembea zaidi ya kilometa 20, kwenda Kata ya Gallapo kwenye Kituo cha Afya Gallapo.

"Watoto wetu hawapati huduma ya kliniki ya kila mwezi kwa sababu ya kukosa zahanati, pia hatuna kituo cha afya na tunachokitegemea kwa ajili ya kupata huduma ya matibabu ni kituo cha afya Gallapo na kipo mbali na makazi yetu," alisema Aloyce.

Mkazi wa kitongoji hicho, Rukia Kemo, alisema huduma za afya katika eneo hilo ni za kusuasua na tatizo hilo la kukosekana kwa huduma hiyo linawagharimu wajawazito kwenda kwa kliniki kwa wakati na muda wa kujifungua.

"Tukitaka kujifungua tunapata shida sana mpaka tuende kituo cha afya Gallapo na kipo mbali na makazi yetu, hadi kufika huko, tunatembea kilometa zaidi ya 20 na wajamzito wakifika huko wanakuwa wamechoka kitendo hicho kinasababisha kufanyiwa upasuaji ili kuokoa maisha ya mama na mtoto," alisema Kemo.

Alisema kufika kituo cha afya Gallapo, wananchi wanatumia Sh. 30,000 kwenda na kurudi kwa ajili ya usafiri wa boda boda.

Aliiomba serikali kuwasaidia kujenga zahanati karibu na eneo hilo, ili wapate huduma kwa karibu.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Babati, Dk. Hosea Madama, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, aliwahakikishia wananchi hao, hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, huduma ya kliniki itakuwa imepelekwa.

Katibu wa CCM Wilaya ya Babati, Filbert Mampwepwe, alimtaka Mganga Mkuu kupeleka haraka huduma ya kliniki kwenye eneo hilo.



Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini, Prof. Shukrani Manya (kulia), akizungumza wakati akikabidhi jengo la kituo cha biashara ya madini ya Tanzanite, kwa Ofisa Madini Mkazi wa Mirerani, Daudi Ntalima (kushoto), juzi, lililojengwa na Suma JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 1.3. Anayeshuhudia (katikati) ni Waziri wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Akabidhi mabati kuezeka madarasa

**Na Allan Isack,** MBULU

MBUNGE wa Jimbo la Mbulu Vijijini mkoani Manyara, Flatei Maasay, amekabidhi mabati 120 kwenye Shule ya Msingi Ng'wandakw Kata ya Haydom ili kutatua tatizo la wanafunzi 400 kukosa madarasa.

Akizungumza jana wakati akikabidhi mabati hayo, alisema lengo ni kupaua vyumba vipya ili wanafunzi waliokosa madarasa wapate eneo la kusomea.

Alisema Shule ya Ng'wandakw ina wanafunzi 1,700 na vyumba vya madarasa vilivyopo ni 10 ambavyo havikidhi mahitaji ya wanafunzi.

Hata hivyo, alisema hadi sasa kuna madarasa manne mapya yamejengwa na kati ya hayo, mawili yamefikia hatua ya upauzi na mengine yapo kwenye hatua ya msingi. "Tutahakikisha wanafunzi hawa wanasoma kwenye mazingira bora ili wapate elimu ambayo itawanufaisha wao na jamii kwa ujumla kwa miaka ijayo," alisema Massay.

Alisema mpango wa elimu bure uliotolewa na Rais John Magufuli, umeleta mwamko wa kusomesha watoto. "Nawapongeza wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini ambao wameitikia wito wa kusomesha watoto baada ya tamko la elimu bure kutolewa," alisema Massay.

Baadhi ya wazee wa eneo la Ng'wandakw walimpatia zawadi ya mbuzi mbunge huyo, kama shukrani ya kuwakabidhi mabati hayo 120.

Mmoja kati ya wazee hao, James Clet, alishukuru kupatiwa mabati hayo kwa kuwa yatawasaidia kuezeka baadhi ya madar-

## Biteko atambua mchango wachimbaji wadogo

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema kuwa Wizara ya Madini inawathamini wachimbaji wadogo wa madini nchini kwa kuwa wameinyanyua sekta hiyo kwa kuongeza mapato kwa wingi.

Biteko ameyasema hayo juzi wakati akikabidhiwa jengo la kituo cha pamoja cha biashara cha madini ya Tanzanite na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dk. Hussein Mwinyi.

Jengo hilo, lilijengwa na askari wa Jeshi la Kujenga Taifa la Suma (JKT).

Biteko alisema baadhi ya wachimbaji wakubwa wa madini awali walisusia kuchimba madini, lakini wachimbaji wadogo waliendelea na shughuli zao ambazo ziliongeza mapato kwa wingi katika sekta ya madini nchini.

Alisema Kampuni ya Tanzanite One, kabla ya kufunga mgodi huo, walikuwa wanachagia mapato kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.1.

Hata hivyo, alisema kampuni hiyo na wachimbaji wakubwa walipoacha kuendelea na shughuli za madini, wachimbaji wadogo waliwapita kwa kuongeza mapato mengi hadi kufikia kiasi cha Sh. bilioni 2.7.

Aliwaomba wachimbaji madini wadogo wa madini ya Tanzanite kuendelea kuwa wazalendo kwa kulipa kodi ili serikali iendelee kuingiza mapato na kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Kwa upande wake, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Hussein Mwinyi, aliwashukuru viongozi wa Wizara ya Madini kwa kuwapa heshima ya kujenga miradi mbalimbali ya madini. "Pamoja na hayo nawapongeza maofisa wa jeshi na askari wengine ambao wamefanikisha ujenzi wa kituo hiki cha pamoja cha kisasa ambacho tunawakabidhi Wizara ya Madini," alisema Mwinyi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Chelestino Mofuga, alimpongeza Waziri Biteko kwa kusimamia Sekta ya Madini.

Alisema sekta hiyo, kwa sasa inatambulika kama sekta rasmi kwa kuingiza mapato mengi ya nchi. Mofuga alisema tangu Biteko akabidhiwe wizara hiyo, ameonyesha juhudi kubwa katika kuongeza mapato kwenye sekta hiyo tofauti na awali.

Meneja wa Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa) wa Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Liberatus Bikulamchi, ambaye ndiye amefunga mfumo wa umeme na taa kwenye ukuta wa machimbo ya Tanzanite alisema wametumia Sh. milioni 716.5.

Bikulamchi alisema kwenye shughuli hiyo, walitengeneza ajira kwa watu 50 kwa muda na hakukuwa na ajali yoyote iliyotokea kwa kuwa sheria za kazi zilizingatiwa na kufuatwa.



# Serikali yafuatilia mwanafunzi anayedaiwa kutoroshwa na mama

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MAMLAKA za serikali wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, zimeombwa kuingilia kati sakata la mwanafunzi wa kike wa kidato cha nne anayesoma mchepuo wa Sayansi katika Shule ya Sekondari ya Kibacha, kudaiwa kutoroshwa na mama yake mzazi ili akafanye biashara kwa mchumba wake anayetarajia kumuoa.

Imedaiwa kuwa mwanafunzi huyo alitoroshwa na kuachishwa masomo yake mwanzoni mwa mwaka huu, akiwa mikononi mwa mama yake anayeishi eneo la Stesheni, Wilaya ya Same.

Ombi hilo lilitolewa jana wilayani hapa na wanaharakati 20 wanaounda Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo) la Wilaya ya Same, wakati wakiwasilisha malalamiko yao kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Charles Anatoly.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Tamari Mndeme, alisema mwanafunzi huyo aliyekatishwa masomo yake na kutoroshwa, anasoma Sekondari ya Kibacha iliyopo Kata ya Kisima na alipaswa kuhitimu masomo yake mwishoni mwa mwaka huu.

"Huyo mwanafunzi ni miongoni mwa wasichana wanaosoma masomo ya Sayansi ambao wanafanya vizuri darasani, tumejadiliana sana namna ya kumkomboa binti huyo arudi shule na tumesema hatua ya kwanza ni kuleta jambo hili katika mamlaka husika ili zichukue hatua baada ya kujiridhisha," alieleza Mndeme.

Akijibu madai hayo ya wanaharakati, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Charles Anatoly, alisema: "Nimepokea malalamiko yenu na nitayawasilisha kunakohusika na pia nitaliingiza kwenye vikao vyetu ili tuchunguze na baadaye kutafuta ufumbuzi wake."

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, kutoa ufafanuzi iwapo jambo hilo limefikishwa rasmi ofisini kwake, alisema mpaka sasa hawajapelekewa taarifa hiyo na kwamba ndani ya saa 24 kuanzia sasa atakuwa amejua ukweli wa jambo hilo.

Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia, Veronika Ullomi, akizungumzia jambo hilo alisema lengo lao ni kuwakomboa wanawake katika ukatili wa kijinsia.

"Nia yetu ni kujenga uelewa wa pamoja wa dhana muhimu za kijinsia zikihusishwa na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, lakini kuhamasisha jamii na kukuza uelewa wao kuhusu dhana na itikadi ya ufeministi kama ya kufikia usawa wa kijinsia," alieleza Ullomi.



Msaidizi wa Kisheria, Michael Shayo (kushoto), akiwa na mjane Magdalena Massao (wa pili kulia) na watoto wake wawili, baada ya mjane huyo kukabidhiwa, kiwanja ambacho aliporwa na shemeji yake katika Kijiji cha Mvuleni-Mji Mpya, Moshi Vijijini, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mradi wa mil. 800/- washindwa kukamilishwa

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

MRADI wa maji wa Shimbi Mashariki uliopo Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, haujakamilika tangu mwaka 2013, licha ya mkandarasi anayetekeleza mradi huo kulipwa Sh. milioni 400.

Taarifa ya Mhandisi Joseph Mcharo anayesimamia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) wilayani humo, inaeleza kuwa mradi huo umechukua muda mrefu kukamilika na mkandarasi huyo aliondoka eneo la mradi kwa muda mrefu.

"Huu mradi wa Shimbi Mashariki una thamani ya Sh. milioni 887.4 na mpaka sasa umeshatekelezwa kwa asilimia 88. Anachodai kwa sasa mkandarasi huyu ni kiasi cha Sh. milioni 86 tu," alisema.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mcharo, sababu kubwa wanayoitoa makandarasi ya kuchelewa kukamilisha miradi ni kutolipwa madai yao kwa wakati na wanapoandikia madai yao, huwa wanasimamisha ujenzi mpaka walipwe fedha zao ndio waendelee na kazi.

Kutokana na tatizo hilo, inaelezwa kuwa tayari Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameelekeza kuchukuliwa kwa hatua ikiwamo kuagiza kufuatwa kwa taratibu za kisheria za kuvunjwa mkataba huo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Naibu Waziri huyo ametaka asilimia 12 zilizobaki za mradi kukamilika zifanywe na wataalamu wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Wilaya ya Rombo.

Pia Aweso ameagiza kushughulikiwa kwa madai yanayotokana na stahiki za vibarua kulipwa fedha zao na kuhakikisha mzabuni wa pampu za maji analipwa fedha yake na ziwahishwe ili wananchi wa eneo hilo wapate huduma maji.

Mradi mwingine kama huo ambao haujakamilika kwa muda mrefu na unalalamikiwa na wananchi ni wa maji wa Kijiji cha Leto, wenye thamani ya Sh. milioni 927.9 kutokamilika kwake kunasababisha wanakijiji kwenda kuchota maji nchi jirani ya Kenya.

## Uaminifu wakwamisha utoaji fedha kwa wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

MKUU wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, Thomas Apson, amesema tatizo kubwa linalojitokeza hivi sasa na kukwamisha utoaji wa asilimia 10 ya mikopo ya fedha kwa makundi maalum ni jamii ya watu wenye ulemavu kushindwa kuaminiana.

Apson alisema hali hiyo inaifanya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, wakati mwingine kuchelewa kutoa kwa wakati fedha hizo, baada ya kukutana na tatizo la kutoaminiana miongoni mwa wanavikundi vya watu wenye ulemavu hususani katika usimamizi wa fedha.

"Tunajaribu kutafuta namna ya kuwaweka sawa na hili ni tatizo kwa kweli, watu ambao ikitokea wameshindwa kuaminiana katika kikundi unawezaje kuwapa fedha. Tunawapa elimu na kila kundi litapata mgao wake kwa jinsi maofisa maendeleo ya jamii wataona," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, aliagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, asilipwe mshahara wa mwezi Februari kutokana na kushindwa kujibu maswali kuhusu utengaji wa asilimia 10 ya fedha za mikopo ya makundi maalumu.

Alichukizwa na kitendo cha Mkurugenzi huyo kushindwa kujibu maswali ya halmashauri hiyo kushindwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Kutokana na tatizo hilo, Dk. Mghwira ameagiza wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za Mkoa wa Kilimanjaro, kuhakikisha wanatenga na kutekeleza bajeti za utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Pia amewaelekeza wakuu wa wilaya kuhakikisha wanavisaidia vikundi vyote vyenye utayari wa kupatiwa mikopo hiyo ikiwa ni pamoja na kuwa tayari kuwasilikiliza na kuwapa miongozo ya kuifikia huduma hiyo.

Ukurasa 18



Mkuchika afafanua ushiriki wa nchi utawala bora Afrika

Licha ya ulemavu wa kusikia atangaza atagombea 2020



Ukurasa 15

Kimataifa



Kifo cha mwanamuziki Kizito chaitikisa Afrika Mashariki

Ukurasa 14

siasa

JUMATANO FEBRUARI 19, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Afrika Kusini; 'siasa kali' yakwamisha kwa muda hotuba ya Rais Ramaphosa

Ukurasa 19

# Prof. Lipumba tayari kurudi Ukawa ikiwa...

- Aonya kupokea walioenguliwa CCM

**Na Sabato Kasika**

WAKATI joto la uchaguzi mkuu likiendelea kupanda, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) Taifa, Profesa Ibrahim Lipumba, ameibuka na kuanza kukumbushia uwezekano wa kufufua umoja wa kimkakati ulioundwa na wapinzani waliojiunga na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Hata hivyo, anataja masharti kwa vyama vya upinzani vinavyohitaji ushirikiano huo wa kimkakati akisema ili kuishirikisha CUF ni lazima wakubaliane naye kuwa hakuna sababu ya kukumbatia waliotemwa na chama tawala.

Mwenyekiti huyo anasema, kama vyama vya Chadema na ACT Wazalendo vinataka CUF iungane navyo, katika uchaguzi mkuu, basi visipokee 'mabaki' yaliyoenguliwa kutoka Chama Cha Mapinduzi.

Kwake ndilo sharti kuu, ambalo kiongozi huyo analitoa wakati akizungumza na wanahabari kwenye makao makuu ya chama hicho, yaliyopo Buguruni Dar es Salaam.

Kiongozi huyo anasema, CUF haiko tayari kuungana au kushirikiana na vyama vingine vinavyosubiria wagombea walioenguliwa na kuonekana hawafai, katika nafasi mbalimbali ndani ya CCM.

Endelea 14



Philip Mangula.

Neno la 'lala salama' madiwani waondokao Ukurasa 17

# Kifo cha mwanamuziki Kizito chaitikisa Afrika Mashariki

Na Mashaka Mgeta

TAKRIBANI siku tatu baada ya kukamatwa na kuwekwa kwenye mahabusu katika kituo cha polisi Remera, manusura wa mauaji ya kimbari yaliyotokea Rwanda mwaka 1994, Kizito Mihigo, amekutwa amekufa, akidaiwa kujiua.

Mwanamuziki huyo ambaye awali alionekana kuwa kipenzi cha serikali ya Rwanda, anadaiwa kujinyonga kwa kutumia shuka, maelezo yanayotolewa na polisi.

Taarifa zinazohusu maisha ya Kizito ambaye pia alikuwa msanii maarufu wa muziki wa Injili nchini humo, zinamuelezea kama kijana aliyekuwa na ndoto za kulitendea haki taifa lake kupitia uongozi wa umma, lakini mara kadhaa akajikuta akitiwa nguvuni ama kupata 'kashikasi' nyingine za kisiasa.

Miongoni mwa nyimbo zilizomfanya Kizito afahamike sana Rwanda ni Inuma ukimaanisha njiwa na Igisobanuri cy'urupfu ambao maana yake ni kifo.

Kizito mwenye umri wa miaka 38, alikamatwa na polisi wiki iliyopita na taarifa zilieleza kwamba alikuwa anakimbilia nchini Burundi, kwa mujibu wa idara ya upelelezi ya Rwanda (RIB) na kwamba alikuwa na nia ya kutorokea Ubeligiji.

Sehemu ya taarifa ya jeshi la polisi nchini humo iliyotolewa kuhusiana na kifo hicho inasema, "alikuwa kwenye mahabusu ya polisi kwa siku tatu zilizopita kutokana na RIB kumshutumu kwa kujaribu kuvuka mpaka ili kuingia Burundi kinyume cha sheria, na pia kwa masuala ya rushwa."

Taarifa hiyo inaeleza zaidi kuwa, akiwa mahabusu hapo, Februari 15 na 16, mwaka huu, Kizito alitembelewa na ndugu zake waliofuatana na mwanasheria wake.

"Uchunguzi unaendelea kubaini sababu iliyomfanya akajiua," sehemu ya taarifa ya polisi nchini humo inaeleza.

Taarifa inayotolewa na Msemaji wa Polisi, JB Kabeera kupitia mitandao ya kijamii, inasema mwili wa Kizito ulikutwa wakati polisi wakifanya ukaguzi saa 11 alfajiri ya juzi Jumatatu. Hapakuwa na taarifa zaidi.

Kwa mara ya kwanza, Kizito alikamatwa mwaka 2014 akikabiliwa na tuhuma mbalimbali ikiwemo ya kikundi cha Rwanda National Congress (RNC), kinachotajwa na mamlaka za nchini humo kuwa cha kigaidi na ambacho viongozi wake wanaishi Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za mamlaka hizo, lengo la kikundi hicho ni kuondosha hali ya usalama nchini humo. Katika mashtaka yake, Kizito alikutwa na hatia na kuhukumiwa kwenda jela miaka 10.

Septemba mwaka juzi, Rais Paul Kagame, aliwasamehe wafungwa 2,140 wakiwamo wa kisiasa ambapo Kizito alikuwa miongoni mwa waliotolewa gerezani.

Idara ya upelelezi ya Rwanda ilithibitisha Ijumaa iliyopita kuhusu kushikiliwa kwa Kizito kwa madai ya kujaribu kujiunga na vikundi cha wana mgambo kuhatarisha usalama wa nchi hiyo pamoja na tuhuma za rushwa.

Kupitia akaunti yake ya twitter, RIB ilieleza kwamba Kizito alikamatwa na maofisa wa usalama alipokuwa akijaribu kutorokea nchini Burundi kupitia mpaka uliopo wilayani Nyaruguru, kusini mwa Rwanda.

Mitandao ya kijamii ilikosoa na kuita uvumi uliomhusisha Kizito akiwa na watu wengine watatu, kutaka kutorokea nchini Burundi.

Msamaha wa Rais Kagame kuwasamehe wafungwa wa kisiasa, ulimhusu pia mpinzani wake mkubwa, Ingabire Victoire, aliyehukumiwa miaka 15 jela

Wanasiasa wengine walitoka kwa msamaha huo na idadi yao kwenye mabano ni kutokea wilaya za Bugesera (23), Nyarugenge (447), Musanze (149), Gicumbi (65), Nyanza (63), Rubavu (158), Rwamagana (455) na Nyagatare (24). Huko kote ni katika jimbo la Mashariki.

Wengine walitokea Huye (484), Muhanga (207), Ngoma (35), Rusizi (7) na Nyamagabe (23) ikiwa ni upande wa kusini mwa nchi hiyo.



Kizito Mihigo. **PICHA: MTANDAO.**

> "Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za mamlaka hizo, lengo la kikundi hicho ni kuondosha hali ya usalama nchini humo. Katika mashtaka yake, Kizito alikutwa na hatia na kuhukumiwa kwenda jela miaka 10.

**WALIPOTOKA GEREZANI**

Palikuwa na umati mkubwa wa watu nje ya gereza la Nyarugenge lililopo Mageragere jijini Kigali, ukishuhudia Kizito na Ingabire wakitoka kwa msamaha wa Rais Kagame.

Ilikuwa majira ya saa 3:00, Kizito alitoka ndani ya gereza hilo jipya na pekee lililopo jijini Kigali.

Kizito aliwaambia waandishi wa habari kuwa, "nilitarajia kupata msamaha wa Rais Kagame ninayemjua kwa ni mtu wa msamaha."

Mkazi mmoja wa Nyarugu huko Kusini Magharibi mwa Rwanda, aliliambia Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuwa Alhamisi iliyopita, wanavijiji walimzuia mwanamuziki Kizito aliyekuwa amebeba begi kubwa na kumfikisha kituo cha polisi.

"Nilikuwepo, nilimuona. Wanakijiji waliomzuia walisema alikuwa akijaribu kuvuka mpaka kwenda Burundi kwa kupitia 'njia za panya'. Kutoka hapo mpaka mpakani ni umbali wa takribani dakika tano kwa kutembea kwa miguu," akasema mkazi huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Taarifa ya awali ya RIB inaeleza kuwa huenda Kizito alijinyonga kwa kutumia shuka, lakini uchunguzi utakaotoa taarifa rasmi bado unaendelea.

Baada ya tukio hilo, mwili wake ulichukuliwa na kwenda kuhifadhiwa kwenye hospitali ya Kacyiru.

Taarifa iliyo rasmi inaeleza kuwa ni Kizito alikuwa msanii wa muziki wa Injili, mtunzi wa nyimbo, mpiga kinanda na gitaa, mtangazaji wa runinga na mwanaharakati wa amani na maridhiano.

Alisomea nchini Ufaransa na mwaka 2010 kwa kugharamiwa na serikali iliyomuona ana kipaji kikubwa cha uimbaji. Mwanamziki huyo alianzisha Mfuko wa Wakfu wa Amani wa Kizito Mihigo.

Alizaliwa Julai 25, mwaka 1981 huko Kibeho, Rwanda. Wazazi wake wanatajwa kuwa ni Augustine Buguzi na Placidie Ilibagiza. Na Kizito ni mwathirika wa mauaji ya kimbari na kwamba ni manusura wa mauaji hayo.

Aprili 2014, Kizito alirekodi wimbo uliokosoa na kupinga mauaji ya halaiki, ndipo alipokamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kupanga za kuipindua serikali ya Rais Kagame.

Shauri hilo ndilo lililomsababisha kupatikana na hatia na Februari mwaka 2015, alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 10 jela.

Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa Amani –amina.

**MAKALA HII IMEANDIKWA KWA MSAADA WA VYANZO VYA MTANDAONI. 0754691540**

# Mwenye ulemavu wa kusikia atangaza naye yumo 2020

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MWAKA 2020 ndiyo huu na kikubwa kinachozungumzwa ni uchaguzi mkuu, ndiyo maana wananchi wameanza kujiandikisha na kuwa na vitambulisho vya kupigia kura ili kujihakikishia nafasi ya kuchagua viongozi kuanzia rais, wabunge pamoja na madiwani.

Wanasiasa mbalimbali wanajipanga kuwania nafasi hizo na wale ambao tayari walikuwa wameshikilia nyadhifa hizo na wanataka kurudi tena ulingoni watapata fursa ya kujitangaza kwa wananchi kuelezea walichokifanya kwa miaka mitano ili wapiga kura wawapime kama wanaweza kuwarudisha au kuweka pembeni.

Wapo ambao wanajivunia kuwa wametekeleza ahadi walizotoa kwa wananchi, na hao ni wale ambao wanatamba kuwa waliwatembelea wananchi na kujadili nao changamoto zilizopo na kushirikiana nao kuzitatua, wanajinadi kuwa wamefanyakazi nao wamo..

Katika kuelekea kwenye uchaguzi mkuu , Nipashe inakutana na Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kongowe mkoani Pwani, Tatu Kondo, ambaye ni mlemavu wa kusikia mwenye nia ya kulipanda jukwaa la uongozi wakati wa uchaguzi mkuu wa Oktoba, akisema penye nia na njia ipo..

Tatu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wanaoishi na Ulemavu (Shivyawata) Mkoa wa Pwani, amekuwa akijihusisha na mambo ya kijamii mara kwa mara. Jambo analolieleza kuwa ni sababu kutaka kuwa na nafasi hizo za uongozi.

Anaeleza kuwa, katika nafasi ya mwenyekiti wa Shivyawata walikuwepo wanaume wawili ambao waligombea, lakini akafanikiwa na kuwazidi kikura kutokana na sera zake, lakini pia uwepo wa idadi kubwa ya wanawake wapiga kura.

Tatu anasema, tangu chama hicho kianzishwe mwaka 2007 hakujawahi kuwa na mwenyekiti mwanamke na yeye ndiye wa kwanza kushika nafasi hiyo.

Akiongelea nafasi yake ya ujumbe Mtaa wa Kongowe anasema, haikuwa kazi rahisi kupata nafasi hiyo kutokana na kuishi na ulemavu wa kusikia.

Anaeleza kuwa, baadhi ya watu wamekuwa wakiwakatisha tamaa watu wenye ulemavu kuingia katika ulingo wa kisiasa kwa madai kuwa hawatazimudu nafasi hizo.

" Wanawake wana changamoto nyingi wakati wanagombea uongozi lakini, kwasisi tunaoishi na ulemavu ni zaidi, kwani wengi wanatukatisha tamaa na bila kusimamia na kujizatiti huku ukijiamini kuwa unaweza, huwezi kuingia kwenye kinyang'anyiro," anaeleza Tatu.

Mjumbe huyo anasema, jamii kwa kiasi kikubwa ina wasiwasi kuwachagua watu wenye ulemavu, lakini kwa upande wake suala la kushirikiana mara kwa mara katika shughuli za kijamii, na kujitolea katika mambo ya chama ndiyo chachu ya kuwa katika nafasi hiyo.

" Pamoja na kuwa na hali ya kusua sua kutoka kwa wananchi na hofu waliyojijengea kama watu wenye ulemavu hawawezi kuongoza, nimepambana kujitolea katika mambo mbalimbali kwenye jamii.

Nimekuwa nikiwatembelea wananchi wenzangu, kushirikishana mambo mbalimbali, nimeshiriki pia vikao vya chama na kufundisha walimu lugha ya alama. Aidha nimekuwa kinara wa kushawishi mambo ya maendeleo, nikiwaonyesha wananchi kuwa tukipewa nafasi za uongozi tunaweza," anasema.

Ninachotaka kuionyesha jamii ni kwamba, watu wenye ulemavu wanapojitokeza kugombea wawape nafasi kwani wana uwezo sawa na wale wenye viungo vyote.

" Lakini pia nawasisitiza watu wanaoishi na ulemavu wasijitenge, wasikubali kukatishwa tamaa, kwani kuwa na ulemavu si sababu ya kushindwa kuongoza" anasisitiza Tatu.

Halikadhalika anasema kuwa, kutokana na nafasi aliyonayo amekuwa na mipango ya kuendelea kuwashawishi wanawake kuwa familia moja, kushirikiana pale mmoja wao anapoweka nia ya kugombea.

Aidha, anawahamasisha wanawake wenye ulemavu kujishughulisha na kuachana na utegemezi, wajiunge na vikundi ambavyo vitawarahisishia kupata mikopo za kuendesha shughuli zao.

" Wanawake wenye ulemavu wengi wao hawajiamini, wamekuwa waoga kutokana na vitisho pamoja na kukatishwa tamaa na baadhi ya wanajamii ambao wamejijengea dhana potofu kuwa mtu mwenye ulemavu hana uwezo wa kuongoza , jamii inapotutisha kwa maneno kama hayo wengi wanakata tamaa" anaeleza kiongozi huyo.



Tatu Kondo (kulia) akipokea cheti kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Fahari ya Wanawake Viziwi, Anneth Gerana, baada ya mafunzo ya ujasiriamali.

### KUSIMAMA UONGOZINI

Aidha, anasema, kushika nafasi alizonazo kwasasa, imetokana na kuungwa mkono na familia yake, chama chake Cha Mapinduzi (CCM), na wanajamii ambao wanawathamini watu wenye ulemavu na kuwapa nafasi.

"Naamini hii nafasi ya ujumbe niliyo nayo kwa sasa imechangiwa na kuwa na mkalimani wakati najieleza mpaka tulipomaliza zoezi la kuhesabu kura na kutangazwa washindi. Mwaka 2015 haikuwa hivi nadhani pia hali ile ilinikosesha udiwani," anasema Tatu.

Akiongelea harakati zake katika kuwania nafasi mbalimbali, Tatu anasema, mbali ya kuwa katika nafasi anayoshikilia mwaka 2015 aliingia katika kinyang'anyiro cha udiwani .

Anasema, akiwa katika ngazi ya kura za maoni kata ya Kongowe, kulikokuwa na wagombea 40 alivuka kiunzi na kushika nafasi ya nane, pamoja na hali ya ulemavu anayoishi nayo.

Tatu anabainisha kuwa nafasi hiyo aliipata kwa vile hakukuwa na mkalimani wa lugha ya alama wakati anajinadi hadi muda wa kuhesabu kura.

Anasema, kipindi hicho kulitokea changamoto ya mkalimani wake kuzuiliwa kuingia ndani ili kutafsiri lugha na hivyo kusababisha kushindwa kujieleza.

" Naamini hii nafasi ya ujumbe niliyo nayo kwa sasa imechangiwa na kuwa na mkalimani wakati najieleza mpaka tulipomaliza zoezi la kuhesabu kura na kutangazwa washindi. Mwaka 2015 haikuwa hivi nadhani pia hali ile ilinikosesha udiwani," anasema Tatu.

### OMBI KWA SERIKALI

Mjumbe wa serikali ya mtaa wa Kongowe, anaiomba serikali kuzingatia suala la kuweka wakalimani maeneo yote ambayo yana walemavu, ili kurahisisha jambo linalofanyika katika muda huo nao waweze kushirikiana kikamilifu kama wengine.

Aidha, anaiomba jamii kuondoa imani potofu kuwa, watu wenye ulemavu wa kusikia wanawategemea zaidi wakalimani kuongea hata mambo ambayo wao hawajayafanya, na badala yake kuelewa kuwa Lugha inayotafsiriwa na mkalimani ni kutokana na kitu kinachosemwa na mlemavu.

Akiongelea suala la wakalimani, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kibaha Mjini, Afidu Luambano, anasema, katika maeneo ambayo wataelezwa kuwapo kwa watu wenye ulemavu wanaohitaji wakalimani watahakikisha wanakuwepo.

Luambano, anawasisitizia watu wenye Ulemavu kuacha kujitenga na badala yake kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Anasema, hata pale watakapoamua kushiriki katika uchaguzi kwa kugombea, chama hicho kitaendelea kuwapa ushirikiano sawa na ambao hawana ulemavu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Jenifer Omolo, amewahakikishia ushirikiano watu wote katika kipindi chote cha uandikishaji wa daftari la mpiga kura na shughuli zote kuelekea uchaguzi Mkuu.

Omolo anasema, katika maeneo yote kutakapokuwapo na watu wenye Ulemavu wanaohitaji wakalimani watahakikisha wanakuwapo.

Wanawake mkoani Pwani wengi wao sasa wameanza kuondokana na utegemezi, kwa kujishughulisha na shughuli mbalimbali huku wengine wakijiingiza katika siasa na kazi mbalimbali za uongozi.

SIASA

# Lipumba tayari kurudi Ukawa, ikiwa...

## ■ Aonya kupokea walioenguliwa CCM

“Nipo tayari kuungana na Freeman Mbowe na Zitto Kabwe, pamoja na vyama vingine vya upinzani, iwapo watakuwa tayari kutekeleza sharti hilo, vinginevyo, sisi kama CUF tutakwenda kivyetu na wao kivyao,” anasema.

Prof. Lipumba anasema, siyo utaratibu wa kufanya umoja wa kusubiri nani atakeyetemwa na CCM au kuenguliwa bali CUF itashirikiana na vyama vyenye nia ya dhati ya kusimamia mabadiliko ya kweli.

“Vyama vya upinzani havijazungumza chochote kuhusu ushirikiano, na huwezi kusema ushirikiano wakati hujaongea na vyama. Unatakiwa ushirikiano wa kuitoa CCM madarakani na siyo ushirikiano wa kusubiri mabaki ya CCM,” anasema.

**ACT WAZALENDO**

Wakati Lipumba akitoa sharti hilo, tayari Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alishasema, lazima vyama vya upinzani viungane katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kwamba, vikiona anatosha kuwania urais atakubali na kufafanua kuwa kwa muda mrefu amekuwa na nia ya kuwa rais wa Tanzania, na kusisitiza kuwa suala hilo si la mtu mmoja bali ni uamuzi wa chama au vyama vya siasa.

“Iwapo vyama vitaona mimi ndiyo mgombea ninayestahili kupeperusha bendera nitagombea, lakini vikiona mtu mwingine ndiyo anafaa zaidi, basi nitamuunga, lazima tushirikiane kuiondoa CCM madarakani,” anasema Zitto.

Zitto anatoa kauli hiyo Desemba mwaka jana Dar es Salaam wakati wa mahojiano katika kipindi cha Konani cha kituo cha televisheni cha ITV wakati akijibu maswali ya mtazamaji aliyetaka kujua kama ana nia ya kugombea urais kwenye uchaguzi ujao. Zitto amesema kwa muda mrefu amekuwa na nia ya kuwa Rais wa Tanzania,

Anasisitiza kuwa suala hilo si la mtu mmoja bali ni uamuzi wa chama au vyama vya siasa kwa vile ushirikiano ni jambo la muhimu kwa ajili ya kuiondoa CCM madarakani, lakini vinginevyo, bado kutakuwa na ugumu.

“Ninaumizwa kuona takribani Watanzania milioni 14.7 wanaishi katika umaskini licha ya wingi wa rasilimali zilizopo na nikiwa rais nitasimamia zaidi sekta ya kilimo, ambayo ndiyo inaajiri watu wengi,” anasema.

**KUMBUKIZI**

Mwaka 2014 wakati Bunge Maalum la Katiba likiendelea na vikao vyake jijini Dodoma, baadhi ya wajumbe kutoka vyama vya upinzani walisusia bunge hilo na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi.

Walisusia bunge hilo kwa kile walichodai kuwa ni kupuuzwa kwa makusudi maoni ya wananchi wanaotaka muungano wa muundo wa serikali tatu kama yalivyopendekezwa katika rasimu ya katiba, huku mmoja wajumbe hao Prof. Lipumba akilalamikia kauli za ubaguzi za baadhi ya wajumbe.

“Hatuwezi kuwa kama kundi la wapiganaji linalohamamisha ubaguzi ndani ya Tanzania, hili hatulikubali, hatulikubali, hatulikubali, watu wote tunaotaka katiba ya wananchi tunawaachia muendelee na kikao chao. Ahsanteni sana,” alisema Prof Lipumba.

Baada ya kusema hivyo, wajumbe waliounga mkono kauli yake waliinuka na kutoka ndani ya ukumbi na kuungana kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa mwamvuli wa Ukawa.

Vyama vilivyounda Ukawa ni Chadema, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD, lakini kabla ya uchaguzi huo, Prof. Lipumba alijiondoa aliachia nafasi ya mwenyekiti wa CUF na kubaki kuwa mwanachama wa kawaida.

Siasa za upinzani kuelekea uchaguzi mkuu huo, zilizidi kutoa sura mpya, huku mshikamano ndani ya Ukawa waliotangaza kusimamisha mgombea mmoja wa urais na kuachiana majimbo ukaelekea kuzorota zaidi kutokana na tofauti zilizokuwa zikijitokeza siku hadi siku.

Wakati akitangaza hatua ya kuachia nafasi hiyo mbele ya wanahabari, alidai uamuzi huo unatokana na Ukawa kushindwa kusimamia makubaliano yao, ambayo hata hivyo hakuyawekwa wazi.

Ni wakati huo wa kuelekea uchaguzi mkuu, ndipo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Wilbroad Slaa , aliamua kujiweka pembeni huku akiwa na sababu mbalimbali ikiwamo kutoridhishwa na Ukawa.

Hatua hiyo ilikuwa ni pigo kwa umoja huo, ambao ulionyesha nguvu kubwa za upinzani kuelekea kwenye uchaguzi huo, hasa kutokana na ujio wa Lowassa, ambaye alionekana kuwa kikwazo kwa Prof. Lipumba na Dk. Slaa.

Kujitenga kwa wanaasiasa hao kulisababisha taharuki ndani ya upinzani, huku wachambuzi wa siasa wakidai kuwa kujitenga kwao ni kulitokana na kutopendezwa na ujio wa Edward Lowassa ndani ya Chadema na kupewa nafasi ya kuwania urais kwa mwamvuli wa Ukawa.

Kwa upande wake Dk. Slaa alirejea ndani ya CCM, lakini Prof. Lipumba alibaki kuwa mwanachama wa kawaida, katika chama cha CUF kwa miezi kadhaa kabla ya kuamua kurudia uenyekiti.

Yawezekana hilo likawa na ukweli ndani yake, kufuatia sharti lake alilotoa kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwamba, CUF haitaungana na vyama vinavyosubiri ‘mabaki’ kutoka CCM.

**MGOGORO CUF**

Mwanzoni mwa mwezi Agosti mwaka 2015, ndipo Prof. Lipumba alipotangaza kuachia nafasi ya uenyekiti wa CUF taifa, lakini chama kiliendelea kuwa ndani ya Ukawa na kushiriki, katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

Ingawa hatua ya Lipumba ilikuwa ni pigo kwa Ukawa, lakini vyama viliendelea kushirikiana, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa kuachiana kata na majimbo na kufanikiwa kujizolea viti vingi vya udiwani na ubunge.

Hata hivyo, baadaye mwaka 2016, mwanasiasa yuko alitangaza kurejea kwenye nafasi yake ya uenyekiti wa CUF taifa na kusababisha mgogoro wa uongozi uliodumu kwa muda mrefu.

Mgogoro huo ulisababisha Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Sief Sharif Hamad kujiondoa katika chama hicho na kujiunga katika Chama cha ACT Wazalendo, na sasa anataka kuungana na vyama vingine, lakini kwa sharti moja.



Baadhi ya viongozi wa Ukawa wakati huo kabla ya Prof. Ibrahim Lipumba kujiondoa.

> “Ninaumizwa kuona takribani Watanzania milioni 14.7 wanaishi katika umaskini licha ya wingi wa rasilimali zilizopo na nikiwa rais nitasimamia zaidi sekta ya kilimo, ambayo ndiyo inaajiri watu wengi,” anasema.




Maalim Seif akiwa mwanachama wa ACT Wazalendo baada ya kukimbia CUF. **PICHA: MTANDAO**

> “Hatuwezi kuwa kama kundi la wapiganaji linalohamamisha ubaguzi ndani ya Tanzania, hili hatulikubali, hatulikubali, hatulikubali, watu wote tunaotaka katiba ya wananchi tunawaachia muendelee na kikao chao. Ahsanteni sana,” alisema Prof Lipumba



Baadhi ya madiwani katika Baraza la Madiwani wa Mkuranga, wakiwa kikaoni. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

# Neno la ‘lala salama’ madiwani waondokao

**Na Yasmine Protace, Mkuranga**

NI siku za ‘lala salama’ kwa madiwani, hata wabunge . Zimebaki katika kumaliza miaka yao mitano ya kuwatumikia wananchi wao.

Pamoja na kuwa ni siku zinazoitwa ‘lala salama.’ Madiwani wametakiwa kuendelea kuwatumikia wananchi na sio kuishia safari kati .

Siku hizo zilizobaki, madiwani wanatakiwa kuendelea kusimamia majukumu yao kwa kuwaletea maendeleo wananchi na hali hiyo inaweza ikamfanya diwani ama kupigiwa kura tena na wananchi, endapo jina lake likapitishwa na kugombea tena.

Kuna miradi ya maendeleo ya maji, elimu na afya kwa kutaja machache, yote inatakiwa kusimamiwa ili kuleta maendeleo ya wananchi katika maeneo yao. Huo ndio wajibu wao wa msingi,.

Suala la kusimamia miradi ya maji na yakapatikana kwa wingi, ni suala litakalowasaidia wananchi wa maeneo hayo kupata maji safi na salama.

Kuhusu miradi ya elimu, ni kwamba kijiji kikiwa na shule wanafunzi watapata elimu na hali hiyo itawasaidia kuwaondolea ujinga.

Inapozungumzwa suala la huduma za afya, hiyo nayo ni njia mojawapo ya kuwezesha wananchi kupata huduma bora kama za afya, kuwapunguzia mwendo mrefu wa kutembea kwenda maeneo mengine kuzifuata huduma hizo.

Haya yote yanaposimamiwa na madiwani, kwa kushirikiana na mbunge ikiwamo na halmashauri maendeleo lazima yawepo katika eneo hilo.

Hivi karibu, katika kikao maalumu cha Bajeti cha Baraza la Madiwani, kilichofanyika Mkuranga mkoani Pwani, halmashauri ilipitisha zaidi ya Sh. bilioni 30, ambazo ni bajeti ya mwaka 2020/21 kutumika katika kipindi cha mwaka 2021.

Pamoja na kupitishwa bajeti hiyo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya hiyo, Ally Msikamo, aliwaambia madiwani wa wilaya kwamba ni ‘kipindi cha lala salama’ wanachopaswa wakitumie vizuri.

“Mna miradi mingi katika maeneo yenu. Inatakiwa muisimamie vizuri, ili ilete manufaa kwa wananchi,” anasema

Anaongeza kwamba, hicho kipindi cha lala salama, hakipaswi kuwavunje moyo na kinachotakiwa ni kuhakikisha mnafanya kazi kwa weledi ikiwamo kuwatumikia wananchi.

Mwenyekiti anasema, nafsi yake anatamani madiwani wote waliopo hivi sasa warudi tena katika nafasi zao ili waendeleze yaliyo ya maendeleo, waliyoyaanzisha katika maeneo yao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Juma Abeid, anasema kila diwani ana wajibu wa kuendelea kusimamia miradi na vyanzo vya mapato vilivyoko katika maeneo yake.

Anasema pamoja na kuwa kimebaki kipindi cha ‘lala salama’ ni wajibu wao kuhakikisha wanaendelea kuwatumikia wananchi, ikiwamo kusimamia miradi yao ya maendeleo.

“Ni kipindi cha ‘lala salama’ kinachotakiwa kuendelea kusimamia vyanzo vya mapato. Tusijali kuwa muda umekwisha tuendelee kusimamia miradi ya maendeleo,” anasema.

Mwenyekiti anaongeza kuwa, hata kunapokuwapo diwani anayejihisi hatorudi tena katika nafasi hiyo, ataendelea kuwatumikia wananchi, kwa sababu atakapoishia njiani atampa wakati mgumu, diwani atakayechukuwa nafasi hiyo.

Rai yake ni kwamba, inapotokea diwani anajihisi dikiona hawezi kurudi, aendelee kuwasimamia wananchi, hata akija mwingine atakayeendeleza aliyoyakuta.

# Mkuchika afafanua ushiriki wa nchi utawala bora Afrika

## • APRM, ACDEG zinafanana

**Na Gaudensia Mngumi**

MWAKA 2019 kwa Tanzania unaweza kuwa wa kujivunia kutokana na kupata mafanikio makubwa ya utawala bora hasa kwenye eneo la kupambana na rushwa.

Anasema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, bungeni wakati akichangia maoni kuhusu mafanikio ya mapambano dhidi ya rushwa, kwenye mkutano wa bunge uliomaliza Dodoma Februari 7, mwaka huu.

Anasema Tanzania imeongeza kiwango cha utawala bora na hasa eneo la mapambano dhidi ya rushwa nchini, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti ya mwaka 2019 iliyotolewa na taasisi ya kimataifa ya Transparency International na Global Corruption Barometer Africa 2019.

Anasema Tanzania imefanya vizuri ikiwa na alama 37 na kushika nafasi ya 96 kati ya nchi 180 zilizopimwa ikiwa ni ongezeko la nafasi 21 ukilinganisha na mwaka 2015 wakati huo ikipata alama 30 na kushika nafasi ya 117.

"Kwa matokeo ya takwimu za utafiti, kila mwaka Tanzania imekuwa inapanda nafasi kuanzia mwaka 2015. Mwaka 2018 Tanzania ilipata alama 36 na kushika nafasi ya 99 ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo ilipata alama 36 na kushika nafasi ya 103 ikiwa ni ongezeko la nafasi nne," anasema.

Kwa matokeo ya takwimu zote hizo, kwa upande wa Nchi za Afrika Mashariki, Tanzania imeendelea kushika nafasi ya pili nyuma ya Rwanda kwa vipindi vyote tangu mwaka 2015, anasema Waziri.

Akinukuu ripoti ya Shirika la `MO Ibrahim ya African Governance (IIAG) ambayo hutoa taarifa kuhusu utawala bora kwa nchi za Afrika, mwaka 2018, anasema Tanzania ilipata alama 58.5/100 na kuwa ya 14 kati 54 ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo ilipata alama 57.5chini ya 100 na kuwa nchi ya 17 kwa mataifa ya Afrika yalipopimwa.

Akinukuu pia utafiti uliofanywa nchini na shirika la kijamii la Repoa (Afrometer), 2017, anasema umeonyesha kuwa wananchi saba kati ya 10 waliohojiwa wanasema ushiriki wa serikali katika mapambano dhidi ya rushwa ni mzuri.

Anaongeza kuwa imani hiyo ikaongezeka kutoka asilimia 37 ya kwenye matokeo yaliyotolewa mwaka 2014.

Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na TWAWEZA mwaka 2017 nao umebainisha kuwa asilimia 85 ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia 11 ya waliohojiwa mwaka 2014

SABABU ZA MAFANIKIO

Waziri anasema moja ya sababu kubwa ya mafanikio haya ni utashi wa kisiasa alionao Rais John Magufuli na serikali yake katika kuongoza mapambano dhidi ya rushwa.

"Kutokana na utashi huo, Imani ya wananchi imeongezeka, nidhamu ya watumishi serikalini umeimarika, matumizi mabovu ya fedha ndani ya serikali yamedhibitiwa," anasema.



Waziri Mkuchika . **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI**

Aidha, anasema mifumo ya utendaji kazi imeimarishwa ikiwa ni pamoja na kuziimarisha taasisi zinazosimamia na kupambana na rushwa ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) pamoja na kuanzisha Mahakama ya Mafisadi ambayo inasaidia kudhibiti vitendo vya kifisadi.

"Kutokana na kuimarika kwa utawala bora eneo la mapambano dhidi ya rushwa tumeona mafanikio makubwa kwenye miradi mingi ya serikali," anaongeza.

UTAWALA BORA KIKANDA

Baada ya kueleza mafanikio hayo, wanachama wa uandishi wa habari za utawala bora, walikutana na Waziri Mkuchika na kuzungumza naye kuhusu ushiriki wa Tanzania kwenye masuala ya utawala bora kikanda.

Akijibu swali hilo, anasema Tanzania inashiriki na ni mdau mkubwa wa masuala ya kidemokrasia na utawala bora ya kikanda ikiwamo Umoja wa Afrika (AU), ambayo imeanzisha chombo cha ushauri cha kikanda dhidi ya rushwa.

Chombo hicho kijulikanancho kama African Advisory Body on Corruption (AUABC) kwa mujibu wa Waziri Mkuchika kina makao yake makuu jijini Arusha.

AUABC ilipitishwa na wanachama wa AU jijini Maputo nchini Msumbiji Julai 2003, na hadi sasa wanachama Zaidi ya 40, wameridhia japo vita dhidi ya rushwa ni changamoto kubwa barani Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa za AU zilizoko mitandaoni, majukumu ya AUABC ni pamoja na kuhamasisha kutunga sheria, kuunda taasisi za kuzuia, kudhibiti, kutambua na kuadhibu wahusika wa vitendo vya rushwa ili kutokomeza rushwa ndani ya mataifa ya Afrika na Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na janga hilo.

Waziri anasema pamoja na taasisi hiyo, AU ina chombo cha utawala bora ambacho ni mpango wa Afrika wa Kujitathimini Yenyewe (APRM).

"Tanzania inafanya vizuri na ina mjumbe wa bodi ya APRM ambaye ni Balozi Ombeni Sefue," anasema Mkuchika.

APRM ni mpango unaojihusisha na kuwahimiza wanachama wa AU kuhamasisha na kuongoza kwa kusimamia haki za binadamu , utawala bora, kuongoza kwa haki, kusimamia Amani, usalama wa raia na uongozi unaopata mamlaka kutoka kwa raia.

Kuanzishwa kwa chombo hicho mwaka 2003 ni kuendeleza nia ya Afrika ya kufikia ajenda ya pamoja ya ushirikiano wa kimkakati wa Afrika uliopewa jina la New Partnership for Africa's Development (Nepad).

Mpango wa APRM unalenga pia kubaini na kuvitambua vyanzo bora vya kuleta mabadiliko ili kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii , kuwa na usalama wa kitaifa, huku ukiwaelekeza wanachama wa AU kuijua mianya na vyanzo vya uvunjifu wa amani barani Afrika na kuzuia machafuko, vita na maasi.

Kupitia mpango huo wanachama wa AU hubadilishana na kupeana uzoefu wa uongozi bora unaohusu ushirikishwaji umma, kuwapa fursa ya kujitathimini, kujipima na kuoga mafanikio mema kutoka kwa wanachama.

Pamoja na mpango wa kujitathimini Waziri anasema kuna ushirikiano wa taasisi za kupambana na rushwa za Afrika Mashariki (EAC).Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inashirikiana na vyombo vingine vya nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Tanzania pia ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) na ni mshirika wa Chombo cha Umoja wa Mataifa cha Kupambana na Rushwa (UN Convention Against Corruption). Yote hayo kwa mujibu wa maelezo yake ni jitahada za pamoja za kupambana na rushwa na kuendeleza utawala bora.

MKATABA WA AU WA ACDEG

Tanzania inatizamwa kwa jicho la kuishangaa na baadhi ya wadau wakiwamo wa nje na ndani baada ya kuufumbia macho mkataba wa Afrika wa Demokrasia , Uchaguzi na Utawala Bora (ACDEG) licha ya kwamba imefanya mambo mengi yanayotajwa na AU kwenye mkataba huo. Ni kwanini?

Waziri Mkuchika anapoulizwa swali hilo anasema licha ya kwamba suala ya kusimamia demokrasia na uchaguzi lipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ukweli ni kwamba AU ina vyombo vingi vinavyohusika na masuala ya utawala bora na demokrasia , ambavyo Tanzania ni mwanchama vikiwamo APRM na AUABC.

"Ukiangalia ACDEG ni suala la utawala bora, demokrasia, haki za binadamu ambayo mengi yanafanana na APRM –mpango unaohusu Kujitathimini Wenyewe." Anasema.

Anaeleza kuwa pamoja na mpango wa Afrika wa kujitathimini Tanzania ilikuwa mwanachana wa Mpango wa Kuendesha Serikali kwa Uwazi ulioasisiwa na rais wa zamani wa Marekani Barak Obama na Waziri Mkuu wa Uingereza, David Cameron.

"Tanzania ilijiondoa na kubakia kwenye mpango wa Afrika wa Kujitathimini Yenyewe kwa vile taasisi zote zina malengo yanayofanana. Lakini pia vyombo ni vingi na taifa linapojiingiza kuna gharama zake mnawajibika kulipa ada ya kila mwaka, kutekeleza majukumu yanayohusisha malengo yake. Kwa ujumla kazi zinazofanywa na taasisi hizo zinafanana, "anasema Mkuchika, hivyo kupanga ni kuchagua.

UCHAMBUZI

# Afrika Kusini; 'siasa kali' yakwamisha kwa muda hotuba ya Rais Ramaphosa

- Julius Malema ainyima usingizi ANC
- Rais De Klerk anaibuliwa kelele mpya

**Na Nimi Mweta**

KUNDI la siasa kali za 'ukombozi wa kiuchumi' (Economic Freedom Fighters) majuzi lilileta kizaazaa bungeji jijini Cape Town, wakati Rais Cyril Ramaphosa akianza kusoma hotuba yake ya hali ya nchi katika mwaka uliopita na unaokuja. Wakati ambapo eneo muhimu zaidi la ugomvi na kuvuruga mtiririko wa kiitifaki wa kusikilizwa hotuba hiyo na wabunge ambao ni zaidi ya 400, wabunge 44 wa kundi la EFF walitumia uwepo wa rais wa mwisho wa utawala wa kibaguzi, Frederick de Klerk, kama chombo cha kuvuruga hali ya hewa. Walimtaka Spika Thandi Modise amfukuze kiongozi huyo wa zamani, ombi lililokataliwa.

Wakionyesha kutokujali kuwa Mzee de Klerk alipata nishani ya Nobel pamoja na rais wa kwanza wa Afrika Kusini ya utawala wa walio wengi, Nelson Mandela kwa juhudi zao za kumaliza kwa amani ubaguzi wa rangi na kuweka misingi ya demokrasia mpya, EFF walipiga kelele: 'Kuna muuaji ukumbini.' Rais Ramaphosa alikuwa aanze kusoma hotuba yake saa moja jioni (kwa saa za Afrika Mashariki) ila badala yake akasitisha huku EFF wakiendelea na kelele, wakianza kutoka bungeni kwa taabu na kujaribu kujenga hoja dhidi ya de Klerk. Alipanda tena jukwaani kutoa hotuba yake iliyokuwa inangojwa kwa hamu saa mbili baadaye.

Moja ya hoja zao dhidi ya rais mstaafu de Klerk ni kuwa 'hajatubu' makosa yake makubwa wakati wa ubaguzi wa rangi, huku wakionywa na spika kwa kudhania kuwa wana uhuru usio na mpaka wa kuongea wanalotaka, kuingilia haki za wengine huko ni kuvuruga. Kiongozi wa EFF Julius Malema aliwahi kufanya hivyo katika moja ya hotuba za hali ya taifa mwanzoni mwa mwaka, wakati wa utawala wa rais aliyepita nchini humo, Jacob Zuma. Malema anasisitiza kuwa de Klerk hajawahi kutubu kuwa ubaguzi wa rangi ulikuwa uhalifu dhidi ya binadamu.

Licha ya kuwa kundi la EFF lina takriban moja ya kumi ya wabunge nchini humo lakini kwa jumla ndiyo upinzani halisi kwa utawala wa chama cha ukombozi, African National Congress (ANC). Agenda yao muhimu ilianza kwa kutaka ardhi ambayo imeshikwa na Wazungu inyang'anywe wapewe wazalendo, dai ambalo hata ANC ilianza kulitafakari. Ramaphosa aliendelea kusisitiza uangalifu mkubwa.

Katika hotuba yake ya hali ya taifa majuzi, Rais |Ramaphosa hakuelekeza macho yake katika suala la ardhi kwani linaibuka hapa na pale nyakati za ubaguzi wa Bunge, ila mwelekeo wa uchumi na mkwamo wa mashirika makubwa ya umma. Ndiko ambako Malema, nje ya kutaka de Klerk atolewe bungeni, alikolenga hisia zake, kuwa serikali ya ANC inashindwa kulinda mashirika ya umma na kuyapa mitaji, huku mageuzi yanayotazamiwa yatasababisha mamia ya maelfu ya wafanyakazi (au wazalendo kwa lugha ya EFF) kukosa kazi. Ubinafsishaji ni kama usaliti kwa EFF, wakati Ramaphosa anaona ni njia adhimu kuleta mitaji mikubwa.




Malema Julius

Makelele ya 'kuna muuaji bungeni' yalisikitisha viongozi wa vyama vingine vya siasa bungeni, na hakuna hata kimoja kilichoinuka kuunga mkono hotuba ya EFF na kiongozi wake, au kurudia mashambulizi kwa Ramaphosa. Shambulio dhidi ya de Klerk linaonyesha kuwa itachukua muda kwa makovu ya kipindi cha ubaguzi wa rangi kuondoka nchini humo, kwa sababu wanaokosa kazi kwa sababu hizi au zile wananyooshea kidole ubaguzi kama chanzo cha umaskini.

> "Kwa mfano aliyekuwa rais wa awamu ya pili nchini humo, Thabo Mbeki, alifanya kila awezalo kuzuia Jacob Zuma, akiwa naibu wake, kuwa kiongozi wa ANC na kuongoza nchi, chama hicho...

Ni kawaida kwa fikra za Afrika kutoa aina hiyo ya sababu, iwe ni ukoloni au kunyonya rasilimali.

Wakati katika uchambuzi wa sera uvurugaji wa shughuli za Bunge kwa saa mbili au zaidi hakuongezi hoja za upinzani na hasa huu wa siasa kali kuhusu ni hasa kifanyike kuinua uchumi wa Afrika Kusini, hatari iko kwingine. Kiwewe cha kisiasa cha EFF na wabunge wake 44 ni kielelezo cha hisia za makundi makubwa ya wananchi wa Afrika Kusini wanaojihisi wako nje ya mfumo, na ikitangazwa kuwa mamia kwa maelfu watakosa kazi katika ubinafsishaji, itabidi dola ijiandae kwa uharibifu kiasi fulani. Hata hivyo serikali ya ANC siyo wageni mno katika masuala hayo, kwani wamekuwa wakifanya hivyo katika sekta ya madini na mara kwa mara hali ya vita imezuka maeneo hayo. Maafa yakitokea pale migomo na kuzuia shughuli za migodi, siasa kali wanatulia kidogo, halafu wanaanza tena.

Siasa za Malema ni kitendawili cha siasa za Afrika Kusini, kwani mwanzoni alikuwa kiongozi wa umoja wa vijana wa ANC, halafu akaanza kuonekana kuwa na fedha zisizo za kawaida, makundi ya kisiasa yakimtaka achukue nafasi muhimu zaidi. Sababu mojawapo ni kuwa chama cha kikomunisti cha Afrika Kusini kwa jadi yake kina uhusiano wa karibu na ANC, hivyo wale wasioridhika na mfumo wa uelewano uliopo unaofuata mrengo wa 'nusu ujamaa na nusu utandawazi' hutaka mwakilishi wa dhati zaidi.Wanaamini Ujamaa kamili ndiyo ukombozi wa Afrika Kusini, pamoja na kuwa haihitaji utaalamu wa uchumi kujua nchi itaporomoka.

Kuna upande mwingine wa siasa za Malema ambazo zinatokana na migawanyiko ya kitaifa nchini humo, kuwa tabaka kubwa la wafanyakazi migodini na hata viwandani wanatoka kabila la Wazulu. Kabla ya ukoloni walikuwa ndiyo watemi wa nchi hiyo, wakati wa ubaguzi watawala wao wa jadi wakapuuzia harakati za ukombozi, na mila ina nguvu zaidi maeneo hayo (Kwazulu Natal) kuliko kwingine. Hivyo baada ya ANC kuchukua madaraka ujadi huo umeleta hali ya kutoyaamini makabila ya wasomi (Xhosa na wengine) hivyo uanaharakati katika maeneo mengi unakuwa na chembe ya u-Zulu ndani yake. Hali hii haijaisha bado.

Kwa mfano aliyekuwa rais wa awamu ya pili nchini humo, Thabo Mbeki, alifanya kila awezalo kuzuia Jacob Zuma, akiwa naibu wake, kuwa kiongozi wa ANC na kuongoza nchi, chama hicho kikishinda wingi wa wabunge.

Malema aliongoza vita ya kuzuia hatua hiyo, kwa upande mmoja akidhania kuwa Zuma kwa vile siyo msomi wa ngazi ya kina Mbeki atakuwa mwanamapinduzi zaidi, na kwa hali yoyote ile ni mzawa wa Kwazulu Natal. Akatangaza '..tutaua kwa ajili ya Zuma' yaani asipochaguliwa kiongozi wa ANC nchi haitakalika. Baadaye ilipodhihirika kuna mianya ya kina ya rushwa chini ya Zuma akaanza sasa kumsakama kwa kina.

RUTO KWENYE HATIHATI

# Ahusishwa kwenye utapeli

## Urais 2022 auweka rehani?

Na Moshi Lusonzo

MAKAMU wa Rais wa Kenya, William Ruto, anakabiliwa na shinikizo la kutakiwa kujiuzulu kutokana na kuhusika kwa ofisi yake kwenye kuandaa mpango wa kifisadi wa manunuzi ya silaha.

Mapema wiki hii ofisi yake ilivamiwa na wachunguzi kufuatia madai ya mpango wa kununua silaha wenye gharama ya Dola milioni 397 sawa na Sh. bilioni 39 za Kenya.

Ruto anakiri kwamba watu waliopanga kashfa ya mamilioni ya fedha, walitembelea ofisi yake katika jumba la Harambee House Annex, lakini yeye hana hatia na mpango huo.

Akizungumzia sakata hilo, Ruto akitumia mtandao wa Twitter, alisema alikutana na watu hao akiwamo Waziri wa Michezo wa Kenya, Rashid Echesa, hata hivyo alitumia muda mfupi sana kuzungumza nao.

Hata hivyo, amewaonya wabaya wake kwamba 'mbali na dakika 23 alizokutana na watu hao katika ofisi yake, je ni ofisi gani za serikali zinazohusishwa na zabuni hiyo ambazo walaghai hao walitembelea zinatajwa?

Anaongeza kwamba kile kinachoendelea dhidi ya ofisi yake ni sawa na ufadhili wa porojo katika vyombo vya habari na kusisitiza kuwa ofisi yake haikununua vifaa vya kijeshi vya serikali.

Vyombo vya habari nchini humo vinasema ujumbe wa Twitter wa hivi karibuni unionyesha kwamba aliyekuwa waziri wa michezo Echesa ambaye kwa sasa anakabiliwa na mashtaka ya kuhusika katika mkataba bandia wa kununua silaha, alitumia ofisi ya Ruto ili kuratibu na kufanya biashara hiyo.

Katika ujumbe mwingine wa twitter, Ruto alimtaja Echesa ambaye ni rafiki yake wa karibu na wengine kuwa watu walaghai.

Ruto ambaye ofisi yake ilivamiwa na maofisa wa wachunguzi kuangalia namna tukio hilo lilivyofanyika, alikana kukutana na waziri huyo wa zamani pamoja na wafanya biashara wake walipotembelea ofisi yake na hakuhusika katika mkataba huo.

Echesa ambaye amefikishwa mahakamani akishtakiwa kwa makosa ya ulaghai, alikana madai hayo yeye na wenzake na waliachiliwa kwa dhamana ya Sh. 1,000,000 za Kenya kila mmoja wao.

Katika mashtaka hayo, Echesa na wenzake wanadaiwa kujaribu kujipatia dola za Marekani 395, 442,000 kutoka kwa wafanyabiashara wa Poland kwa kuwaahidi zabuni ya kuiuzia idara ya ulinzi ya Kenya vifaa vya kijeshi.



Rashid Echesa. **PICHA: MTANDAO**

> "Waziri huyo wa zamani wa michezo alifutwa kazi na rais Uhuru Kenyatta, mwezi Machi mwaka 2019 kutokana na sababu zisizojulikana.

Waziri huyo wa zamani wa michezo alifutwa kazi na rais Uhuru Kenyatta, mwezi Machi mwaka 2019 kutokana na sababu zisizojulikana.

Wakati akifukuzwa, Echesa, aliliambia gazeti la Daily Nation, wakati huo kwamba hakuambiwa kwanini alikuwa anafutwa kazi , lakini aliamini ni kutokana na kumuunga mkono Ruto.

Stakhabadhi za mahakamani zinaonesha kwamba maofisa wa polisi wanaamini 'biashara' hiyo ilifanyika mwisho wa mwaka jana katika ofisi ya naibu wa rais katika jumba la Annex.

Tayari wapelelezi nchini Kenya wanaendelea kuwahoji wafanyakazi katika ofisi ya naibu huyo. Echesa pia ameshtakiwa na kujifanya kuwa msaidizi binafsi wa naibu wa rais Ruto.

Polisi wanasema kwamba Echesa tayari alikuwa amelipwa takriban dola 115,000.

### ODINGA ATAKA AONDOIKE

Mtu ambaye anaaminika kuwa adui yake wa kiasiasa, Railla Odinga, amemtaka makamu wa rais kujiuzulu haraka kwa sababu ofisi yake imehusishwa na mpango huo.

Odinga na Rais Uhuru Kenyata, wameonekana kuwa karibu kisiasa kitendo ambacho kinaonekana kwa watu wanaomuunga mkono Ruto, kuwa kashfa hiyo ni kama njia ya kumuondoa kiongozi hiyo katika mbio za siasa mwaka 2022.

Gavana Ngilu, anasema sakata kama hilo linalomuhusisha Ruto si mara ya kwanza na safari hii ni lazima akae kando.

"Lazima akae kando uchunguzi ufanyike, kwani si mara ya kwanza kwa ofisi yake kuhusishwa na mambo kama haya," anasema Gavana Ngilu.

> "Lazima akae kando uchunguzi ufanyike, kwani si mara ya kwanza kwa ofisi yake kuhusishwa na mambo kama haya," anasema Gavana Ngilu.





Wafanyabiashara wa ndizi katika Soko la Kalasha Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, wakiendelea na biashara sokoni hapo juzi, huku eneo hilo likiwa katika mazingira ya uchafu, hali inayoweza kusababisha magonjwa ya mlipuko. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mzindakaya ataka reli kuunganisha bandari

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

MWANASIASA mkongwe nchini, Chrisant Mzindakaya, ameishauri serikali kutekeleza mipango ya ujenzi wa reli inayounganisha Bandari ya Kiwira wilayani Kyela na Bandari ya Kasanga mkoani Rukwa ili kurahisisha usafiri wa mizigo na abiria katika maeneo hayo.

Mzindakaya aliyasema hayo kwa niaba ya wawekezaji wazawa kwenye Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Songwe lililofanyika katika Mji wa Vwawa, wilayani Mbozi.

Alisema mipango ya serikali ya kuendeleza mikoa ya Kusini iliyojulikana kama Mtwara Corridor, iliainisha kuendeleza miundombinu ya reli kuunganisha mikoa ya kusini kuanzia Bandari ya Mtwara iliyopo kwenye Bahari ya Hindi hadi Bandari ya Kasanga iliyopo Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa.

"Tuitekeleze mipango hii kwa faida ya maendeleo ya uchumi wetu, tunaihitaji sana reli iliyopangwa kuanzia Ziwa Nyasa wilayani Kyela hadi Bandari ya Kasanga katika Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa, naiomba serikali ianze mchakato wa ujenzi wa reli hiyo," alisema Mzindakaya.

Mzindakaya alisema kwa sasa ushindani mkubwa wa biashara baina ya taifa moja na lingine uko kwenye miundombinu ya uchukuzi, hivyo Tanzania haipaswi kuzubaa katika suala hilo badala yake itekeleze mipango mizuri iliyopo ili kumudu ushindani huo.

Alisema mipango iliyokuwapo kupitia Mtwara Corridor ni kujenga reli kuanzia Bandari ya Mtwara hadi Ziwa Nyasa kwa upande wa Ruvuma kisha reli hiyo iendelee tena kuanzia wilayani Kyela hadi mkoani Rukwa.

Alisema mipango hiyo ilitakiwa kwenda sambamba na ujenzi wa meli za mizingo na abiria katika Ziwa Nyasa ambazo zingekuwa kiungo kizuri cha reli hizo.

"Nashukuru serikali imekwishaanza ujenzi wa meli katika Ziwa Nyasa, maana meli mbili za mizigo zimekwishajengwa na sasa wanakamilisha meli moja ya abiria, lakini meli hizi zingekuwa na tija kama ujenzi wa reli hiyo nao ungefanyika," alisema Mzindakaya.

Alisema kuwa endapo reli hiyo itajengwa itakuza biashara kati ya Tanzania na wananchi wa Congo DRC ambao wanapenda sana kufanya biashara na Tanzania, lakini wanakumbana na vikwazo vingi pale wanapolazimika kupitia nchi ya Zambia.

Aidha, Mzindakaya alisema reli hiyo itakuwa na tija kubwa kwa vile itatumiwa na mataifa mengi yaliyo Kusini mwa Tanzania ambayo hayana bandari, sambamba na kuifanya Bandari ya Mtwara kufanya kazi kwa tija.

Mgeni rasmi katika ufungaji wa kongamano hilo, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ambaye alisema upo umuhimu mkubwa wa Tanzania kujenga Bandari Kavu mkoani Songwe ili kunufaika na soko kubwa la nchi zilizo kusini mwa Afrika.

Alisema kutokana na kasi ya maendeleo, hapaswi tena watu wa mataifa ya Kusini mwa Afrika kusafiri hadi jijini Dar es Salaam kufuata bidhaa na badala yake wanapaswa kuzichukulia jirani kupitia bandari kavu itakayokuwa imejengwa mkoani Songwe.

"Nchi nyingi za Kusini mwa Afrika hazina bandari, hii ni fursa kubwa kwetu, lakini hatupaswi kuwaacha wafuate mizigo yao Dar es Salaam wao wenyewe na badala yake tunatakiwa kuwasogezea karibu kwa kujenga bandari kavu katika mikoa hii iliyo pembezoni na kwa mtazamo wangu, naona Mkoa wa Songwe ndio wenye sifa kubwa ya kuwa na bandari hiyo kavu," alisema Pinda.

# Wauza ndizi wahofia kipindupindu

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

WAFANYABIASHARA wa ndizi wa soko la Kalasha katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, wailalamikia Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kutokuboresha miundombinu ya soko hilo licha ya kuendelea kukusanya mapato.

Wamedai kuwa kuna hatari wakakumbwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu kutokana na eneo hilo kuwa chafu na mitaro ya maji haijaboreshwa hali ambayo inafanya maji machafu yasitoke.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wafanyabiashara hao waliuomba uongozi wa Halmashauli ya Rungwe kuwaboreshea mazingira ya soko hilo ili wafanye biashara vizuri na walipe kodi na michango mingine kwa amani.

Mmoja wa wananchi hao, Pili Luvanda, alisema kutokana na uchafu wa soko hilo ndio maana wanalazimika kulikimbia na kwenda kuuza ndizi zao kwenye hifadhi ya barabara ambako ni hatari.

Alisema katika eneo hilo ndizi zao huwa zinachafuka na hata wateja wanashindwa kulifikia, hivyo akaomba serikali iwasaidie kuyaweka mazingira kuwa safi.

"Hapa tunalipia ushuru kila siku na serikali inajuwa kuwa eneo ni chafu, lakini inatuma watu wake kuja kuchukua ushuru lakini haifanyii maboresho, tunaomba watusaidie kuboresha soko hili," alisema Luvanda.

Alisema eneo la barabarani wanakofanyia biashara, walishakatazwa na serikali, lakini wanalazimika kwenda kupanga ndizi zao hapo kwa sababu hawana mahali pengine pa kwenda.

Agrey Twalangete, alisema kwa sasa hawana amani na eneo hilo ambalo lilitengwa kwa ajili ya soko kwa sababu linahatarisha afya zao.

Alisema eneo hilo linatoa harufu mbaya kutokana na maji pamoja na takataka zilizooza kutapakaa ovyo na hivyo kuwafanya washindwe kutulia na kufanya biashara zao.

"Sisi hatuhitaji kulumbana na serikali na ndiyo maana tunalipa kodi na ushuru, sasa tunaiomba serikali ya wilaya yetu itusaidie hata kwa kuweka mitaro vizuri ili maji yaendelee kupita hasa kipindi hiki cha mvua," alisema Twalangete.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter, alikiri soko hilo kuwa chafu.

# Wadau waombwa uboreshaji wa elimu

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

WADAU wa maendeleo katika Wilaya ya Chunya, pamoja na wazazi, wametakiwa kuendelea kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri na kuongeza ufaulu.

Hayo yalisemwa juzi na Diwani wa Mbugani, Bosco Mwanginde, alipokuwa anakabidhi madawati 15 katika Shule ya Sekondari Isenyela na kompyuta moja katika Shule ya Msingi Isenyela.

Alisema wananchi na wadau mbalimbali wana nafasi kubwa ya kutoa michango ya kuboresha sekta ya elimu na kufikia uchumi wa viwanda na serikali inasisitiza hilo.

"Ili sekta ya elimu iweze kukua na kuwa na manufaa ni lazima wadau na wazazi kuhakikisha tunashirikiana na serikali kuhakikisha miundombinu inakuwa mizuri na inawavutia wanafunzi kuipenda shule," alisema Mwanginde.

Mwanginde alisema katika kata hiyo kuna wadau mbalimbali ambao ni wafugaji, wachimbaji wa madini na wafanyabiashara, hivyo hayo matatizo wanayamaliza.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Isenyela, Bereth Gerrard, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na hiyo ya upungufu wa madawati.

Alisema shule hiyo ilikuwa na upungufu wa madawati 45 na baada ya kupatiwa msaada wa dawati 15 na Diwani wa Kata hiyo, uhitaji umekuwa ni madawati 30.

Alisema kamati ya shule hiyo inaendelea na harakati za kuwatembelea wadau mbalimbali ili wasaidie kutatua matatizo yanayoikabili shule hiyo.

Naye Kaimu Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Chunya, Porcup Mbunda, alisema msaada alioutoa diwani huyo unasaidia kupunguza changamoto ya wanafunzi kukaa chini wakiwa madarasani.

Alisema ili kuhakikisha matatizo yanayozikabili shule wilayani humo ni wajibu wa jamii kuchangia shughuli zote za sekta ya elimu badala ya kuiachia serikali ifanye kazi hizo.





# Tanzania yapiga hatua kugundua maambukizi TB

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto, imepiga hatua kwa kuwa na uwezo mkubwa wa kugundua wenye maambukizi ya kifua kikuu (TB) nchini kwa ongezeko la asilimia 18.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Dk. Leonard Subi, wakati akifungua kikao cha mapitio na tathmini ya mpango wa taifa wa kudhibiti kifua kikuu na ukoma (NTLP) ambao unajumuisha wadau mbalimbali wa kifua kikuu nchini.

"Kikao hiki ni cha mapitio na tathmini ya mpango mkakati wa miaka mitano ambao unatimilika mwaka huu, tumekuwa tukifanya mapitio haya kila baada ya miaka mitano hadi sita, ambapo mwaka 2014 tuliweza kujitathmini tuna uwezo gani wa kupambana dhidi ya kifua kikuu na ukoma," alisema.

Dk. Subi alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kwani uwezo wa kugundua TB umeongezeka kutoka asilimia 37 mwaka 2015 hadi asilimia 53 ya wagonjwa wanaokadiriwa kuwa na kifua kikuu mwaka 2018. "Lakini vifo vitokanavyo na kifua kikuu vimepungua kwa zaidi ya asilimia 27, haya ni mafanikio makubwa sana ya mpango huu," alisema.

Aidha, Dk. Subi alisema licha ya mafanikio hayo, hivi sasa wameongeza uwezo wa kuchunguza TB kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa kipimo cha kielektroniki (Gene-Expert Mashine) ambapo wizara imeweza kununua mashine zipatazo 239 na kuzisambaza kwenye vituo vya afya vya msingi nchi nzima.

Alisema vipimo hivyo vinatoa majibu ya mgonjwa ndani ya saa mbili tofauti na zamani walipokuwa wakitumia harubini na kutoa majibu kwa zaidi ya saa 48. Alisema kupitia elimu ya afya kwa umma ambayo hutolewa na wizara kupitia NTLP, wananchi wanaelewa na imesaidia kupungua kwa magonjwa haya na watu kwenda vituo vya kutolea huduma kwa uchunguzi na matibabu.

"Tanzania ni nchi mojawapo imefanikiwa kulingana na malengo ya kimataifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwani tunaonyesha mwelekeo mzuri kwa kasi ambayo tumeionyesha kwenye kifua kikuu."

Kwa upande wa ugonjwa wa ukoma, alisema kuwa nchi imefikia kiwango cha kuondosha ukoma kabisa na kubakiza halmashauri kumi na sita, takribani wagonjwa 2,000 wanakadiriwa kuwa na ugonjwa huo nchi nzima hivyo wanaendelea na mkakati wa kuhakikisha kuwafikia wagonjwa wote na kuwatibu ili kupunguza madhara ambayo wamekuwa wakiyapata ikiwamo ulemavu.

Tathmini hiyo itafanyika kwenye baadhi ya mikoa ambayo italeta matokeo na changamoto ili kutengeneza mpango mkakati mwingine wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 ili kuweza kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya kifua kikuu.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha kwa waandishi wa habari, mkoani humo jana, gari lililokamatwa na jeshi hilo, hivi karibuni kwa kusafirisha wahamiaji haramu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waomba mifereji kupitisha maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Kata ya Nzuguni jijini Dodoma, wameiomba serikali kuwawekea mifereji ya kupitishia maji katika barabara ya Nzuguni 'B' na ile ya kuelekea kwa Masister ambayo hivi sasa haipitiki kutokana na kuharibika kwa mvua zinazoendelea kunyesha.

Aidha, wamedai kuwa kutokana na hali hiyo hivi sasa wamekuwa wakipata wakati mgumu kwenda katika majukumu yao ya kila siku na watoto kukosa shule kutokana na magari ya shule na daladala, kushindwa kufika katika eneo hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, wakazi hao walidai kwa sasa hali imekuwa ngumu zaidi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kuharibu miundombinu ya barabara pamoja na daraja katika eneo hilo, hivyo kuwapa wakati mgumu kufika mjini na kurudi majumbani.

Jasmine Ramadhani, mkazi wa eneo hilo alisema sasa hivi wengi wenye magari wameyaegesha kutokana na kukwama na wakati mwingine kusombwa na maji, hivyo wamekuwa wakitumia usafiri wa bodaboda kufika stendi ya daladala za kwenda mjini.

"Mpaka ufike kwenye stendi ya daladala, bodaboda tu ni Sh. 2,000 hapo unaenda mjini bado hujarudi, lakini ukiwa katika bodaboda unapandisha miguu juu ili usilowane, wakati mwingine inabidi usivae viatu, tunawakati mgumu sana, tunaomba tusaidiwe," alisema Jasmine.

Naye Daudi Mzengo, alisema wamekuwa wapiga kelele kila siku kwamba wanahitaji msaada kutokana na barabara hiyo kujaa maji, lakini wanaohusika wamekuwa kimya.

Alisema kutokana na gharama za nauli kuwa juu anatamani kupanga chumba kimoja eneo la mjini kwani amekuwa akikutana na wakati mgumu wakati wa kwenda na kurudi nyumbani.

Naye Habel Steven, alisema kikosi cha Zimamoto na Ukoaji kimekuwa kikisaidia watu kuvuka katika daraja la kwa Masister kutokana na kubomoka.

"Daraja limebomoka kuvuka ni shida sasa hivi kikosi cha Zimamoto na Ukoaji Mkoa wa Dodoma ndio wanaotuvusha tunawaomba Tarura watusaidie," alisema.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) Jiji la Dodoma, Geofrey Mkinga, alisema tatizo la kujaa maji katika barabara hiyo ni kutokana na wakazi wa maeneo hayo kujenga kwenye mifereji ambayo ilitakiwa kupitisha maji.

"Watu wamejenga katika maeneo ambayo maji yanatakiwa kupita, hivyo hakuna sehemu ya kupitisha maji ndio maana barabara inajaa maji, tunatakiwa kuwapa elimu wajue tatizo ni wao," alisema.

Alisema Tarura imeanza usanifu wa barabara hiyo ili kujengwa kwa kiwango cha lami katika siku za baadaye.

## Jafo asikitika vichwa vikubwa, mgongo wazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameeleza kusikitishwa na jinsi ambavyo watu wenye matatizo ya vichwa vikubwa na mgongo wazi kutowekewa mikakati ya kukabiliana na changamoto walizonazo.

Jafo aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa ofisi ya Shirika la Kimataifa la Lishe jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kuhamia makao makuu ya nchi.

Alisema watu wenye matatizo ya mgongo wazi na vichwa vikubwa wamekuwa hawatembelewi ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo isipokuwa kukutana nao kwenye matukio mbalimbali.

"Ukienda ukikaa na familia hizi hasa kinamama hawawezi kushiriki katika shughuli za uchumi inakuwa ni tatizo kwani muda wote wamebeba watoto mgongoni, ukifika utaona familia husika hata kujenga uchumi wao ni tatizo sana," alisema Jafo na kuongeza:

"Kwa bahati mbaya sana hatuzitembelei familia hizo, tunakutana nazo kwenye matukio ya Siku ya Vichwa Vikubwa, Siku ya Mgongo Wazi au maadhimisho ya lishe, lakini kama ukitembelea hizi familia zenye matatizo utagundua tatizo hili ni kubwa, wadau mbalimbali tuendelee kushirikiana na serikali katika suala hili."

Hata hivyo alisema kiwango cha udumavu kwa watoto nchini kimepungua kutoka takribani asilimia 50 mwaka 1991 hadi 32 kwa sasa.

Alisema kiwango cha asilimia 32, bado ni kikubwa hivyo serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wanatakiwa kuongeza kasi ili kupunguza asilimia hizo.

Jafo alilipongeza shirika hilo kwa kutekeleza mradi wao wa lishe katika mikoa 12 nchini yenye halmashauri 69, hivyo kuwashauri katika mpango wao wa ushirikiano na serikali wanaweza kwendakatika halmashauri nyingi zaidi.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Nutrition International nchini, Dk. Daniel Nyagawa, alisema shirika limekuwa likishirikiana na Wizara ya Afya na Tamisemi katika kusaidia afua za lishe kwa wanawake, watoto, wajawazito, kundi la lika balehe na watoto wachanga.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Nutrition International, Joel Spicer alisema kufungua ofisi Dodoma na kufanya kazi na serikali kutasaidi kukabiliana na changamoto ya udumavu nchini.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Nutrition International, Dk. Richard Pendame, alisema makao makuu Afrika yapo Dakar Senegal lakini kwa ushawishi wa Mkurugenzi Mkuu Joel Spicer alitekeleza uamuzi wa kuanzisha ofisi nchini Tanzania.

Alisema baada ya kutembelea Tanzania alibaini kwamba kuna haja ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuanzisha ofisi jijini Dar es Salaam ili kusaidiana na serikali katika kampeni ya kukabiliana na udumavu nchini.



**HABARI ZANZIBAR**

## Ubalozi Marekani kuwanoa Kiingereza wanafunzi TZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UBALOZI wa Marekani nchini Tanzania, unakusudia kutanua programu ya mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa Tanzania ili kuwajengea uwezo katika masomo ya vyuo na ushindani kwenye soko la ajira wanapomaliza masomo.

Ofisa wa ubalozi huo nchini Tanzania anayeshughulikia masuala ya lugha ya Kiingereza kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, George Chinnery, alisema programu hiyo iitwayo 'Access', inalenga kuwajengea vijana mustakabali mzuri wa maisha.

Akizungumza wakati wa mahafali ya kuwatunuku vyeti wahitimu wa mafunzo hayo kutoka Zanzibar yaliyofanyika juzi katika Kituo cha Walimu Beit el Ras, Chinnery alisema ofisi yake inaridhika na kazi kubwa iliyofanywa na walimu na ushirikiano wa wazazi kuwaruhusu watoto wao kushiriki mafunzo hayo.

Alieleza kuwa Serikali ya Marekani ilianzisha programu ya kwanza ya mafunzo ya Kiingereza nchini Morocco mwaka 2004, zaidi ya wanafunzi 150,000 kutoka nchi 35 duniani wakiwamo 400 wa Tanzania.

Alisema kufanikiwa kwa programu hiyo kumetokana na jitihada kubwa na kujitoa kwa walimu, wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu ikiwamo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kufanya madarasa hayo kuwa ya kisasa na yanayoleta mafanikio makubwa.

"Lengo sio tu kukuza Kiingereza, bali pia kuimarisha elimu kote nchini Tanzania. Kupitia programu hii, pia walimu na wanafunzi wanapata fursa ya kwenda Marekani ili kujiendeleza na kupata mafunzo ya uongozi," alisema.

Aliwaeleza wahitimu hao kuwa, wao ndio wasimamizi wa maisha yao ya baadaye kutokana na elimu waliyopata, ambayo iliambatana pia na kazi za kujitolea katika jamii ikiwamo kusafisha mazingira kwenye nyumba za wazee na maeneo ya utalii.

Aliwataka waendelee kuhamasishana wenyewe ili wawe mfano bora kwa jamii na akiwataka wazazi kuwasaidia watoto wao kila wanapotaka kutafuta fursa zaidi za elimu.

# Hoteli za kitalii zaonywa unyanyasaji wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Zanzibar imesema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyakazi wa sekta binafsi hasa wa hoteli za kitalii kufanyiwa unyanyasaji na kutopatiwa mikataba ya kazi hali inayosababisha kufukuzwa wakati wowote.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Shadia Suleiman, wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Katika swali lake la msingi, Jaku alitaka kujua hatua zilizochukuliwa kwa maofisa wakaguzi kazi wasiotekeleza wajibu wao ipasavyo.

Naibu Waziri Shadia alisema maofisa wakaguzi wa kazi wanaofika hotelini hawafanyi kazi ipasavyo kwa vile wanaonekana kushirikiana na wamiliki wa hoteli na kupatiwa chakula na fedha na kuacha kushughulikia matatizo ya wafanyakazi au kuwachongea kwa waajiri wao. Alisema serikali kupitia wizara yake iko mstari wa mbele kufuatilia tuhuma mbalimbali zinazowasilishwa kwa watendaji wake katika suala hilo.

"Naomba nitanabahishe kwamba si maofisa kazi pekee ambao wanafanya ukaguzi katika taasisi hizo bali hata Mamlaka ya Mapato (TRA), Uhamiaji, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na vyama vya wafanyakazi hufika katika maeneo tofauti katika utekelezaji wa kazi zao," alisema.

Alieleza kuwa wizara yake haitolifumbia macho wala kumwonea aibu ofisa yeyote atakayethibitika kujihusisha na jambo lolote ambalo lina mwelekeo wa unyanyasaji wa wafanyakazi.

Alisema kufanya hivyo ni kukiuka miiko na maadili ya utumishi wa umma na kwa kipindi hiki bado wizara yake haijapokea malalamiko kwa wafanyakazi wa hoteli kufanyiwa unyanyasaji.



Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme, Hassan Ali Mbarouk, akijibu swali lililoulizwa katika mkutano wa utekelezaji wa mpango kazi kwa kipindi cha Julai -Desemba 2019, uliofanyika katika ukumbi wa Ikulu Mjini Zanzibar jana, chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani). **PICHA: IKULU ZNZ**

# Dk. Shein ataka sheria za vyakula kupitiwa upya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuna umuhimu wa kutizama upya sheria zinazosimamia mwenendo wa usalama wa chakula nchini, ili kuondokana na malalamiko mbalimbali ya wafanyabiashara.

Akipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi ya Wizara ya Afya, kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019, aliutaka uongozi wa wizara hiyo kuziangalia upya sheria zinazosimamia usalama wa chakula, hasa katika suala la ukaguzi wa bidhaa zinazotoka na kuingia nchini.

Alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu tozo wanayolipa kugharamia ukaguzi huo.

Alisema wafanyabiashara wanalalamikia gharama hizo, kwa kigezo kuwa dhima ya kuthibitisha ubora wa bidhaa uko mikononi mwa serikali badala ya wao kubebeshwa mzigo huo.

Dk. Shein alisema pamoja na sheria zilizopo kuwa na uwiano katika nchi nne za Afrika Mashariki, kuna umuhimu wa kuzipitia upya kwa kuzingatia kuwa serikali ndiyo yenye dhima katika kufanya utafiti na kupata matokeo.

Dk. Shein alisema wafanyabiashara wanalalamikia kuwapo kwa utitiri wa taasisi za uchunguzi, jambo linaloongeza urasimu.

Alieleza kuwa mbali na taasisi hizo kuongozwa na sheria yake kila moja, kuna umuhimu wa viongozi kukaa pamoja ili kuwa na mfumo maalumu wa utoaji wa tozo moja.

Alisema serikali haiwezi kupuuza malalamiko ya wafanyabiashara hao na itafanya juhudi za kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo ili kuondokana na malalamiko.

Aliitaka wizara hiyo kusomesha na kuwaendeleza wafanyakazi wake katika fani nyanja tofauti, ikiwamo za injinia na nyingine zenye upungufu ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi.

Rais Dk. Shein aliutaka uongozi wa wizara hiyo kuhakikisha huduma zote za maabara zinafanyika ndani ya hospitali za serikali badala ya kufanyika taasisi za nje, kwa kigezo kuwa serikali inatenga kiwango kikubwa cha fedha.

Naye Waziri wa Wizara ya Afya, Hamad Rashid Mohamed, akiwasilisha muhtasari wa utekelezaji wa mpango kazi wa wizara hiyo, alisema katika kipindi hicho wizara ilipanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 57.8, kati yake Sh. bilioni 47.8 kwa ajili ya idara na taasisi zilizomo ndani ya wizara hiyo na Sh. bilioni 9.9 kwa ajili ya Hospitali ya Mnazimmoja.

Pia katika kipindi hicho wizara hiyo imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mafanikio makubwa ikiwamo ununuzi wa dawa na kuwezesha upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya afya na hospitali kwa asilimia 90.

Alisema katika kipindi hicho gharama za usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi zilipungua kutoka Sh. 341,292,993 hadi kufikia Sh. 32,186,488.

Wakati huo huo, Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa wizara hiyo, alisema katika kipindi hicho wizara ilikadiria kununua tani 3,500 za karafuu, lakini hadi kufikia Desemba 2019, ilinunua tani 1,638.5 zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 20.3 na kiwango kikubwa cha karafuu hizo ziliuzwa katika nchi za India na Singapore.

# 61 mbaroni tuhuma uhamiaji haramu

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WATU 61 ambao wanadaiwa kuwa wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro, kwa tuhuma za kuingia nchini bila kuwa na kibali.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Mugabo Wekwe, wahamiaji hao walikamatwa Februari 16, mwaka huu majira ya usiku katika Kitongoji cha Kwampangile kilichopo kijiji na kata ya Doma Tarafa ya Mlali wilayani Mvomero.

Kamanda Wekwe alisema askari Polisi wakiwa doria ya misako mbalimbalii walipokea taarifa kutoka kwa msiri za kuwapo kwa kundi la watu wasiofahamika.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, walifika eneo la tukio na kufanikiwa kuwakuta wahamiaji hao wakiwa wamejificha porini.

Kamanda Wekwe alisema baada ya kuwahoji walibainika kuwa ni wahamiaji haramu ambao ni raia wa Ethiopia, walioingia nchini bila kibali na kutekelekezwa tangu Februari 15, mwaka huu katika eneo hilo na mwenyeji wao, ambaye anaendelea kutafutwa na Polisi.

Alisema wahamiaji hao wana umri kati ya miaka 19 hadi 35, na kwamba uchunguzi na msako unaendelea kubaini waliowaingiza pamoja na washirika wenzao wanaofanya shughuli za usafirishaji wa binadamu.

Kamanda Wekwe alisema hatua za kuwafikisha watuhumiwa mahakamani zinafuatwa kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kufichua uhalifu na wahalifu wa aina zote.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, akionyesha mifuko mbadala isiyokuwa na nembo na hairuhusiwi kutumika (kulia) na mifuko yenye nembo inayoruhusiwa kutumika hapa nchini, katika mkutano na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: OMR**

# Vijana watakiwa kuchangamkia mikopo, zawadi fedha, bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka vijana nchini kuchangamkia fursa za mikopo na zawadi za fedha taslimu na bodaboda kwa lengo la kurasimisha biashara zao.

Ushauri huo ulitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, kwenye uzinduzi wa NMB Mastaboda uliofanyika Peramiho nje kidogo ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma na kukutanisha wendesha bodaboda zaidi ya 200.

Alisema sekta ya bodaboda kwa sasa inaheshimika na kutambulika kama ajira rasmi, hivyo wahusika hawana budi kutumia fursa hiyo kujinufaisha.

Kupitia kampeni ya mastaboda, waendesha bodaboda wamerasimishwa, hivyo kuaminika na kupewa msaada kupitia mikopo ya fedha hata ya vyombo vya kazi kama pikipiki za miguu miwili na miguu mitatu.

Mhagama alisema kwa sasa serikali inatambua sekta hiyo kuwa rasmi na kuahidi vijana wote nchini kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kushirikiana na wabia kama Benki ya NMB.

"Kuwa na fedha ni jambo moja ila namna ya kuzitunza ni jambo jingine, kuna haja ya mafunzo kutolewa kwenu yatakayowaongoza katika matumizi mazuri ya fedha kwa ajili ya maendeleo ya sasa na baadaye," alisema.

Aliongeza kuwa: "Nimeambiwa hapa na Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB kuwa kwa sasa hamtapata shida, abiria anaweza kukulipa kutoka kwenye benki yoyote na ikaingia kwenye akaunti yako moja kwa moja."

Alisema asilimia 56 ya nguvukazi nchini ni vijana na ajira rasmi hivi sasa ni chache, hivyo kuwataka vijana kutafuta mifumo tofauti ya ajira na kujiajiri au kusaidiwa kutengeneza ajira.

"Leo hii Benki ya NMB inataka kubadilisha mfumo wa ajira ya bodaboda kwenda kuwa ni shughuli iliyorasimishwa na kuwa ajira yenye staha miongoni mwa ajira nyingine zinazopatikana Tanzania," alisisitiza.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Benedicto Baragomwa, aliwahakikishia waendesha bodaboda na serikali kuwa huduma hiyo itatoa fursa kwa maelfu ya waendesha bodaboda nchini kwa kutumia huduma za benki, hatua itakayoimarisha usalama wa fedha na mali zao.

Kiongozi wa bodabada ambaye amehitimu chuo kikuu na kukosa ajira rasmi, alisema hadi kufikia mwaka 2019, idadi ya madereva bodaboda katika Mkoa wa Ruvuma ilifikia 85,000.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Pololet Mgema, alipongeza benki hiyo kwa kuanzisha huduma hiyo ambapo amewaomba waendesha bodaboda kujiunga sambamba na kuchukua vitambulisho vya wajasiriamali ili kupata mkopo kutoka benki hiyo.

# Waziri avutiwa kasi ya viwanda

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amefanya ziara ya siku moja kutembelea baadhi ya viwanda katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, huku akiipongeza kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji.

Katika ziara yake jana Mjini Kibaha, Waziri Bashungwa akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Riziki Shemdoe, alieleza namna alivyoridhishwa na halmashauri hiyo inavyotekeleza sera ya uwekezaji wa viwanda kwa vitendo.

Akiwa katika kiwanda cha kuunganisha mabasi makubwa kinachomilikiwa na Kampuni ya BM Motors, alimpongeza mwekezaji wa Kitanzania kwa uwekezaji wake wenye tija.

Alisema, kitendo cha mwekezaji huyo mzawa kuwekeza hapa nchini, ni manufaa kwa Taifa katika suala la kodi, ajira kwa Watanzania, lakini ni fursa kwa viwanda vingine kwani malighafi zinazotumika zinapatikana nchini.

Mbali ya kiwanda hicho, Waziri Bashungwa pia alitembelea kampuni ya wawekezaji wazawa ya GF Vehicle Assemblies kilichopo eneo la Tamco.

Kampuni hiyo ambayo inatarajia kuanza kuunganisha magari mchanganyiko yenye uzito usiozidi tani nane, uzinduzi wake unatarajia kufanyika Mei mwaka huu.

Bashungwa aliwapongeza wawekezaji waliowekeza nchini, huku akitoa rai kwa mamlaka na taasisi zinazohusika na viwanda vidogo vidogo zikiwamo SIDO, DIT na NEMC kuwa karibu na wawekezaji kwa ushauri wa kitaalamu.

Jonas Nyagawa, ni Mkurugenzi wa Kampuni ya BM Motors, alisema mabasi yanayounganishwa katika kiwanda hicho, yana uwezo wa kubeba abiria kuanzia 50.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Vehicle Assemblies, Imran Karmali, alisema atakapoanza kuunganisha magari 100 na ajira zitakuwa 100 zinaendelea kuongezeka kulingana na namna kiwanda kinavyoongeza idadi ya kuunganisha magari.

Halmashauri ya Mji wa Kibaha imetenga eneo mahususi la viwanda vikubwa lenye ukubwa wa ekari 1,246 la Zegereni umbali wa kilomita 4.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro.

## HABARI KIMATAIFA

## Raia 40 wa Marekani waambukizwa virusi vya corona

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imewarudisha nyumbani raia wake waliokuwa wamekwama ndani ya meli, iliyokuwa na watu walioambukizwa na virusi vya corona nchini Japan.

Hadi jana idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na ugonjwa huo iliongezeka na kufikia zaidi ya 1,700.

Ripoti zinasema kuwa, ndege mbili zilizowabeba raia wa Marekani, waliokuwa ndani ya meli hiyo iliyokuwa imetengwa, zimeondoka katika uwanja wa Haneda jijini Tokyo nchini Japan.

Wamarekani waliokuwa ndani ya meli hiyo iliyokuwa imezuiwa, walikuwa 400, na wamekuwa katika hali hiyo tangu Februari 3, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, licha ya maofisa nchini China kusema kiwango cha maambukizi ya virusi vya corona kinapungua, inaripotiwa kuwa idadi ya watu walioambukizwa virusi hivyo kufikia siku ya Jumatatu ni zaidi ya 70,500.

Idadi kubwa ya maambukizi hayo, yanasalia katika mji wa Wuhan katika Jimbo la Hubei, wakati huu Shirika la Afya Duniani (WHO) likisema kwa sasa ni vigumu kueleza ni lini maambukizi haya yatafika mwisho.

**RFI**

# Watoto wafariki kwa kula chapati zenye sumu

**KAMPALA, Uganda**

WATOTO wawili nchini Uganda wafariki dunia huku wengine 11 wakipelekwa hospitali baada ya kula vitafunwa aina ya chapati vilivyotengenezwa kwa sumu ya kuua wadudu badala ya mafuta.

Watoto wote wanatoka familia moja Budumba, magharibi mwa Uganda na kusemekana kwamba walikuwa na umri wa miaka mitano hadi sita.

Taarifa zinaeleza kuwa watoto hao walijipikia wenyewe vitafunwa hivyo ambavyo vinafahamika kama Kabalagala.

Inasemekana kwamba miongoni mwa viambato walivyotumia wakati wanapika ilikuwa dawa ya kuua wadudu inayonyunyizwa kwenye matikiti maji na mboga zinazokuzwa wakidhani kwamba ni mafuta.

Taarifa zinaeleza kuwa watoto hao walianza kutapika na kupelekwa hospitali ya Busolwe ambapo wawili wao waliaga dunia, huku wengine 11 wakiendelea kupata matibabu.

Mkuu wa polisi wa eneo hilo, Ceasar Tusingwire alithibitisha tukio hilo.

"Watoto 13 kutoka familia moja wanashukiwa kwamba wamekula chapati zenye sumu. Walichanganya dawa ya kuua wadudu na mafuta ya kupikia kwa bahati mbaya," alisema Tusingwire na kuongeza:

"Walionusurika wanaendelea vizuri lakini bado hawajapata nguvu. Tunajitahidi kuhakiksha watoto wamerejea katika hali yao ya kawaida."

Polisi imesema miili ya waliokufa inafanyiwa uchunguzi na kuongeza kwamba upelelezi wa tukio hilo unaendelea.

***BBC***



Wauguzi wa afya nchini China wakimhudumia mgonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Maswali lukuki kifo cha mwimbaji injili

**KIGALI, Rwanda**

MASWALI kadhaa yameibuka baada ya kifo cha msanii wa nyimbo za injili nchini Rwanda, Kizito Mihigo, huku wananchi wakilinyooshea kidole Jeshi la Polisi.

Mihigo, alipatikana amefariki juzi katika chumba ambacho alikuwa anazuiliwa kwa muda wa siku tatu jijini Kigali, nchini Rwanda.

Jeshi la Polisi na Shirika la Upelelezi la Rwanda wanasema alijiua. Lakini baadhi ya watu, wanasema hoja hiyo sio ya kweli.

Mapema Jumatatu wiki hii mamlaka ilitangaza kwamba imeanzisha uchunguzi. Baada ya kutangazwa kifo cha Kizito Mihigo, watu wameendelea kutoa maoni mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii.

Kwenye mitandao ya kijamii ya Twitter na Facebook, wananchi wameendelea kuinyooshea kidole serikali ya Rwanda.

Baadhi ya wananchi hao akiwamo Alice Mutimukenye alisema: "Ni vigumu kuamini kwamba (...) mtetezi wa maridhiano nchini Rwanda hayuko tena katika ulimwengu huu, asante kwa mchango wako kwa ujenzi wa Rwanda. Kizito Mihigo pumzika kwa amani."

Mmoja wa wanasiasa wa upinzani nchini humo, Victoire Ingabire ambaye aliwahi kufungwa na kuachiwa huru mwaka 2018 aliandika: "Watu wenye tabia nzuri hufariki mapema. Ni jambo ambalo halieleweki."

Kifo cha Mihigo pia kimeleta simanzi kubwa kwa wanaharakati wa haki za binadamu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Shirika la Haki za Binadamu la Lucha limeelezea masikitiko yake kwa kifo cha msanii huyo kwa kusema: "Buriani Kizito Mihigo. Tutaendelea kukumbuka milele maneno yako ya haki na amani".

Baadhi ya watu wameishutumu serikali ya Rais Paul Kagame kwamba ndio ilimuua mwimbaji huyo maarufu, ambaye alinusurika katika mauaji ya halaiki yaliyotokea Rwanda mwaka 1994.

RFI

## Wezi wenye silaha wavamia, waiba 'toilet paper'

**HONG KONG, China**

WEZI waliokuwa na silaha mjini Hong Kong wameiba karatasi za chooni zenye thamani ya Dola za Marekani 130.

Kwa sasa Jiji la Hong Kong linakabiliwa na upungufu mkubwa wa karatasi hizo za kwenda chooni kwa sababu ya wasiwasi uliopo wakati mlipuko wa virusi vya corona ukiendelea.

Jeshi la Polisi mjini Hong Kong limesema wezi hao waliokuwa na visu walimvamia kijana aliyekuwa anazipeleka karatasi hizo nje ya duka moja.

Walisema wamewakamata wanaume wawili na kupata baadhi ya bidhaa zilizokuwa zimeibwa. Tukio hilo lilitokea katika eneo la Mong Kok, mjini Hong Kong Jumatatu.

Kulingana na taarifa za mashuhuda wa tukio hilo, wahalifu walimtishia kijana huyo wakati anashusha karatasi hizo ili kuziwasilisha katika duka kubwa la kufanyia manunuzi liitwalo 'Wellcome Supermarket'.

Kulingana na taarifa iliyotolewa karatasi zaidi ya 600 za chooni zimeibwa.

Maduka yaliyopo maeneo hayo yamekuwa yakishuhudia foleni ndefu za wateja punde tu bidhaa zinapowasilishwa kwa hofu ya kutokea kwa virusi vya corona ambako kutalazimisha watu kusalia majumbani.

Licha ya kwamba serikali imetoa hakikisho kwamba maeneo ambayo virusi vya corona bado havijatokea, yataendelea kupata huduma zao kama kawaida, wananchi wamekuwa wakinunua bidhaa kwa wingi ili kuzihifadhi.

Bidhaa nyingine za nyumbani kama vile mchele, tambi na vifaa vya kufanya usafi uhitaji wake umeongezeka maradufu.

**BBC**

# Mahakamani madai ya mauaji ya askari

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma, imeanza kusikiliza maelezo ya awali ya kesi inayowakabili washtakiwa 11 ya mauaji ya askari polisi wawili, mmoja kwa kukatwa sehemu za siri wakati wa operesheni ya kuwaondoa wavamizi wa maeneo ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Oktoba 18, mwaka 2018.

Washtakiwa hao kutoka wilayani Uvinza, wamefikishwa mahakami hapo wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kuua kwa kukusudia Inspekta Ramadhani Mdemu na Koplo Mohamed Zengo, wakati wa mapambano baina ya wananchi na askari eneo la Bulongore, kitalu namba 47.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiendeshwa na Wakili Mwandamizi Riziki Matitu na Happy Mayunga, huku upande wa utetezi ukiwa na mawakili watatu Sadiki Aliki, Raymond Kabuguzi na Ignatius Kagashe.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo, Wakili Matitu alidai washtakiwa walitumia silaha za jadi kama mikuki, mishale, fimbo na mapanga, kupambana na polisi kujeruhi na kuua kisha kukimbia.

Alidai kuwa washtakiwa wengine walikamatwa mkoani Tabora wakiwa wanajaribu kutoroka na wengine wakati wakipatiwa matibabu baada ya kujeruhiwa kwa risasi wakati wa mapambano.

Baada ya maelezo hayo Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Ivin Mugeta, aliwataka washtakiwa wote 11 kujibu mashaka hayo.

Washtakiwa wote walikana mashtaka na kueleza kuwa maelezo sahihi ni majina yao pekee.

Upande wa Jamhuri utawasilisha mashahidi 37 wakiwamo askari waliokuwa katika oparesheni hiyo, wananchi madaktari pamoja na vielelezo vinavyohusiana na tukio hilo.

Nao upande wa utetezi ulieleza kuwa utatumia ushahidi wa kimazingira kutokana na washtakiwa kutokuwapo eneo la tukio na kila mshtakiwa atawasilisha shahidi, kasoro mshtakiwa mmoja ambaye hana shahidi.

Jaji Mugeta aliahirisha kesi hiyo hadi Msajili wa Mahakama Kuu atakapopanga tarehe nyingine kwa ajili ya kusikiliza shauri hilo.




Mwendesha Bodaboda Nissa Mkimwa akiwa amempakia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, wakati wa uzinduzi wa huduma ya NMB MASTA BODA kwa Mkoa wa Ruvuma, Peramiho, wilayani Songea juzi. Waliosimama kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Benedicto Baragomwa na Meneja wa NMB Songea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani atimuliwa kikaoni kutokuwa na sare za CCM

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

DIWANI wa Nyida katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Seleman Segreti, ametolewa kwenye mkutano wa Halmashauri ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya pamoja na wajumbe wengine watatu kwa kutovaa sare za chama hicho.

Walitolewa nje jana na Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Wilaya ya Shinyanga, Emmanuel Lukanda, kabla ya kuanza kwa mkutano huo, ambao baadaye uliahirishwa.

Lukanda alisema walikubaliana wajumbe wote pale wanapokutana kwenye vikao vya chama wawe wanavaa sare za CCM, lakini alishangaa kuona wengine hawajavaa sare, jambo ambalo ni ukiukaji wa taratibu.

"Ndugu wajumbe tulikubaliana kila tunapokutana kwenye vikao vya chama tuvae sare za CCM, lakini hapa naona baadhi yenu hamjavaa...ambao hamjavaa hebu simameni na mtoke nje," aliamuru Lukanda.

"Baada ya mkutano kuisha mtaandika barua za kujieleza kwanini hamkuvaa sare za Chama Cha Mapinduzi CCM," alisema.

Diwani Segret alisema hakuvaa sare za chama sababu juzi alilala kwa mgonjwa Shinyanga Mjini, na kwamba hakurudi nyumbani kwa sababu ni mbali na kuamua kuingia hivyo hivyo kwenye mkutano.

Alisema amejisikia vibaya sana kuondolewa kwenye mkutano huo, huku akikiri kukiuka taratibu za chama, akidai haikuwa dhumuni lake bali ni dharura ilijitokeza.

## Mjane arejeshewa mali alizodhulumiwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

HATIMAYE mjane Magdalena Massao (40) jana alirejeshewa mali na shemeji yake ikiwamo nyumba na ardhi alizoachiwa yeye na wanawe wawili baada ya mumewe kufariki dunia.

Mali hizo alirejeshwa kwa msaada wa wasaidizi wa kisheria wakishirikiana na serikali ya Kijiji cha Mvuleni-Mji Mpya katika kata ya Mabogini, Wilaya ya Moshi.

Aidha, wajumbe wa serikali ya kijiji hicho waliagizwa na Mwenyekiti wa Kijiji, Joseph Meza pamoja na msaidizi wa kisheria wa eneo hilo, Michael Shayo, wazee na baadhi ya wananchi kukabidhi rasmi mali hizo kwa familia ya marehemu Adrian Massao.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa eneo hilo, mjane Magdalena alisema baada ya mumewe kufariki dunia mwaka 2016 na kumwachia watoto wawili, Getrude Massao (24) na Magreth Massao (12), shemeji yake (jina limehifadhiwa) alitoa amri ya kubomolewa makazi yao na kisha kuchukua mali zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo.

Kwa mujibu wa uongozi wa kijiji hicho, anayetuhumiwa kutaka kudhulumu mali za familia ya mjane huyo, hakuwa msimamizi wa mirathi.

"Alichukua mali zote na tulipomuuliza alisema zimeibiwa baada ya kubomoa, lakini cha ajabu alileta barua ya kutuzuia kufika katika kiwanja cha marehemu mume wangu na sasa amesema kuna eneo jingine katika Kata ya Rau Manispaa ya Moshi nalo atalitwaa ili ajenge makazi yake ya kudumu, alisema na kuongeza:

"Tumeomba msaada kijijini na kwa wasaidizi wa kisheria wa Moshi kuingilia kati na tunashukuru Mungu eneo la kwanza lililopo Mvuleni-Mji Mpya tumelikomboa na kukabidhiwa na kijiji."

Alisema ombi lake kubwa kwa sasa kwa serikali ya kijiji, wasaidizi wa kisheria na Wakili Elizabeth Minde ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Kwieco linalotoa msaada wa kisheria kuisaidia familia hiyo kupata hati ya kimila itakayowawezesha eneo hilo kutoingiliwa tena.

Awali Msaidizi wa Kisheria, Michael Shayo, aliyefanikisha kurejeshwa kwa mali za mjane huyo, alisema baada ya kuchunguza kwa makini na kufuatilia malalamiko ya familia hiyo uongozi wa kijiji pamoja na yeye walilitwaa eneo hilo na kulirejesha kwa mjane huyo Februari 16, mwaka huu.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME ãNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. MWENYE NYUMBA **0757 804 970**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA CRAZY HORSE FILMS LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **CRAZY HORSE FILMS LIMITED** yenye namba ya usajili 86920, iliyopo plot namba 115 Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2011 umeamua kuifunga Kampuni hiyo ambayo haijawahi kufanya shughuli yeyote hapa nchini.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA COASTAL RESORTS LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **COASTAL RESORTS LIMITED** yenye namba ya **usajili 60132,** iliyopo plot namba 115 Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2007 umeamua kuifunga Kampuni hiyo ambayo haijawahi kufanya shughuli yeyote hapa nchini.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA COASTAL LOGISTICS LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **COASTAL LOGISTICS LIMITED** yenye namba ya **usajili 66024,** iliyopo **plot namba 115** Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2008 umeamua kuifunga Kampuni hiyo ambayo haijawahi kufanya shughuli yeyote hapa nchini.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA BAOBAB DEVELOPMENTS LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **BAOBAB DEVELOPMENTS LIMITED** yenye Tin Namba **100-267-330** iliyopo **plot namba 924B** Chole road Kinondoni iliyosajiliwa mwaka 1988 umeamua kuifunga Kampuni hiyo **kutokana na sababu za kiuchumi.**

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA CTM TANZANIA LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **CTM TANZANIA LIMITED yenye Tin Namba 107-498-753** iliyopo plot namba **115** Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2008 umeamua kuifunga Kampuni hiyo kutokana na sababu za kiuchumi.

151635202

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FESTO CHEDEGO MACHELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC323 CAG. Chesis no. namba PJL07HT000647 na Engine no. PMI 157 FMT 17000647.

Yeyote ataeona atoe taarifa kituo Cha polisi. DOD/DOD/R-B/148453/2020

156364

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA CSI TRADING LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **CSI TRADING LIMITED** yenye **Tin Namba 102-512-472** iliyopo plot namba 115 Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2006 umeamua kuifunga Kampuni hiyo kutokana na sababu za kiuchumi.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA OSPREY SAFARI LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **OSPREY SAFARI LIMITED yenye Tin Namba 105-357-478** iliyopo plot namba 115 Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 2006 umeamua kuifunga Kampuni hiyo kutokana na sababu za kiuchumi.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA KILIMATITI CAMP LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **KILIMATITI CAMP LIMITED** yenye **Tin Namba 117-255-751 iliyopo plot namba 107** Coastal Building, Upanga road, iliyosajiliwa mwaka 2011 umeamua kuifunga Kampuni hiyo kutokana na sababu za kiuchumi.

151635202

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**KAMPUNI YA FISHERMAN'S COVE LIMITED**

Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya **FISHERMAN'S COVE LIMITED yenye Tin Namba 123-861-930** iliyopo plot **namba 115** Nyerere road iliyosajiliwa mwaka 1984 umeamua kuifunga Kampuni hiyo kutokana na sababu za kiuchumi.

151635202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA Usimamizi wa Mirathi NAMBA 19/2020

Ombi la JUMA ISSA MZALAU kuteuliwa

Msimamizi wa mirathi marehemu CHAUSIKU SALIMU MTUNGUJA

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 06/03/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wamarehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe14/02/2020

156367

## KUPOTEA KWA KADI

**Bartholomeo Mwambane Sanga** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI CANTER yenye namba ya usajili wa namba T 135 CRT iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: KBA/PS/B.I/29/VOL.XXIV

156360

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA HAKIMU MKAZI**
**S.L.P. 48**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**MULEBA MJINI.**

**KUMB. NO. SHAURI LA MADAI NO. 16/2020**

**BONIFACE BILABAYE @ERNEST.........MDAI**

**DHIDI YA**
**AWAZI NUHA .....................MDAIWA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Mdai Boniface Bilabaye @ Ernest alifungua shauri la madai dhidi ya mdaiwa Awazi Nuha. Mahakama ya Mwanzo Muleba Mjini ilikuwa ikitoa hati ya kuitwa shaurini kwa mdaiwa bila kufika mbele ya Mahakama.

Kwa tangazo hili mdaiwa Awazi Nuha anapaswa kufika Mahakamani tarehe 21/02/2020 juu ya shauri ambalo limefunguliwa dhidi yake mbele ya Mahakama.

156359

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAHAD IMRAN RAMADHANI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.0825-0041 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari MUDIO ISLAMIC SEMINARY mwaka 2012.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
DAR/MSI/RB/150891/2020

115633402

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

FLORAH TINUGA MKAZI WA IBINZAMATA MANISPAA YA SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YAKE YA KIWANJA NAMBA 155 KITALU '2' HD IBINZAMATA AMBAYO ILIPOTEA TANGU MWAKA 2018 MAENEO YA SHINYANGA

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA FLORAH TINUGA KWA SIMU NAMBA 0757463343 RB NAMBA SHY/RB/ 2020

215634402


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DEL PIERO AMUITA GUARDIOLA JUVE

**TURIN, Italia**

NYOTA wa zamani wa Juventus, Alessandro Del Piero amesema kwamba, Pep Guardiola atakwenda kuwa kocha wa mabingwa hao wa Italia.

Lakini, Juve watalazimika kupambana kweli kupata huduma ya raia huyo wa Hispania baada ya Guardiola mwenyewe kuwaambia marafiki zake kwamba ataendelea kubaki Manchester City msimu ujao.

Matumaini ya Juve kwenye kunasa huduma ya Guardiola yalipatikana baada ya Uefa kutangaza kuwafungia Man City kucheza michuano ya Ulaya kwa kipindi cha misimu miwili.

Del Piero alisema: "Huku Italia tayari kumekuwa na uvumi wa kuhusu kocha huyo na wachezaji wengine ambao watakuja Juventus. Watu wote kwenye soka wanaamini kwamba Juve watafanikiwa kumwiba kocha huyo kutoka Manchester City.

"Mwaka jana kulikuwa na mambo mengi kwamba anakuja Juventus, lakini hilo bado halijatimia."

Akizungumza kwenye tuzo za Laureus Sports huko Berlin, Del Piero aliongeza: "Kila klabu duniani ingependa kuwa na huduma ya kocha huyo na napenda kumwona Pep Italia.

"Ameshinda Hispania, Ujerumani na England. Kama atafuata njia zilizo sahihi basi naona anakoelekea ni Juve."

Kocha wa zamani wa Chelsea, Ruud Gullit naye anaamini kwamba, Guardiola atabadili timu mwishoni mwa msimu huu.

Man City sasa inapiga hesabu tu za kubeba ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu ambapo kwenye hatua ya 16-bora itakabiliwa na mtihani mzito wa kuikabili Real Madrid wiki ijayo.




## PSG YAANZA KUJIPANGA KUMSHAWISHI NEYMAR

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imeripotiwa kwamba inataka kuanza mazungumzo na Neymar kwa ajili ya kusaini mkataba mpya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barcelona kabla ya kuanza kwa msimu huu, lakini akaendelea kubakia hapo jijini Paris.

Baada ya mwezi uliopita kudaiwa kwamba Neymar anataka mkataba mpya na PSG, imeripotiwa mazungumzo bado hayajafanyika.

PSG na Neymar bado haijakutana kwa ajili yakujadiliana kuhusu kuongezwa mkataba mpya pale Le Parisien.

Neymar mwenye umri wa miaka 28, mkataba wake na PSG unamalizika 2022, lakini hakuna majadiliano yaliyofanyika hadi sasa.

Mshambuliaji huyo jana Jumanne alitarajiwa kurudi uwanjani kuichezea PSG kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya Borussia Dortmund.

## Bayern wafikiria kuachana na Sane

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich inafikiria kuachana na mpango wa kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho baada ya mchezo huo kubadili wakala.

Awali Bayern ilishafikia makubaliano binafsi na Sane, lakini kitendo cha kubadili wakala kinamaanisha kuwa pande hizo mbili zinatakiwa kurudi mezani na kuanza kujadili upya dili hilo.

Hicho kimewakera vigogo wa Bayern ambao wanafikiria kumpotezea Sane. Lakini wakati hayo yakiendelea Manchester City nayo inahaha kutaka kumfunga winga huyo na kwa kumpa mkataba mpya.

Mkataba wa Sane na Man City unaisha Juni 2021, kwa muda mrefu timu hiyo imekuwa ikihaha kumpa mkataba mpya, huku Bayern ikiwa inapambana kumng'oa kutoka Etihad.

Sane, staa wa kimataifa wa Ujerumani amekuwa akisakwa na Bayern Munich tangu dirisha la usajili la Januari 2019 na kwa muda mrefu alikuwa majeruhi hadi hivi karibuni alipoanza mazoezi mepesi ingawa Man City haijaweka wazi ni lini atarudi uwanjani rasmi.



# WENGER

## APIGILIA NYUNDO KIFUNGO MAN CITY UEFA

**LONDON, England**

ARSENE Wenger ameunga mkono adhabu iliyotolewa na Uefa kwa Manchester City kwa kuvunja sheria ya usawa wa matumizi ya fedha, lakini amebainisha kwamba, kunahitajika baadhi ya "mapinduzi" kwenye sheria hizo.

Ijumaa Uefa ilitangaza kwamba City imefungiwa kwa misimu miwili kushiriki michuano ya Ulaya na kulipa faini ya euro milioni 30 kwa kuvunja sheria hiyo ya manunuzi.

Klabu hiyo imethibitisha kwamba itakata rufani kwa Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo, CAS.

Na kocha huyo wa zamani wa Arsenal, Wenger pamoja na kukubaliana na adhabu hiyo, lakini anataka kufanyika kwa marekebisho kwa baadhi ya sheria hizo.

"Mara zote nilikuwa na utawala wa sheria za fedha. Klabu zinatakiwa kutumia fedha wanazozipata," alisema Wenger, ambaye anafanya kazi na Fifa kama ofisa maendelezo wa soka duniani.

"Nafikiri kunatakiwa kufanyika mapinduzi kwenye baadhi ya sheria. Maana kuna baadhi zinatakiwa kufanyiwa marekebisho."

# Lampard awalaumu wachezaji kichapo Utd

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amelaumu kikosi chake kwa kushinda kutumia nafasi baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Manchester United Jumatatu.

Mabao kutoka kwa Anthony Martial na Harry Maguire yalishuhudia Chelsea ikifikisha mechi ya nne kwenye Ligi Kuu bila kushinda.

Chelsea ambayo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo imeizidi pointi moja Tottenham, huku Man United iliyopo nafasi ya saba imeipita pointi tatu.

"Spendi kupoteza mchezo," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Sipendi namna tunavyopoteza mchezo kwa sababu tulikuwa na nafasi kubwa hasa tukiwa tunacheza nyumbani.

"Hatupati mabao ya kutosha kutoka eneo la washambuliaji. Tammy (Abraham) alikuwa na nafasi nzuri mwanzoni mwa msimu, sasa hatupati mabao ya kutosha. Hatupati mabao ya kutosha na huo ndio ukweli."

"Ni ngumu kushinda mechi. Unatawala mchezo kwa namna ile, lakini kwenye Ligi Kuu ya England si timu nyingi ambazo nyavu zake hazitikiswi kwa wiki."



# Pogba amgombanisha wakala wake na Solskjaer

**MANCHESTER, England**

MINO Raiola amemjia juu Ole Gunnar Solskjaer kwa kauli yake aliyoitoa juu ya Paul Pogba, akisema kiungo huyo si "mali" ya wakala wala kocha wa Manchester United.

Pogba mwenye umri wa miaka 26, amekuwa nje ya dimba kwa kipindi kirefu cha msimu huu wa 2019-20 akisumbuliwa na majeraha ya enka na ameendelea kuhusishwa na kutakiwa kuondoka Old Trafford.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 ambaye kwa mara ya mwisho alichezea Man United kwenye Boxing Day, alicheza dakika 45 kwenye ushindi wa United wa 4-1 dhidi ya Newcastle.

Solskjaer Jumatatu kabla ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Chelsea alisema: "Paul ni mchezaji wetu na si wa Mino.

Jioni ya Jumatatu wakala huyo wa Pogba, Raiola alijibu kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram akisema: "Paul si wakwangu na kwa uhakika kabisa si mali ya Solskjaer, Paul ni Paul Pogba.

"Sijakaa naye chini na kumwambia Paul amwambie wakala wake nini cha kusema. Na sijawahi kuzungumza na Mino, huo ndio ukweli."

"Lakini kabla Solskjaer hajasema chochote kuhusu vitu nilivyosema anatakiwa kwanza ajihakikishie mwenyewe nini anatakiwa kusema.

"Mimi ni raia huru ambaye naweza kufikiri na kuelezea mawazo yangu. Hadi sasa pengine nilikuwa mtu mzuri kwake. Solskjaer anatakiwa kukumbuka vitu alivyosema kuhusu Paul wakati wa kipindi cha majira ya joto. "Nafikiri pengine Solskjaer amedanganywa kwa sababu tofauti na sasa haelewi nini anachopaswa kukisema."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUENDOUZI AMTIBUA ARTETA, AMFUNGUKIA

●●●Wachezaji ambao wanafanya mazoezi vizuri, wanajiheshimu vizuri, huchaguliwa...

**LONDON, England**

MPASUKO uliojitokeza na Mikel Arteta, Arsenal ilipokuwa kambini Dubai wakati wa mapumziko ya majira ya baridi, umemgharimu Matteo Guendouzi kupata nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza dhidi ya Newcastle United, gazeti la Telegraph limeeleza.

Hata hivyo, kukosekana kwake hakukuweza kuiathiri 'Gunners', ambayo ilionyesha kiwango bora katika kipindi cha pili na kufanikiwa kufunga mabao 4-0, na kujizatiti katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Matokeo hayo yameonyesha kuwa mafunzo waliyoyapata kipindi cha mapumziko ya majira ya baridi yamelipa gawio, na ushindi huo ukiwa moja ya viwango bora kabisa kutoka kwa Arsenal msimu huu.

Arteta alilenga kutumia mapumziko hayo ya majira ya baridi kama fursa ya kuwajua vizuri wachezaji wake na pia kuwatengeneza katika falsafa zake. Wakati wakipata mafanikio makubwa wakiwa huko, inaonekana kwamba pia kulikuwa na wakati wa kutofautiana katika kambi hiyo.

Sasa imeanikwa kwamba Guendouzi alikuwa na hoja na Arteta kwenye uwanja wa mazoezi wakati wa mapumziko ya msimu wa baridi na hoja hizo ziliongezeka baadaye katika hoteli ya timu hiyo jioni.

Na hatimaye ilimsababishia Mfaransa huyo kukosekama katika kikosi kilichocheza Jumapili, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwake kutokea msimu huu.

Guendouzi alijiunga na Arsenal akitokea Lorient ya Ufaransa mwaka 2018 na licha ya ukinda wake, haraka aliweza kujiimarisha mwenyewe kama memba wa kikosi cha kwanza. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, tayari ameshaichezea Gunners zaidi ya mechi 50 na ana moto ndani yake ambao haujatambuliwa hadi sasa.

Hata hivyo, kocha huyo raia wa Hispania, Arteta pamoja na benchi lake la ufundi hawakuvutiwa kabisa na tabia na mtazamo wake huko Dubai jambo lililosababisha kutofautiana kwenye uwanja wa mazoezi.

Arteta hapo awali alikiambia kikosi chake kuwa ilikuwa juu yao kuishi kulingana na matarajio yake na wachezaji wote walishangazwa na kufurahishwa na mbinu zake kali.

Mhispania huyo pia ametoa umuhimu mkubwa kwa tabia ya mchezaji tangu achukue jukumu la kuinoa timu hiyo na hata alikiri Jumapili kwamba Dani Ceballos alikuwa hajaanza mapema kwa sababu kulikuwa na masuala kadhaa na tabia yake.

Hata hivyo, baada ya ushindi huo dhidi ya 'Magpies', Arteta alisema ulikuwa uamuzi wa kimbinu kumwacha nje Guendouzi, lakini akafunguka kwamba kulikuwa na suala la kinidhamu na mchezaji huyo.

Alipoulizwa moja kwa moja sababu ya kukosekana kwa Mfaransa huyo, haya yalikuwa majibu yake: "Sababu ni kwamba wachezaji ambao kwa maoni yangu, wanafanya mazoezi vizuri, wanajiheshimu vizuri na wanaotumika zaidi kutoa kile tunachotaka uwanjani, ni wachezaji ambao huchaguliwa."

## KWA UFUPI

**SPURS, EVERTON KWA SMALLING**
Tottenham na Everton zinavutiwa na beki wa Manchester United, Muingereza Chris Smalling, 30, ambaye anaichezea Roma kwa mkopo. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

**WENGER AFUNGUKA KIFUNGO CITY**
KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amesema "sheria zipo na lazima zitekelezwa" wakati alipoulizwa kuhusu Manchester City kufungiwa miaka miwili kushiriki michuano ya Ulaya, akaongeza: "Siwezi kusema kama adhabu ni kubwa sana ama ndogo sana." ***(Gazzetta dello Sport)***

**YAYA TOURE KUTUA BOTAFOGO**
KLABU ya Botafogo ya Brazil inatarajia kukamilisha usajili wa kiungo wa zamani wa Manchester City, Yaya Toure, 36, leo ama kesho. ***(Globo Esporte - in Portuguese)***

**WERNER AMPAGAWISHA KLOPP**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anaendelea kuvutiwa na Timo Werner, lakini 'Wekundu' hao bado hawajafanya makubaliano na RB Leipzig kuhusu mshambuliaji huyo raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 23. ***(Independent)***

**STERLING AJILIPUA MAN CITY**
MSHAMBULIAJI wa England, Raheem Sterling, 25, amejitolea kubaki Manchester City licha ya klabu hiyo kufungiwa kushiriki michuano ya Ulaya, amesema wakala wake. (Manchester Evening News)

**BARCA KUMUIBUKIA BRAITHWAITE**
Barcelona inajiandaa kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Middlesbrough, Mdenmark Martin Braithwaite, 28, kutoka Leganes kwa dili la dharura. ***(Mundo Deportivo, via Teeside Gazette)***

**SOUMARE AZIVUTA UTD, LIVER**
KOCHA wa Lille, Christophe Galtier amesema kuna mvutano kati ya klabu na kiungo Mfaransa Boubakary Soumare, 20, anayewinda na Manchester United, Liverpool na Chelsea. ***(Express)***

**CITY KUENDELEA KUULA PUMA**
Manchester City haitakabiliwa na kupuunzwa kwa dau lao la pauni milioni 65 kwa msimu la udhamini wa jezi kutoka Puma hata kama kufungiwa kwao kwenye michuano ya Ulaya hakutaondolewa. ***(Mail)***

**KING KIDUCHU ATUE UNITED**
Manchester United iliiambia Bournemouth kwamba ilikuwa na dakika 15 kabla ya siku ya mwisho ya usajili kufungwa kukubali ofa ya pauni milioni 25 kwa straika wao, Mnorway Joshua King, 28, ama ingemsajili mchezaji kutoka China. ***(The Athletic)***

**SOUTHAMPTON, BURNLEY VITANI**
Southampton na Burnley ni miongoni mwa klabu kibao za Ligi Kuu England zinazovutiwa kumsajili beki wa Oxford United, Rob Dickie, 23. ***(Football Insider)***

**AJAX KUPOTEZA 8 KIANGAZI**
Ajax inaweza kukabiliwa na vita ya kuwapoteza wachezaji wake nane katika dirisha la usajili wa majira ya joto lijalo. ***(The Athletic)***

**UBAGUZI TATIZO URENO - AMORIM**
KOCHA wa Braga, Ruben Amorim amesema ubaguzi wa rangi pia ni tatizo katika jamii za Kireno, wakati akijibu kitendo cha kubaguliwa kwa mshambuliaji wa Porto, Moussa Marega. ***(A Bola - in Portuguese)***

## HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS YAONJA MACHUNGU UNAF

**Na Somoe Ng'itu, TUNISIA**

BAADA ya kushinda mechi mbili mfululizo kwenye michuano ya Kombe la UNAF, hatimaye Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imeonja machungu na kujiweka katika mazingira magumu ya kutwaa ubingwa huo kufuatia kukubali kipigo cha mabao 3-2 dhidi ya Morocco katika mchezo uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Kram jijini Tunis nchini hapa.

Kwa matokeo hayo, Twiga Stars imeendelea kukaa kileleni ikibaki na pointi sita sawa na Morocco, lakini ikiwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

Mwanahamisi Omary "Gaucho" alikuwa wa kwanza kuipatia Twiga Stars bao la mapema katika sekunde ya 20 ikiwa ni la tano kwenye michuano hii na kuwachanganya wapinzani wao Morocco ambao wananolewa na kocha kutoka Marekani.


Morocco walisawazisha bao hilo dakika ya nane kwa penalti kupitia kwa Addi Nourimane baada ya mchezaji wao kufanyiwa faulo na Happiness Hezron ndani ya 18 huku sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko Mssoudy Sanaa akiwafungia Wamorocco hao bao la pili.

Hata hivyo, Twiga Stars ilibakia pungufu baada ya Happiness kuonyeshwa kadi nyekundu ikiwa ni njano ya pili kutokana na kumchezea faulo Sanaa aliyekuwa anaelekea kufunga.

Dakika ya 67 Sanaa aliifungia Morocco bao la tatu lililowapa ushindi huku kiungo Diana Msewa akifunga bao la pili kwa Twiga Stars.

Katika mechi ya mapema jana, Algeria ilipata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Mauritania na kurejea katika kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa wa michuano hiyo.

Mashindano hayo yataendelea tena kesho kwa Algeria kuivaa Tunisia huku Morocco wakiwakaribisha Mauritania wakati Twiga Stars yenyewe itakuwa haina mchezo, ikisubiri kucheza mechi ya mwisho dhidi ya wenyeji Tunisia hapo Jumamosi.



Mshindi wa Sh. milioni 437.6/- za Jackpot ya SportPesa, Yassin Ridhiwani (kulia), akimwonyesha Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Sportpesa Tanzania, Tarimba Abbas, daftari alilotumia kuweka kumbukumbu ya michezo yake ili kuhakikisha anabashiri kwa usahihi. **PICHA: SPORTPESA**

# Simulizi mshindi mil. 437/- za SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni wiki moja imepita baada ya mshindi wa Jackpot ya SportPesa kutoka Ubungo jijini Dar es Salaam, Yassin Ridhiwani kukabidhiwa kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 437 kufuatia kubashiri kwa usahihi mechi 13, amesimulia namna alivyoshinda wakati akitoa shukrani zake kwa Kampuni ya SportPesa kumkabidhi kitita chake bila longolongo.

Akizungumzia na mwandishi wetu jana, kwanza Ridhiwani aliishukuru SportPesa kwa kuwa wakweli kutokana na kumlipa kiasi alichoshinda bila usumbufu, na kisha akasema kawaida yake huweka kumbukumbu ya michezo katika daftari ili kumsaidia kubashiri kwa usahihi.

Ridhiwani ambaye alishinda Sh. milioni 437.6 alisema: "Mbinu niliyotumia kushinda ni kuweka mikeka kwenye daftari. Hii inasaidia sana kwani inaweka kumbukumbu ya michezo iliyopita. Na mara nyingi huwa nabashiri kuanzia saa saba usiku wakati familia yangu ikiwa imelala.

"Nilipokuwa nafuatilia matokeo, mechi ya mwisho ilikuwa ni Brescia dhidi ya Udinese ambayo niliweka droo, hadi kufika dakika ya 80 Brescia ilikuwa inaongoza 1-0 kwa kweli nilivurugwa kabisa, nikiamini kuwa nitaishia mechi 12. Ila amini usiamini dakika ya 92 Rodrigo De Paul anafunga goli la kusawazisha, kwanza nilitupa simu chini na chozi lilinitoka, yaani nililia kilio cha furaha. Sikuamini kama nimeweza kubutua mechi zote 13."

Aliongeza: "Kwanza, namshukuru Mungu kwa ushindi huu nilioupata wa peke yangu kwani wachezaji tupo wengi sana ila nimeweza kuibuka na ushindi huu, sijagawana na mtu. Na tayari fedha zangu nimeshakabidhiwa."

Kuhusu malengo aliyojiwekea baada ya kupokea kitita hicho, alisema: "Katika maisha yangu nimekuwa na ndoto kuwa siku nikipata pesa nyingi basi niwajengee watoto wangu ghorofa na kwa pesa hii niliyopata nitaifanyia kazi kwa bidii na umakini ili nifikie malengo yangu ya kuwajengea wanangu ghorofa.

"Malengo mengine ni kuwahamisha watoto wangu kutoka shule za kawaida na kuwapeleka shule za kimataifa. Pia kuboresha biashara yangu ya kuuza mitumba niwe naingiza mabalo ya mitumba kwa jumla. Baada ya kuhakikisha biashara yangu ya mitumba imesimama, nitahamia kwenye kilimo na ufugaji. Hii pesa ina malengo makubwa ambayo namuomba Mungu anisaidie niiyatimize."

Aidha, Ridhiwani aliwashauri Watanzania kucheze na SportPesa kwa kuwa si wababaishaji. Nimepata ushindi huu Jumapili iliyopita na tayari fedha zangu nimekabidhiwa zipo kwenye akaunti yangu ya benki.

"Hivyo, nawaaminisha watu wote wanaocheza au wanatamani kucheza na SportPesa wasisite, SportPesa ni waaminifu wanakupa pesa yako bila usumbufu, kumbuka kwa shilingi 2,000 tu ndizo zimeniingizia zaidi ya milioni 437, unasubiri nini kuwa mshindi wa wiki hii?" Alihoji.

Jackpot ya SportPesa kwa sasa imefikia Sh. 203,654,480 na unatakiwa kubashiri kwa usahihi mechi 13 ili kushinda, lakini pia unaweza kupata bonasi endapo utapatia kwa usahihi mechi 10, 11 na 12.

# Azam, Ndanda FC hakuna kulala leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Azam FC leo itakuwa na kibarua kigumu, itakapokuwa ugenini kumenyana na Ndanda FC kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara katika mfululizo wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Azam inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza michezo yao ya nyumba ambapo ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Coastal Union wiki iliyopita.

Huku Ndanda wenyewe wakishinda kwa bao 1-0 ugenini walipokutana na Singida United katika Uwanja wa Namfua ambao kwa sasa umebadilishwa jina na kuitwa Liti.

Timu zote hizo zinahitaji alama tatu muhimu ili kila mmoja kujiweka katika nafasi nzuri, huku Azam wakipambana kutafuta nafasi ya kupanda katika nafasi ya kwanza na Ndanda kujinusuru katika kushuka daraja.

Kocha Msaidizi wa Azam, Idd Nassor Cheche ameliambia Nipashe kwamba bado wanapambana kwa ajili ya mechi zinazofuata na leo wanaingia kutafuta alama tatu muhimu dhidi ya wenyeji wao Ndanda.

Alisema wanatambua ugumu wa mechi za ugenini pia wana heshimu wapinzani wao, kwa hatua ya ligi waliofika hawana muda wa kupoteza kuhakikisha wanarejea Dar es Saalam na alama muhimu.

**"Tumekuja kutafuta alama muhimu, hivyo tunaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa, wachezaji wanatambua kwamba mpira ni sehemu ya makosa, yale tuliyokosea tumefanyia kazi ili tufanye vizuri," alisema Cheche.**

Naye Kocha Mkuu wa Ndanda, Meja mstaafu Abdul Mingange alisema ushindi walioupata Singida umewatia hasira ya kurejea nyumbani kutafuta alama tatu kutoka kwa wenyeji wao Azam.

"Tuko katika nafasi ya 15 katika msimamo hii si sehemu salama kwetu, hivyo tayari nimeongea na wachezaji wangu na wanatambua kwamba tunahitaji kujituma ili kubaki na alama tatu katika uwanja wa nyumbani," alisema Mingange.

# Michezo

Jumatano Februari 19, 2020

Nipashe




## Guendouzi amtibua Arteta, amfungukia

HABARI UK 30

LA PILI...



Harry Maguire (Jezi Na.5) akiutendea haki mpira wa kona kutoka kushoto uliyopigwa na Bruno Fernandes, na kuuzamisha kimyani kwa kichwa kwenye mechi ya Ligi Kuu England wakati Manchester United ikishinda 2-0 ugenini dhidi ya Chelsea juzi. **HABARI UK. 29**

# WAMESHIKWA TENA

## ●●●Ni Yanga mikononi mwa Polisi, hiyo ikiwa sare ya tatu mfululizo, Namungo yaishusha hadi...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mzunguko wa kwanza kulazimishwa sare ya mabao 3-3 jijini Dar es Salaam, hatimaye timu ya Polisi Tanzania imeishika tena pabaya Yanga kwa kutoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi jana.

Matokeo hayo yanafanya bundi wa sare kuendelea kutawala mtaa wa Twiga na Jangwani kwani hiyo ni ya tatu mfululizo kwa miamba hiyo inayopiga hesabu ya kuwashusha watani zao, Simba kileleni.

Ushindi wa mwisho Yanga ulikuwa Februari 8, mwaka huu, ilipoichapa Ruvu Shooting bao 1-0, lakini baada ya hapo ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City, kabla ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Tanzania Prisons, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Bao la dakika ya 71 lililofungwa na straika hatari wa Polisi Tanzania, Sixtus Sabilo liliinyima Yanga pointi tatu kwenye mechi hiyo ambazo zilionekana kuelekea Jangwani.

Straika huyo ambaye alifunga bao lake la tano kwenye orodha ya wafungaji msimu huu, alijitwisha mpira wa kona na kumuacha kipa Farouk Shikalo akiruka bila mafanikio.

Dakika nne tu zilizopita, Marcel Kaheza alikuwa ameifungia Polisi Tanzania bao, lakini lilikataliwa kwa madai ya mchezaji huyo kucheza madhambi kabla hajaukwamisha wavuni. Yanga ilitangulia kupata bao kipindi cha kwanza kwenye dakika ya 40, kupitia kwa straika wake Tariq Seif kwa kichwa, baada ya kutokea purukushani kwenye lango la Polisi Tanzania.

Ni straika huyo huyo aliyeikosesha Yanga bao dakika ya 33, baada ya kushindwa kuugusa mpira ili utinge wavuni, lakini dakika saba baadaye alisawazisha makosa yake.

Katika mechi hiyo, Yanga ilitawala zaidi kipindi cha kwanza na kumuweka matatani kipa Mohamed Yusuph mara kwa mara, lakini Polisi Tanzania nayo ilimiliki kipindi cha pili na kama ingekuwa makini ingeweza kuondoka na ushindi.

Bernard Morrison na Ditram Nchimbi wangeweza kuipatia Yanga mabao dakika ya 13, na 21 na kuimaliza mechi, lakini hawakuwa makini walipokuwa mbele ya lango.

Kwa matokeo hayo, Yanga imeshuka hadi nafasi ya nne, licha ya kwamba imepata pointi moja na kufikisha 40, huku Polisi Tanzania ikikamata nafasi ya nane kwa pointi zake 34.

Hii ni baada ya Namungo FC kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC, hivyo nayo kufikisha pointi 40, lakini ikiwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa kuliko Yanga.

Hata hivyo Yanga imecheza mechi 21, huku Namungo ikiwa imeshuka dimbani mara 22.

Matokeo mengine ya mechi za jana, Coastal Union ikiwa nyumbani Uwanja wa Mkwakwani, imechapwa mabao 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting, JKT Tanzania na Biashara zikitoka sare ya bila kufungana, Mbao FC nayo imezinduka usingizini ikiwa nyumbani CCM Kirumba kwa kuichapa Singida United mabao 3-1, Mbeya City ikiwa Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, ikiiadhibu Lipuli mabao 2-1.

# Ndayiragije afurahia kundi la Stars CHAN

**Na Saada Akida**

WAKATI Tanzania ikiangukia Kundi D pamoja na Zambia, Guinea na Namibia kwenye fainali za kuwania Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema hana hofu na timu ambazo wamepangwa nazo na kinachotakiwa kwa sasa ni kuhakikisha wanafanya maandalizi mazuri.

Katika droo iliyopangwa jijini Yaounde Cameroon juzi usiku ya michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Aprili 4 hadi 25, mwaka huu, wenyeji hao wamepangwa Kundi A pamoja na Zimbabwe, Mali na Burkina Faso huku washindi mara nyingi zaidi wa michuano, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambao wamebeba kombe hilo mara mbili, wao wakiangukia Kundi B pamoja na jirani zao, Kongo Brazaville, mabingwa wa 2014, Libya na Niger.

Mabingwa watetezi, Morocco wao wamepangwa Kundi C pamoja na Togo watakaoshiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza, Rwanda na Uganda.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Ndayiragije alisema timu ambazo wamepangwa nazo si za kutisha kama ambazo Stars ilikutana nazo kwenye michuano ya Afcon 2019, hivyo anachohitaji ni kuandaa kikosi chake kwa umakini.

Alisema kutokana na timu walizopangwa nazo, hajaona jina kubwa ambalo linaweza kuwafanya Watanzania kuhofia kikosi chao, huku akiamini katika maandalizi mazuri na wachezaji kujituma.

"Ukiangalia kundi letu hakuna jina kubwa sana ambalo tumepangwa nalo, hivyo tunatarajia kuingia kambini Machi 12, mwaka huu kwa ajili ya maandalizi ya michuano hiyo," alisema Ndayiragije.

Chini ya Ndayiragije, Stars imefuzu CHAN ya mwaka huu baada ya kuzitoa Kenya na Sudan, hiyo sasa ikiwa ni mara ya pili kwa Tanzania kushiriki fainali hizo tangu 2009 iliposhiriki kwa mara ya kwanza nchini Ivory Coast.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >